

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA NNE**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 27 Januari, 2009**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatuh Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

Waheshimiwa Wabunge katika mkutano wa Kumi na Tatuh wa Bunge tulipitisha Miswada saba ya Sheria ya Serikali ifuatayo: *The Contractors Registration Amendment Bill , 2008, The Unity Titles Bill 2008, The Mortgage Finance Special Provisions Bill 2008, The Height Skins Bill, 2008, The Animal Welfare Bill 2008, The workers Compensation Bill 2008 na The Mental Health Bill 2008.*

Baada ya kuitishwa na Bunge Miswada hiyo iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais ili kama inavyohitaji Katiba yetu ipate kibali chake. Kwa taarifa hii nawaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari Mheshimiwa Rais amekwishatoa kibali chake na sasa Miswada hiyo ni sheria za nchi na sasa inaitwa *The Contractors Registration Amendment Act, 2008 Na. 15 ya mwaka 2008, The Unit Titles Act, 2008 Na. 16 ya 2008, The Mortgage Finance Special Provisions Act, 2008 Na. 17 ya mwaka 2008 The Height Skins and Leather Trade Act, 2008. Kwa hiyo, ni sheria Na. 18 ya Mwaka 2008. The Animal Welfare Act 2008 Sheria Na. 19 ya mwaka 2008 na The Mental Health Act 2008 Sheria Na. 21 ya mwaka 2008 huu ndiyo mwisho wa taarifa.*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA):-**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita muuliza swali la kwanza napenda nisimame kuwatachia heri ya mwaka mpya ya 2009. (*Makofi*)

Na. 1

**Matumizi ya Lugha ya Kiingereza Bungeni**

**MHE. MARTHA MOSSES MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Bunge letu linaendesha vikao vyake kwa lugha ya Kiswahili; na kwa kuwa, sio Wabunge wote wenye uwezo wa kufahamu vizuri lugha ya Kiingereza:-

(a) Je, kuna sababu gani kwa viongozi wa Afrika Mashariki kuzungumza na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lugha ya Kiingereza?

(b) Je, viongozi hao wanafahamu kuwa Wabunge wengi hawaelewi Kiingereza na wala siyo lugha yetu?

(c) Je, kwa nini Bunge linapopata wageni wasiofahamu lugha ya Kiswahili kusiwekwe Mkalimani ili Wabunge wasikie kirahisi kinachosema na wageni hao?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, lenye (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lugha rasmi zinazozungumzwa na zinazoelewka kwa wananchi walio wengi katika Ukanda wa Afrika ya Mashariki ni Kiswahili na Kiingereza.

Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 144(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007 imetamka kwamba, Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa Lugha ya Kiswahili au Kiingereza na kwa sababu hiyo, Viongozi wa Afrika Mashariki wanapozungumza na Wabunge na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana hiari ya kuchagua kuzungumza kwa kutumia mojawapo ya lugha hizo mbili.

Kigezo cha msingi ni lugha ipi viongozi hao wanaimudu kuizungumza kwa ufasaha kwa ajili ya kufikisha ujumbe wanaotaka kuutoa kwa Wabunge. Inawezekana kabisa sababu inayowafanya viongozi hao watumie Lugha ya Kiingereza ni kwamba, wanaona Kiingereza ni lugha wanayoimudu kuizungumza kwa ufasaha zaidi kuliko Lugha ya Kiswahili.

(b) Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Wabunge wengi hawaelewi Kiingereza na wala siyo kweli kuwa "hiyo si lugha yetu." Ibara ya 67(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sura ya 2, Toleo la 2007 imeweka mojawapo ya sifa za

mtu kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge ni kujua kusoma na kuandika katika Kiswahili na Kiingereza. (Makofi)

Aidha, kuweka Kiingereza katika Kanuni za Bunge kama moja ya lugha rasmi Bungeni inayoweza kutumika inadhihirisha kwamba, Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanao uelewa mzuri kabisa wa lugha hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, Ibara ya 144(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 inatamka wazi kwamba, Shughuli za Bunge zitaendeshwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza bila ya tafsiri ya lugha hizo kutolewa. Hiyo ndiyo sababu iliyofanya pasiwepo na mkalimani wa kutafsiri hotuba za viongozi Bungeni hadi sasa. Hata hivyo Ofisi ya Bunge ina mkakati wa kuweka vifaa maalum vyta kutafsiri pale Bunge linapopata mgeni asiyefahamu ama Luga ya Kingereza au Luga ya Kiswahili kama ilivyotokea katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lilipotembelewa na kuhutubiwa na Rais wa Visiwa vya Comoro.

Mwisho, kwa kuwa sasa dunia ni kama kijiji kimoja kutokana na maendeleo katika teknolojia ya mawasiliano, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge amba wanalo tatizo la kuielewa lugha hii ya Kiingereza kuweka juhudini za makusudi za kujifunza lugha hiyo ili waweze kufahamu masuala mbalimbali yanayoendelea duniani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaruhusu swali la nyongeza naomba radhi nilighafilika nawaomba tusimame kwa dakika moja kumkumbuka mwenzetu Mheshimiwa Marehemu Richard S. Nyaulawa.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja kumbuka Marehemu Richard S. Nyaulawa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Sasa tunamwomba Mwenyezi Mungu mwenye rehema zote aweze kuiweka roho ya Marehemu mpandwa wetu Richard Nyaulawa mahali pema peponi. Amina.

**MHE. MARTHA MLATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri mimi nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa nchi nyingi zilizoendelea hapa duniani zinaheshimu na kutukiza lugha zao za kitaifa na hata ukifika kwenye mikutano yao hutumia lugha zao hata kama wanajua Kingereza. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa kuitkuza lugha ya Kingereza haoni kwamba anadidimiza na kuidharau lugha ya Kiswahili?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amekiri kwamba anatambua upungufu uliopo kwa sisi Wabunge katika kuizungumza vizuri kwa ufasaha lugha ya Kingereza na ndiyo maana Bunge limetambua umuhimu wa kuweka vifaa

maalum ili tuweze kuwasikiliza kwa ufasaha na kwa undani wageni wanapoingia hapa Tanzania au Bungeni? Vifaa hivyo vitawekwa lini? ahsante. (Makofi)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lazima nikiri kwamba Tanzania pia inaheshimuna kuitukuza sana lugha ya Kiswahili. Jithada hizi ziko wazi, sasa hivi lugha ya Kiswahili ni lugha mojawapo katika lugha ambazo zinatumika Umoja wa Afrika (*African Union*). Tanzania ni kitovu cha Kiswahili kwa vyuo vingi Duniani. Kwa hiyo, kwa upande huo hakuna shaka hata kidogo.

Turejee Bungeni, kila nchi ina historia yake. Historia yetu katika kuandika sheria na kuendesha shughuli za Bunge zinatokana na kuwa Mjumbe au mwanachama wa Jumuiya ya Madola. Miswada yetu yote inaandaliwa kwa Kingereza. Katika Jumuiya ya Madola hawa wanaoandaa Miswada wanafunzwa kwa pamoja na Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. Katika nchi zote zaidi ya 53 za Jumuiya ya Madola hamna ambayo imeweza kuandaa waandishi wake wa sheria. Waandishi hawa wanaoandaa sheria za Bunge wanaandaliwa kwa pamoja ikiwa ni pamoja na wale wa Kitanzania na uandishi wa sheria ni taaluma maalum.

Hivyo ni vema Wabunge kuelewa vizuri Kiingereza ili waweze kutafakari vizuri Miswada inayoletwu hapa Bungeni. Ni mpaka hapa ambapo tutakapokuwa na uwezo wataalam wetu wakawa na uwezo wa kuandaa Miswada ya Sheria ndiyo tunawenza tukawa tunatumia Kiswahili moja kwa moja hapa Bungeni. Nimesema kwamba tafsiri ambayo tunaiongelea vyombo tunavyoongelea tunatafsiri hapa Bungeni ni kwa wale viongozi ambao hawafahamu ama Kiswahili au Kingereza. Hatuna haja ya kutafsiri Kingereza. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 2

### **Vigezo vya Upandishaji Hadhi Miji**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kigezo cha ukubwa wa eneo kati ya vigezo vinavyotumika kupandisha hadhi Makao Makuu ya Wilaya kuwa Miji au Mji Mdogo kwa sehemu za milimani kama vile Lushoto si sahihi au kuwe na tofauti na maeneo ya tambarare?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upandishaji hadhi eneo la utawala ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na mamlaka ya Mji Mdogo au Mji hufanywa kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na.7 na (Mamlaka ya Miji) Na.8 za mwaka 1082. Pamoja na Sheria hizo ndivyo vigezo maalum ambavyo havijatofautisha ukubwa wa eneo kwa sehemu za milimani au tambarare.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitangaza eneo la Kata ya Lushoto lenye vijiji 7 kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lushoto kufuatia Tangazo la Serikali (*GN*) Namba 353 la tarehe 17 Septemba, 2004. Eneo hilo ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilikwisharidhia uamuzi wa Serikali na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lushoto imepewa Hati ya kuanzishwa kwake mwezi Januari, 2008 na imeanza utekelezaji wa majukumu yake ya Kisheria.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza uamuzi huo wa Serikali, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imejumuisha Kata ya Ubiri ambayo haikuwepo kwenye Tangazo la Serikali. Kitendo hicho cha Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ni kinyume na utaratibu unaozielekeza Halmashauri kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, hitaji la kuongeza, au kupunguza eneo lililotangazwa limejitokeza katika baadhi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutohana na mahitaji hayo, Serikali imeanza mchakato wa kuvipitia upya vigezo vilivyopo na Sheria inayohusika katika kuanzisha Mamlaka za Miji Midogo ikiwa ni pamoja na kigezo cha ukubwa wa eneo ili kuondoa matatizo yanayojitokeza mara kwa mara.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa vile ni vizuri kuwa na Makao Makuu ya wiliaya yaliyopangwa vizuri. Je, serikali iko tayari kufanya yale yanayowezekana ikibidi kurekebisha sheria ili makao makuu ya wilaya nchini yaye mamlaka za miji?

Ukichukuwa mji kama Lushoto, ambao sasa umejumuisha Kata 2 na vijiji 16 utakuta wakazi wengi wa maeneo hayo ni wakulima na wafugaji wanaotegemea kilimo. Sheria hii ya mwaka 1982, nadhani haitambui kama sijakosea, haitambui uwepo wa mashamba na maeneo ya mifugo katika maeneo ambayo yametamkwa kuwa mamlaka ya Mji mdogo. Je, serikali iko tayari kushirikiana na wananchi wa wilaya ya Lushoto ili kurekebisha kasoro hizo za kisheria ili mamlaka za miji midogo zitambue kuwepo na mashamba ndani ya mji mdogo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa wazo la kuwa na mji mdogo inasisitiza hicho anachosema cha kuwa na mpango. Au atasema kwamba eneo hili sasa tuna kubali liwe ni eneo la mji mdogo, maana yake unachosema pale ni kwamba unasema kwamba uwe ni mji ambao umepangwa liwe ni eneo limepangwa ambalo halitakuwa na watu wanapoketi kule ndani wakajijengea hovyo hovyo. Kwa hiyo, wazo hili ambalo liko katika Wilaya ya Lushoto ni wazo ambalo linakusudia kuona hilo.

Swali la pili Mheshimiwa Balozi Mshangama anataka kujuu kama sisi tutakuwa tayari kuruhusu kuwepo kwa mashamba na wakati huo huo kuwa na mifugo katika eneo ambalo limepangwa. Kinachozungumzwa hapa sasa ni mahusiano ya uzalishaji mali katika eneo lile, ukiruhusu kwamba kutakuwa kuna mashamba katika miji humo humo na ukaruhusu kwamba kutakuwa kuna mifugo humo humo hutatakiwa utuambie pia kwamba unaweka utaratibu gani katika kuweka mifugo na mashamba katika eneo hilo.

Mimi najua anachozungumza Mheshimiwa Mshangama ni kwamba ipo haja ya kuangalia kila eneo kufuatana na hali halisi iliyopo katika eneo lile. Jambo hili siwezi kulitoleaa majibu hapa ni jambo ambalo tunaweza tukakaa naye tukamsikiliza kujuu kwamba tunatakuwa kufanya nini kwa sababu unachozungumza unazungumza habari hapa patapita barabara, hapa patapita maji, hapa patakuwa panapita nguzo za umeme na kadhalika na kadhalika.

Sasa kama anafikiri kwamba na mifugo tuweke humo humo hili ni wazo jipya ambalo nafikiri tutakuwa tayari kumsikiliza ili aweze kulishughulikia.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wanaitegemea sana Serikali yao katika kutoa maamuzi ambayo yanaweza kuwasaidia wananchi. Serikali ilishaamua kwamba Wilaya ya Rarya iwe na makao makuu yake lakini hadi sasa wananchi wa eneo la Rarya hawajajua makao makuu yao yatakuwa wapi.

Je, Serikali leo inatuambia nini kuwashakikishia wananchi wa Rarya wanatamkiwa rasmi mahali pakuwekwa makao makuu yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Sheria ambayo inaunda Halmashauri za Wilaya na Manispaa, sheria Na. 7 na 8 ya Mwaka 1982, inazipa pia Halmashauri hizo na maeneo hayo mamlaka na uwezo wa kuamua wao wenyewe kwamba wanafikiri kwamba Halmashauri, Makao Makuu ya Halmashauri yao yawe wapi hakuna mahali ambapo inatamka kwamba Waziri mwenye dhamana ndiye atakaye tamka kwamba makao makuu yatakuwa wapi ukiacha kwamba kama kutakuwepo na mgogoro. Sasa Halmashauri ya Wilaya ya Rarya kila wakati imetakiwa ikae na izungumze na iseme kwamba ingetaka makao makuu ya Halmashauri hiyo yawe wapi. Sasa wao ndiyo wanatakiwa kutuambia kwamba wanafikiri ni wapi wangependa wao Halmashauri ndiyo mamlaka zenyewe hizi, mamlaka tunaposema mamlaka za mitaa ndiyo maana yake hiyo yaani kwamba wao ndiyo wanaotakiwa waseme. Mimi nakumbuka wakati Mheshimiwa Lowassa alipokuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na akawa-*challenge* hivyo hivyo akawaambia kwamba kama mtafika mahali mkashindwa ku-*resolve* hili tatizo atamshauri Rais aondeoe jambo hili katika mpango huo. (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwanri naomba niongezee kidogo kuhusiana na suala hili. Alichokisema ni kweli katika mazingira ya kawaida Halmashauri husika ndiyo inakuwa na mapendekezo makubwa ya msingi ambayo kwa kawaida Serikali inayazingatia.

Katika hali ya Rarya ni tofauti kidogo kumekuwa na mvutano mkubwa kati ya wadau ndani ya Halmashauri kama makao makuu yaye Utigi, au yaye Shirati, na wote wana nguvu ambazo zilikuwa zinaleta ugumu sana. Kwa hiyo, ndiyo tulilazimika kulifanyia kazi kwa mara nyingine tena na tumeshampelekea Rais ushauri ambao tunafikiri ni mzuri zaidi ambao atautumia katika kuamua. Kwa hiyo, nilikuwa nataka nitoe wito tu kwamba wafanye subira kidogo nina hakika Rais haitachukua muda mrefu kabla hajatoa kauli yake ya mwisho na kwa kweli tunadhani itakuwa ni kauli ambayo itakuwa sasa lazima iheshimike kwa vyovoyote vile itakavyokuwa ameamua. (*Makofi*)

Na. 3

### **Tatizo la Mimba kwa Wanafunzi Nchini**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI (K.n.y. MHE. CYNTHIA H. NGOYE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Mbeya ni moja ya mikoa inayokumbwa sana na tatizo la mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jambo ambalo limeathiri sana utekelezaji wa Kanuni ya Elimu ya mwaka 1979 ya Uandikishwaji na mahudhurio ya wanafunzi mashulenii:-

(a)Je, Serikali iko tayari kuzisaidia kifedha asasi za Mkoa wa Mbeya zinazoendesha programu za utoaji wa elimu kwa umma na kusaidia ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari.

(b)Je, ni kwanini Serikali isirudishe utaratibu mzuri uliokuwepo huko nyuma wa kuteua na kuwaandaa walimu walezi kwa kila shule ili wawafidishe wanafunzi malezi na tabia njema.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kwa sasa haina uwezo wa kifedha wa kuzisaidia asasi zinazoendesha programu zinazotoa elimu kwa umma na kujenga mabweni katika shule. Aidha, inatambua umuhimu wa mabweni/hosteli kwa wanafunzi wa kike ili kuwanusuru watoto wa kike na vishawishi wanavyokutana navyo njiani wanapokwenda shule na wanaporudi nyumbani hususani pale wanapotembea mwendo mrefu kutoka majumbani mwao. Serikali inatoa wito kwa wananchi, asasi mbalimbali na halmashauri kutenga mapato yake na kuchangia ujenzi wa mabweni. Wizara itaendelea kuwa karibu na asasi zote zinazotoa elimu na malezi kwa vijana na inaunga mkono juhudii zote zinazofanyika kuwanusuru vijana.

(b) Utaratibu wa kuwepo walimu walezi kwa kila shule kwa ajili ya kutoa ushauri na unasihi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari upo kwa mujibu wa waraka wa elimu Na. 11 wa mwaka 2002. Waraka huo unaelekeza kwamba walimu walezi wa shule za msingi na sekondari wachaguliwe na wanafunzi wa shule husika. Ili kutekeleza Wizara inafanya yafuatayo:-

(i) Kuelekeza walimu wakuu na wakuu wa shule kuwapunguzia majukumu walimu walezi ili wapate nafasi ya kutekeleza shughuli za malezi na unasihi.

(ii) Kuhakikisha walimu walezi wanapata mafunzo kuhusu utoaji huduma ya malezi na unasihi.

(iii) Kufuatilia katika shule kuona kama Kamati ya malezi na unasihi imeundwa katika shule na huduma hiyo inatolewa kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, suala la malezi ya vijana ni jukumu la jamii nzima kwa ujumla na kimsingi linaanza katika ngazi ya familia. Nachukua fursa hii kuwasihii wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwa karibu na watoto ili kuwaelimisha athari za mimba za utotonii.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni mazuri; swali la msingi lilikuwa linasema kwamba Serikali sasa itakuwa na mpango gani. Nafahamu kwamba Serikali haina pesa lakini kwa mwaka uliopita kuna Asasi moja katika mkoa wa Mbeya imeonyesha mafanikio mazuri kwa kujumisha wadau wote wa Wilaya zote na Naibu Waziri ni shahidi na imeonyesha mafanikio.

Je, sasa Serikali ina mpango gani hasa kwa upande wa ujenzi wa mabweni kama ilivyowekwa mpango kwenye ujenzi wa mahabara kwamba kila mwaka angalau inatenga pesa kidogo kila mkoa kusaidia nguvu za wananchi ili tuondoe tatizo la mimba kwa watoto wa kike kwenye upande wa Sekondari.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi tumekiri kwamba jambo hilo ni muhimu la kujenga mabweni kwa ajili ya kuwanusuru wasichana.

Hata hivyo ufinyu wa Bajeti na kuwepo kwa vipaumbele vingi suala hili limetushinda kulitekeleza kwa uwiano unaostahili. (*Makofi*)

Hata hivyo tunaunga juhudhi, tunapongeza na pale tutakapojaliwa kwa kadri fedha zitakavyopatikana tutashikirikiana na wenzetu wa mkoa wa Mbeya kuhakikisha tunawasaidia kumaliza mabweni ambayo wameyaanza.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kutoa rai kwamba wazazi wananchi na wadau mbalimbali ambao tunapenda kuhakikisha kwamba wasichana wanapata fursa sawa basi tuunganishe juhudzi zetu na hilo litawezekana.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi, iliunda kamati iliyozunguka nchi nzima kuona na kupata madau ya wananchi kuhusu tatizo la mimba na ufumbuzi wake na Kamati hiyo ilimaliza kazi yake toka mwaka jana mwezi wa pili lakini mpaka leo serikali hajatoa ripoti nilikuwa naomba kujua ripori ile iko wapi na nini serikali inasema sasa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundsi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Awali ya yote napenda nikiri kwamba taarifa ile ipo tayari tumeipokea na iko mikononi mwa waziri ikiwa inasubiri mchakato wa maoni ya kijumla katika uboreshaji wa sera ambayo hatimaye itakapokubalika na wadau wote nchini ndipo itakapoingiza swala hilo. Hivyo kwa sasa Wizara pekee haiwezi kutoa lolote. Katika moja ya mapendekezo ya kamati ile iliyoundwa wakati huo, ilielekeza mambo kadhaa ambayo kwa mujibu wa sheria ya elimu inayotumika sasa, hayapo. Hivyo nawasihi wadau wote wawe na subira tumalize mchakato wa kuiboresha sera ya elimu kama ambavyo itapendekezwa na kukubaliwa na hatimaye tutengeneze sheria ya elimu ambayo itaboreshwa hapo ndipo tutakapoweza kusema mimba zichukuliwe namna gani lakini kwa sasa bado ni mapema.

Na. 4

#### **Mchango wa Serikali Katika Ada za Wanafunzi**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND (K.n.y. ALOYCE B. KIMARO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kwa utaratibu uliowekwa inapaswa kuchangia Shs. 20,000/= kama ada kwa kila mwanafunzi wa shule za sekondari hapa nchini:-

- (a) Je, Serikali inatekeleza jambo hilo kwa kila shule ya Sekondari ya Kata?
- (b) Kama ndiyo. Je, Serikali imetumia fedha kiasi gani kwa kila Mkoa kwa ajili ya ada ya wanafunzi hao?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu, huwa napata tabu hasa kuwatambua akina Mama wa Bungeni humu kwa sababu mnabadili sana mitindo ya nywele. Kwa hiyo inakuwa pengine. Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*).

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali bado haijafikia lengo la kuchangia shilingi elfu ishirini kama ada ya kila mwanafunzi wa shule ya Sekondari ya kutwa hapa nchini. Mpango wa Maendeleo ya elimu ya sekondari (*MESS*) wa mwaka 2008/2009 ulibainisha kuwa kila mwanafunzi anayesoma Sekondari ya serikali ya kutwa alitakiwa alipe ada ya shilingi elfu arobaini kwa mwaka. Serikali ilipunguza mzigo wa ulipaji ada kwa mzazi kutoka shilingi elfu arobaini hadi elfu ishirini serikali ilitarajia kupata fedha kutoka vyanzo vya ndani na nje ili kufidia pengo hilo la ada. Kwa kuwa fedha za wafadhili hazikupatikana kama ilivyotarajiwa serikali, imekuwa ikichangia punguzo hilo la ada kwa kila mwanafunzi wa kutwa katika shule za Sekondari za umma kulingana na fedha hiyo iliyopo. Aidha ongezeko kubwa la shule za sekondari za kutwa hapa nchini limechangia serikali kutofikia lengo la elfu ishirini kwa kila mwanafunzi wa Sekondari za kutwa hapa nchini.

(b) Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 jumla ya fedha iliyopelekwa katika shule za Umma ni shilingi bilioni nne milioni mia sita ishirini na nne kwa wanafunzi 417,712 huu ni wastani wa shilingi 11,700 kwa kila mwanafunzi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 serikali ilitumia shilingi bilioni kumi milioni mia moja tisini na tano mia nne ishirini na tatu mia tano na thelathini kwa ajili wanafunzi laki saba hamsini na sita alfu mia sita kumi na moja kwa mwanafunzi wa kutwa kwa shule za sekondari za umma. Huu ni wastani wa shilingi 13,475 kwa kila mwanafunzi. Fedha hizo hutumwa katika shule zote za serikali za kutwa kulingana na idadi ya wanafunzi waliopo. Ninalo jedwali refu sijui kama utaniruhusu nilisome.

**SPIKA:** Ah. Inatosha, inatosha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa serikali huwa inatoa hizo hela japo hazitoshelezi. Je iko tayari sasa kuagiza shule ambazo zitapokea mchango huo kutangaza rasmi kwa wazazi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zinapopelekwaWakuu wa Shule wanapaswa kuarifu. Kwanza kabisa ni kuiarifu Bodi ya Shule baada ya kikao hicho Bodi ya shule

hupaswa kuitisha kikao cha wazazi na hata matumizi ya fedha zile yanapaswa yawe yameidhinishwa na Bodi za shule. Kwa maana hiyo, tangazo lake si kuweka kwenye magazeti au wapi lakini anapaswa kuweka kwenye *notice board* kuonyesha ni kiasi gani cha fedha alichopata. Na si tu hi fedha ya punguzo la ada au fidia ya ada bali fedha yote inayopelekwa na serikali kwa mujibu wa kanuni na taratibu lazima ionyeshwe kwenye matangazo na matumizi yake pia. Kwa hiyo niseme niwasihii waheshimiwa Wabunge waone kwamba serikali inafanya hivyo na uwazi unapaswa uwepo pale ambapo watakuwa na mashaka naomba tupate taarifa ili tutoe ushirikiano wa karibu.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa shule hizi za serikal za kutwa mzazi anachangia shilingi elfu ishirini kwa mwaka na kwa kuwa shule hizi zimekuwa na michango mikubwa sana zaidi ya shilingi laki moja tofauti na shilingi elfu ishirini ile kwa mwaka na imesababisha wazazi wengi washindwe kupeleka watoto wao shule. Je, serikali inasema nini na inawaambiaje wananchi Watanzania juu ya swala hili ambalo limeleta mtafaruku mkubwa kwa wazazi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meryce Emmanuel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mchango wa wazazi kisheria uliopo wa kulipia ile ada ni shilingi elfu ishirini hata hivyo michango mingine yote itakayoamuliwa na kukubaliwa na Bodi inapaswa kupata kibali cha Kamishina wa Elimu. Kumekuwepo na hilo tatizo katika siku zilizopita na Wizara yangu imelifanyia kazi vya kutosha na kuona uhalisia wa mahitaji pale shulenii baada ya kudhibitika kwamba ziko huduma zinazopaswa kutolewa na nilazima kwa wanafunzi kwa hiyo mchango wote wa mzazi pamoja na mahitaji yote muhimu kwa mwaka huu ni shilingi elfu 60 tu kwa shule za kutwa kwasababu shule hizi nyingi zinaanza kabla ya mwaka wa fedha na hivyo inabidi kuchukua muda kidogo zijiendeshe kidogo hadi pale tutakapoweza kuziingiza kwenye mchakato na kupatiwa fedha. Kinyume chake pale ambapo itabidi iwe zaidi ya shilingi elfu 60 Bodi ya shule lazima ithibitishe, miniti za mkutano huo pamoja na mkutano wa kamati ya wazazi za kuthibitisha na kukiri au kukubaliana juu ya mchango wowote lazima ziifikie Wizara wapate baraka za wizara ndio mchango huo uendee. Tunaomba radhi kwa wale wote ambao wamepata usumbufu na kwamba ichukuliwe kwamba serikali inajali na inadhamini juhudii za wananchi wake.

**SPIKA:** Tumalizie nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa Ufafanuzi zaidi.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ndogo niongezee kwa jibu zuri alilolitoa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Spika, tatizo hili la kila shule kutoa barua za kuwaalika wanafunzi kujiunga na kidato cha kwanza zimeleta matatizo kama Mheshimiwa Mbunge alivyo sema na kupigiwa makofi na waheshimiwa wabunge

wengine. Kwa sababu hiyo Wizara yangu imechukua hatua ya kutoa *joining instructions* kwa shule zote Tanzania nzima ili wasiwatoze wazazi michango ambayo siyo ya kimsingi, ahsante. (*Makofî*).

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Nashukuru sana kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Serikali imeshindwa kutoa hiyo fedha ya shilingi 20,000 lakini wakati huo huo pia inashindwa kutoa fedha ya chakula kwa ajili ya zile shule ambazo ni za bweni na hata zile dola walizosema zitatolewa dola kumi kumi na yenyewe pia imeshindwa kutoa. Je, tatizo liko wapi hasa? Na baada ya kueleza tatizo hilo Serikali imejipanga vipi kutatua tatizo hilo ambalo kwa kweli ni kubwa na ni mzigo mkubwa kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi napenda kujibu swali la Mheshimiwa la Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, serikali haijashindwa kutoa kiasi cha shilingi elfu ishirini, kama idadi ya wanafunzi ingebakia ile ile. Mafanikio makubwa ya mpango wa *MEM* na mafanikio makubwa ya mpango *MMES* umewezesha idadi kubwa ya wanafunzi kufaulu na kupata fursa ya kuendelea na shule ya sekondari. Kwa maana hiyo tutakuwa hatuwatendei haki tukisema fedha ile ilipiwe kama ilivyokuwa imepangiwa hapo awali. Tumesema kidogo kilichopo kigawanywe kwa kadiri ya idadi ya wanafunzi iliyopo, kimkia hicho cha sungura kila mtu apate unyoya na kisikio.

Serikali hatujashindwa kulipa fedha ya chakula tunachokifanya hivi sasa ni kufanya uhakiki wa madeni yale baadhi ya madeni yamebainika, si sahihi na ushahidi tunao, Mheshimiwa mbunge kwa wakati wake namkaribisha ofisini tumuonyeshe maajabu. Kwa kufanya hivi tunachelea kupeleka fedha kama ambavyo madai yamewasilishwa, kuna mambo mengi ambayo tunapaswa tuyaangalie ili kuhakikisha fedha ya serikali inakwenda kama ipasavyo. Hivi sasa tumeanza na tulianza toka mwaka jana mwezi wa saba kila deni lililohakikiwa limelipwa yale yaliyokataliwa wadau waliarifiwa na wakuu wa shule waliarifiwa naomba twende taratibu kwasababu tunaelewa adhari za kulipa bila ya kuchukua uhakiki tutakuja kuingia kwenye matatizo ambayo siyo ya lazima.

Na. 5

### Kukarabati Kiwanja Cha Ndege Tunduru

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni takribani miaka 10 kiwanja cha ndege cha Tunduru hakitumiki kwasababu ya kutelekezwa na Serikali; na kwa kuwa, Wilaya ya Tunduru ipo mpakani mwa Tanzania na Msumbiji:-

(a)Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya kutelekezwa kwa kiwanja hicho?

(b)Je, Serikali itakubali kutenga fedha kila mwaka za ukarabati wa kiwanja hicho ili kitumike mwaka mzima na kuchochea utalii nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kujibu swali la Mheshimiwa Mturura, mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika Serikali haijakitelezea kiwanja cha ndege cha Tunduru kwani bado kinatumika na serikali inakihudumia. Kila mwaka serikali kupitia mamlaka ya viwanja vya ndege nchini hutenga fedha kwa ajili ya uendeshaji, ulinzi na uwekaji wa alama muhimu katika kiwanja cha ndege cha Tunduru. Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba katika mwaka 2006 zilitua na kuruka ndege 15, mwaka 2007 zilitua na kuruka ndege 25 na mwaka 2008 ndege 12 ziliruka na kutua katika kiwanja hicho. Aidha kwa kutilia maanani umuhimu wa kiwanja hicho cha ndege cha Tunduru, katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari mwaka 2008 kiwanja kilifungwa ilikutoa nafasi ya matengenezo ya kawaida kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege, yaani *running way* ambapo shilingi milioni 1.5 zilitumika kwa kazi hiyo.

Baada ya matengenezo hayo kiwanja hicho kiliendelea kutumika hadi tarehe 24/12/2008 na kilifungwa tena tarehe 25/12/2008 baada ya mvua kubwa kunyesha na kusababisha shimo kubwa katikati ya barabara ya kutua na kuruka ndege na hivyo kutishia usalama wa kiwanja. Hivisasa tathmini inafanyika ili kupata makadirio ya gharama za matengenezo ili fedha ziweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania hutenga fedha kila mwaka za uendeshaji wa kiwanja cha ndege cha Tunduru. Kwa mfano, katika mwaka 2007/2008 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilitenga shilingi milioni nne na mwaka 2008/2009 zilitengwa shilingi milioni sita. Fedha hizi zilitumika kwa ajili ya uendeshaji wa kawaida wa shughuli za kiwanja hicho kama vile, ulinzi, mishahara kwa wafanyakazi wa kiwanja, uwekaji wa alama muhimu za kiwanja, yaani *markings and window socks*, ambazo zinamsaidia rubani wakati wa kuruka na kutua ili aweze kutua na kuruka salama. Na katika mwaka 2009/2010 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya mahitaji ya uendeshaji wa kiwanja cha ndege cha Tunduru ili kiweze kuendelea kutumika wakati wote.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo naamini kwa kiwango kikubwa yataleta fadhaa kubwa sana kwa wananchi wa Tunduru, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amelithibitishia Bunge kwamba kiwanja hiki bado kinahudumiwa na Serikali, na Kwa kuwa, ametuthibitishia hapa kwamba mwaka 2006 ndege zipatazo 15 zilitua na kuruka katika uwanja ule naomba Serikali itueleze ni kwanini ndege ambayo ilichukua mwili wa Marehemu Mbunge wetu, Juma

Jamaldin Ukukweti, pamoja na waombolezaji hazikutua Tunduru ili hali uwanja ule unatumika katika kutua ndege?

Kwa kuwa, moja ya sera kuu za Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ni kuondoa kero za wananchi. Na kwa kuwa, uwanja huu wa Tunduru kwa hivi sasa upo katikati ya mji wa Tunduru na unmekuwa ukitoa kero kubwa sana kwa wananchi ambao wanakatisha uwanja ule wanakamatwa na kutozwa fedha faini shilingi 5,000 ambazo hawapewi risiti, Je, Serikali ipo tayari sasahivi kutekeleza wazo lake la kuuhamisha uwanja ule wa Tunduru kwenda kijiji cha sisi kwa sisi ambapo eneo kubwa sana limetengwa ili kuondoa kero kwa wananchi wa Tunduru?

**SPIKA:** Tena hata jina lake ni zuri, *Sisi kwa Sisi Airport*. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. (*Kicheko*).

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tundur, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kiwanja hiki cha Tunduru bado kinahudumiwa na Serikali na kinatumika kama nilivyoeleza katika majibu ya msingi. Sasa sababu ambazo zilifanya ile ndege iliyochukua mwili wa Marehemu Mpewda Wetu, Mheshimiwa Akukweti, isitue Tunduru, kama mutakavyokumbuka kuwa kipindi kile kilikuwa ni kipindi cha mvua kubwa. Kwa hiyo, kwa kuweka tahadhari ya kutosha kwa kuzingatia kwamba tukio lenyewe lilikuwa ni zito; tusingweza ku-*risk* kusema kwamba basi tujaribu kwenda kutua Tunduru na mazingira kama hayo. Kwahiyo kilichofanya ndege ile isiende kule ilikuwa tu ni kwa sababu ya mvua kubwa wakati huo na kuhakikisha kwamba tunaufikisha mwili wa ndugu yetu salama tukalazimika mwili ule utue Mtwara na baadaye kwenda kwa barabara hadi Tunduru.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, uwanja wa Tunduru huo unaozungumza sasa hivi uko katikati ya mji kama alivyosema na mimi nitoe tu mwito kwamba hata hao wananchi ambao wanakatisha uwanja huo, kwanza ni makosa kwa wananchi kukatisha katikati ya uwanja na ningetua tu wito kwamba tushirikiane na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wote wa Tunduru kwamba kukatisha uwanja katikati wakati bado unatumika ni makosa na kwa kweli ni hatari kwao. Ili kwa usalama wao tushirikiane tu kwamba suala la kukatisha uwanja kwa usalama wao wasiendelee kukatisha. Sasa suala la kuuhamisha uwanja huo kutoka hapo Tunduru kwenda mahali panapoitwa Sisi kwa Sisi, wazo hilo tunalipokea na tunaendelea kulifanya kazi. Na kusema kweli tuseme tu kwamba hata na viwanja vingine vyote ambavyo viro katikati ya mji Serikali inaendelea kuvitazama ili kuhakikisha kwamba viwanja hivi vinapelekwa mahali pengine ambapo panakuwa ni pa usalama zaidi. (*Makofi*).

**SPIKA:** Sasa tumechokoza viwanja Musoma, Singida, Ukerewe, haya haraka haraka basi mpate kusema. Tuanze na Mheshimiwa Balozi Dr. Mongela, Mheshimiwa Manyinyi halafu na Singida, Diana Chilolo.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, mwuliza swali anatoka sehemu moja ambayo ni pembezoni mwa Tanzania kama ilivyo Ukerewe. Je, Waziri atakubali ya kwamba katika Bajeti ya mwaka huu kiwanja cha Tunduru kiwekwe kwenye Bajeti pamoja na Nkirizi cha Ukerewe?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe na Rais wa Bunge la Afrika kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nikubaliane tu na Mheshimiwa Mbunge Mongella kwamba umuhimu wa kiwanja cha Tunduru unafanana fanana na kiwanja kilichopo huko Ukerewe. Na sisi kwa upande wa Serikali kwa kweli, tungependa viwanja vyote hivi ambavyo vinahudumia wananchi sio vile vya pembezoni tu, viweze vikawa vinatumika wakati wote na ndio maana katika mipango ya Serikali tuliyonayo tutakuwa tunaangalia mwaka hadi mwaka kwa kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya viwanja hivyo na kuzingatia vile vilivyoko pembezoni ikiwepo pamoja na cha Ukerewe.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kiwanja cha Tunduru, katika Mji wa Musoma tuna tatizo kubwa sana na uwanja wa ndege wa Musoma amba ni hatari kwa maisha ya wananchi wa Musoma. (*Makofi*)

Labda nitoe mfano, ile ndege ya Rais inapotua pale ambayo inapaswa kubeba takribani watu 30 inalazimika kwenda niende nao chini ya 20 wanalazimika kupungua kwa sababu ya ubovu wa kile kiwanja. Halafu vilevile hata mvua ikinyesha ndege ile inalazimika kuruka tu, na hivyo ni sambamba na ndege zingine. Sasa ningependa kufahamu, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inatenga pesa za kutosha kwa ajili ya uimarishaji wa kiwanja hicho ambacho ni pamoja na mpango mzima wa kuhamisha kiwanja hicho ili kiende mahali panapostahili kuliko hapo kilipo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimetoa maelezo hapa wakati nikijibu swali jingine la nyongeza ya kwamba hivi viwanja ambavyo viko katika maeneo ya miji, katikati ya watu ikiwemo na hicho cha Musoma ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja. Kwa kweli sisi tungependa viwanja hivi vikakaa mahali ambapo pana usalama zaidi.

Kwa hiyo, mipango ambayo Serikali inayo ni hiyo ya jumla ambayo nimeisema tu kwamba tutaendelea kuwasiliana na mamlaka zinazohusika kuititia mamlaka yetu ya

Viwanja vya Ndege kuona uwezekano wa kuvihamisha viwanja hivi kutoka mahali hapo vilipo ili viende mahali ambapo ni salama zaidi badala ya kuingiliana na makazi ya watu.

Lakini kuhusu uwezo wa uwanja wa ndege sasa hivi pale Musoma, tunakubaliana naye kwamba kwa uwezo uliopo sasa hivi hauwezi ukakidhi ndege kubwa. Kwa hiyo, utaratibu wa kukiangalia kiwanja hicho cha Musoma kuweza kukipanua zaidi na kiweze kubeba ndege kubwa zaidi unaandaliwa na Serikali na tutaendelea kumfahamisha Mbunge kwa kadri tutakavyokuwa tunakamilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa, matatizo ya viwanja vya ndege ni mengi hapa nchini pamoja na kiwanga cha ndege cha mkoa wa Singida. Kwa kuwa, wananchi wa mkoa wa Singida chini ya kiongozi wao Mkuu wa Mkoa, wakishirikiana na Serikali wamefanya kazi kubwa sana ya kukarabati kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Singida pamoja na kuongeza ukubwa wa kiwanja hicho. Kwa kuwa, hata ndege za biashara zimeonesha nia ya kutua Mkoa wa Singida, na wanashindwa tu kwa kuwa kiwanja hicho hakina lami.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mwenyewe kaka zangu wote kwa pamoja, hawaweze wakaonesha huruma leo hii ndani ya Bunge hili, kutamka tu kuweka lami ili uchumi wa Mkoa wa Singida uendelee na ndege za biashara ziweze kutua?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na wewe ni mdau wa Mkoa wa Singida. (*Makofi*).

**NAIBU WZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ningependa kujibu swali la nyongeza Diana Chilolo, Dada yangu kama alivyosema. Nafahamu sana tatizo la Mkoa wa Singida juzi juzi nilikuwa kule, lakini nataka tu niseme kwamba tulikuwa na mipango hiyo anayosema Mheshimiwa Mbunge, na katika taratibu za kufuutilia tatizo hili tulikuwa tunafuutilia suala la kuweka *aprone* ya *taxing way* katika kiwanja hicho cha ndege cha Singida kwa kujenga tabaka lenye unene wa milimita 200 na sasa hivi tunachosubiri ni kupatikana kwa mkandarasi ambaye tunafikira kwamba atapatikana mwezi wa Aprili mwaka huu.

Na. 6

### **Ndege Kuongozwa na Rubani Mmoja**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, ndege nyingi za mashirika ya hapa nchini zinazoruka ndani ya nchi huongozwa na rubani mmoja; na kwa kuwa, rubani ni mwanadamu kama walivyo wanadamu wengine:-

(a) Je, itatokea nini kama rubani atashindwa kuendelea kuongoza ndege kwa sababu za kibinadamu?

(b) Je, huko siyo kuhatarisha maisha ya abiria kwa ruhusu rubani mmoja tu kurusha ndege?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida idadi ya marubani wanaohitajika kuongoza ndege kwa wakati mmoja inazingatia Kanuni za usafiri wa anga za Tanzania za mwaka 2006, yaani *The Civil Aviation of Aircraft Regualtions 2006*. Kulinga na Kanuni hizo za usafiri wa anga za Tanzania ndege yenye uzito usiozidi kilogram 5,700 kama uzito wa juu wa kuruka, yaani *maximum allowed take-off mass* na viti visivyozidi 19, huruhusiwa kuongozwa na rubani mmoja. Na ndege zenye uzito wa zaidi ya kilogram 5,700 na viti zaidi ya 19 huhitajika kuwa na marubani wasiopungua wawili.

Kwa kuwa ndege nyingi zitumiwazo na makampuni mengi hapa nchini ni ndogo na zenye uzito usiozidi kilogram 5,700 na viti visivyozidi 19, kanuni za usalama wa anga za Tanzania zinaruhusu ndege hizi kurushwa na rubani mmoja.

Aidha kwa mujibu wa Kanuni Namba 148 (2) ya *Civil Aviation Personal Licensing Regualtions* inayohusu *Physical and Mental Requirements* inayoelekeza kwamba rubani hataruhusiwa kabisa kurushha ndege kama atakuwa na ugonjwa wowote ambao unaweza ukamfanya ashindwe kuiongoza ndege akiwa angani. Madaktari wa marubani hutumia Kanuni hii katika kujua hali ya afya ya rubani kabla ya kumruhusu rubani ye yole yule kurusha ndege.

Mheshimiwa Spika, ni nadra sana kutokea kwa rubani mmoja anayeongoza ndege kushindwa kwasababu za kibinadamu au afya. Kwasababu marubani wote huruhusiwa tu kurusha ndege iwapo wao wenyewe watajihisi wana afya njema na pia madaktari maalumu wa usafiri wa anga, yaani *Aviation Doctors*, watahakikisha na kutoa cheti maalum yaani *Medical Certificate* kuwa rubani huyo ana afya njema na kumruhusu kurusha ndege.

Kwa vile hayo yote yanazingatiwa ndio maana katika takwimu za ajali za ndege zilizotokea hapa nchini katika miaka 25 iliyopita hakuna hata ajali moja iliyosababishwa na rubani kushindwa kuiongoza kwa sababu za kibinadamu.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, mimi nina masuala mawili madogo. La kwanza nilitaka kujua ni kigezo gani cha kanuni za usafiri wa anga Tanzania kinachoruhusu ndege ambazo hazina zaidi ya viti 19 kuruhusiwa kuongozwa na rubani mmoja? Hilo la kwanza,

La pili, suala langu ni kuwa hasa labda sababu hizi za kibinadamu zinaweza kutokea wakati ndege tayari iko angani kwa hiyo ikiwa ajali hizi hazikuweza kutoa miaka 25 iliyopita kwa mujibu wa takwimu kama alivyosema Mheshimiwa Waziri hiyo inathibitisha vipi kwamba mbeleni haitaweza kutokea ajali kama hiyo ?

**SPIKA:** Aah! ndiyo umemaliza hivyo? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa wa Miundombinu napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kigezo kinachotumika kuweka huo uzito pamoja na idadi ya watu kwa kweli ni kigezo cha kitaalamu ambacho kimethibitishwa na Watalamu wa *Civil Aviation* kwa kimataifa.

Kwa hiyo, wakafikia hatua hiyo kwamba katika uzito huo na wingi wa watu hao rubani mmoja anaweza akaiendesha hiyo ndege bila wasiwasi wowote na kwa kawaida kwa kweli lazima zitakuwa ni safari fupi fupi ambazo hazitumii muda mrefu sana vinginevyo kama itakuwa ni zaidi ya hapo hawataruhusiwa. Lakini kwamba ajali pamoja na kwamba haijatokea sasa hivi huko mbele tunajuaje?

Mheshimiwa Spika, ajali ni ajali sasa inaweza ikatokea kwa tukio la rubani akiwa peke yake angani au ikatokea kwa tatizo lingine lolote lile. Lakini ikitokea hapo kusema kweli hapo ni kumwomba Mwenyezi Mungu awabebe wananchi maana unafanyaje?

Labda itokee kwamba katika ndege hiyo awepo abiria vilevile ambaye ni mtaalamu wa kuendesha ambaye naye vilevile kiutaratibu hawezi akaingilia pale kati.

Kwa kweli ajali ni ajali ikitokea tunamwachaia Mwenyezi Mungu.

**SPIKA:** Ooh! nimebaini tumekwenda taratibu mno sasa tutakwenda haraka kidogo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na swali ni la Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi. (*Makofî*)

Na. 7

### **Mkakati wa Kupunguza Vifo vyakina Mama na Watoto**

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH** aliuliza:-

Kwa kuwa, moja ya kipimo cha maendeleo na mikakati ya Serikali ya Awamu ya Nne kupitia ilani ya uchaguzi ni kuhakikisha kuwa vifo vyakina mama na watoto vinapungua kwa ujenzi wa zahanati na vituo vyakina afya, kuajiri watumishi wenye sifa katika sekta hii na kubofesha maslahi na mazingira ya kufanyia kazi:

(a) Je, utekelezaji wa mikakati hiyo ikoje?

(b) Je, Serikali imasemaje kuhusu watumishi wa Sekta hii ambao ni wachache na wanafanya kazi usiku na mchana kwa mshahara huo huo bila marupurupu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi kwanzna naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba moja ya maazimio ya ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005-2010 ni kupunguza vifo nya akina mama na watoto kwa kuongeza idadi ya vituo nya kutolea huduma na kuajiri watumishi wa afya wenye sifa. Katika utekelezaji wa mpango huu, Serikali kuititia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Madhumuni ya mpango huu ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa umma kwa kuwa na zahanati katika vijiji, Kata na kuimarisha vilevile hospitali za Wilaya na Mikoa ili ziweze kutoa huduma za afya kwa kiwango cha juu zaidi. Mpango huu unaenda sambamba na jitihada za kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa katika vituo vilivyopo na vitakavyoongezekana.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2008/2009, jumla ya shilingi 33.29 bilioni zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa Zahanati kwa kila kijiji na kituo cha afya kila Kata.

Bilioni 23 kati ya hizo ni fedha za Serikali, bilioni 2.4 ni mchango wa Serikali ya Denmark kuititia shirika la *DANIDA*, bilioni 7.2 mchango wa Serikali ya Ujerumanu kuopitia Shirika la *KFW* na milioni 890 ni mchango wa Serikali ya Urusi. Halmashauri zote zimeagizwa kuandaa na kuwasilisha TAMISEMI bajeti kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vituo vipyta katika maeneo yao. Mpaka sasa takribani nusu ya Halmashauri zote zimekwisha wasilisha Bajeti zao. Baada ya Halmashauri zote kuwasilisha TAMISEMI watawasilisha maombi ya fedha hizo kutoka HAZINA na kuzituma kwenye Halmashauri husika kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuititia Bunge lako Tukufu kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuwasiliana na na Halmashauri zao ili kuhakikisha kuwa bajeti hizo zimewasilishwa TAMISEMI mapema iwezekanavyo ili kuwahi utekelezaji wa mpango huu muhimu.

Aidha, kuhusu suala la ajira, Serikali imeendelea kuajiri watumishi wenye sifa kwa ajili ya kwenda kufanya kazi sehemu mbalimbali nchini. Katika kipindi cha Desemba,2005 hadi Desemba, 2008 jumla ya watumishi 11,086 wa kada mbalimbali za afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Mafundisanifu, Wazoeza Viungo, Maafisa Wauguzi, Wafamasia, Wahudumu wa Afya, Tabitu na Makatibu wa Afya wamepangiwa kufanya kazi katika Sekretarieti za Mikoa yote, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji, na Wilaya zote na katika baadhi ya Wizara. Vilevile, kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya

Kiserikali ya Benjamin William Mkapa *HIV/AIDS Foundation*, jumla ya wataalamu wa afya 275 wameajiriwa na wapo katika halmashauai 52 nchini.

(b)Mheshimiwa Spika nakubaliana na Mheshimiwa kwamba watumishi wa afya ni wachache sana na kwa sababu hiyo wamalazimika kufanya kazi kwa muda mrefu. Katika jitihada za kuwapa motisha watumishi hawa, Serikali ya awamu ya nne katika kipindi cha 2006-2008 imekuwa ikiboresha mishahara yao mara kwa mara kadri uwezo wa Serikali unavyoruhusu.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wake imetayarisha utaratibu wa kutoa motisha kwa wafanyakazi wataofikia malengo ya utekelezaji wa mpango wa kupunguza vifo vya akina mama na watoto katika Halmashauri kwa kulingana na vigezo vilivyowekwa. Utaratibu huu ambao unaitwa *pay for performance* utaanza katika kipindi cha fedha 2008/2009.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa napenda tu Mheshimiwa Naibu Waziri anipe ufanuzi hasa kuhusiana na swali la kipengele A.

Nimesema fedha zilizotengwa mwaka 2008/2009 na sasa tupo katika robo tatu ya mwaka wa bajeti bado ni Halmashauri nusu tu ambazo ndiyo zimewasilisha ule mpango kwa ajili ya mpango mzima wa kuboresha afya na ujenzi wa vituo vya afya huko kwenye kata na vijijini.

Sasa je, Wizara haioni kwamba upo umuhimu sasa kwa Halmashauri zile nusu ambazo tayari zimeshawasilisha ule mpango zikapewa hizi pesa ili zile nyingine ambazo bado zikaja zikamaliziwa ile pesa ambayo itakuwa imebakia ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati Waziri akijibu amezungumzia juu ya watumishi kuongezwa mishahara na mimi nilikuwa nimezungumzia juu ya marupurupu, lakini akaeleza katika kigezo ambacho kinatumika sasa hivi kile cha kupunguza wale ambao watakidhi vigezo vya kupunguza vifo vya watoto na akina mama. Je, hivi vigezo ni vya aina gani na utajuaje kwamba huyu amekidhi vigezo na akapewa hiyo motisha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma H. Killimbah kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba Wizara imeagiza Halmashauri iweze kupeleka mahitaji yao TAMISEMI na itakapofika TAMISEMI wao ndiyo wana jukumu la kwenda kuiombea fedha kutoka Hazina. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba suala la kwamba TAMISEMI wachukue wale nusu ambao wamekidhi wapeleke kule fedha mimi nadhani sasa hilo ni swali ambalo Wizara ya TAMISEMI yenewe italionia, kama wale 52 kama Iramba

wanawenza wakaombewa fedha basi sasa huo ni aumuzi wa TAMISEMI kwa sababu vigezo watakavyopeleka pale TAMISEMI wakiona wamekidhi basi TAMISEMI wenyewe ndiyo wanaendelea na ule mchakato wa utekelezaji.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ananisikia na tutashirikiana naye hapa na Wizara ya Afya ili tuweze kuona kwamba wale ambao wamefikisha basi tunafanyaje. Je, tuwape au tuendelee kuwasubiri na ni kweli kwamba Bajeti imefikia robo tatu.

Mheshimiwa Spika, swal la pili ni kweli kabisa kwamba nilizungumzia suala la mishahara lakini tumezungumzia hapa suala la kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto ndiyo maana nikasema kwamba katika Wizara imeandaa utaratibu ili Halmashauri ziweze kulipwa kwa vigezo. Vigezo hivi vimeandaliiwa na vimepelekwa katika Halmashauri husika ndiyo nikasema kwamba kuna mpango wa *pay for performance*.

Sasa wale ambao watakidhi kwa sababu wameainishiwa vile vigezo na katika Halmashauri hivyo wamepewa sasa labda kama anataka baadaye nimwambie vigezo vyenyewe ni vipi ili Waheshimiwa Wabunge tuwaambie ili iweze kusaidia viweze kupatikana katika sehemu za kutolea huduma basi Wizara baadaye tutafanya utaratibu ili tuweze kuwapatia.

Lakini ni kwamba huu ni mpango hasa unaotilia maanani jinsi ya kupunguza vifo vya akina mama kwa hiyo *performance* hii ina vigezo mbalimbali tutawapatia ili kuweza kuviona.

Na. 8

### **Makundi Yanayotakiwa Kupewa Huduma za Afya Bure**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:

Kwa kuwa, Sera ya Afya ya Serikali inaelekeza makundi ya jamii yanayotakiwa kupewa huduma za afya bure:

- (a) Je, ni makundi gani hayo?
- (b) Je, Serikali inafahamu kwamba katika kijii cha Basanza (Kigoma Kusini) watoto chini ya miaka mitano hutozwa fedha mara waendapo kupima kliniki ?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swal la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Sera ya Afya ya Taifa la Mwaka 1990 na kama ilivyodurusiwa mwaka 2007, inaelekeza makundi ya jamii yanayotakiwa

kupatiwa huduma za afya bure. Kwa mujibu wa sera hiyo makundi ya jamii yanayostahili kupatiwa huduma za afya bure ni kama ifuatavyo:-

- Watoto wa umri chini ya miaka mitano;
- Wanawake wajawazito;
- Watu wenye magonjwa sugu kama vile Saratani, Kifua Kikuu, Ukoma na UKIMWI;
- Wazee wenye umri wa miaka 60 na kuendelea ambaeo wamethitishwa kuwa hawana uwezo; na
- Watu wote wa umri wowote ule ambaeo wana uthibitisho kuwa hawana uwezo.

(b)Mheshimiwa Spika, tofauti na taarifa kupitia swal la Mheshimiwa Mbunge, Serikali hajjawahi kupokea taarifa yoyote kuhusu watoto wa Kijiji cha Basanza Kigoma Kusini kuwatozwa fedha watoto wa umri chini ya miaka mitano wanapokwenda kliniki. Hata hivyo, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya kipengele (a) hapo juu watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanatakiwa kupatiwa huduma za afya bila malipo yoyote katika vituo vyote vya Serikali na ambavyo vina ubia na Serikali kama vile hospitali teule.

Kwa msingi wa ufanuzi huu, ni kinyume na ni kosa kwa vituo vya Serikali na vile vyenye ubia na Serikali kuwatoza fedha watu wote wanaoangukia katika makundi niliyoyataja hapo juu wanapokwenda kwenye vituo hivyo kupata huduma zote za afya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa hii hata hivyo kupitia swal la Mheshimiwa Mbunge, Wizara imemwagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kulifanya uchunguzi suala hili na kuwasilisha taarifa Wizarani kwa hatua zaidi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa utoaji wa huduma bure kwa vigezo ambavyo vimeelezwa katika sera ya afya imeonekana kiuhalisia havitekelezeki. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kupitia Wizara yake wana mikakati gani mipya ya kuvielekeza hivi vituo vya afya ama vituo vyenye ubia na Serikali kuhakikisha basi sera hii inatekelezeka kiukamilifu na siyo kwa kauli za Bungeni pekee?

Swali langu la pili linahusiana na suala hilihili kwamba tunafahamu wastaa fu wetu wa Jeshi wanaishi katika mazingira magumu sana hasa ukizingatia kwamba pension zao za mwezi ni finyu sana.

Je, Serikali ina mikakati gani ya ziada kuhakikisha kwamba wastaafu wa Jeshi nao pia wanapewa au wanaingia katika mpango huu wa huduma za afya bure hasa ukizingatia kwamba wengi wao wanastaafu kabla ya miaka 60?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima J. Mdee kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la kwanza kwamba kihisia haitekelezeki.

Kama nilivyozungumza katika jibu langu la msingi, Serikali kupitia Wizara ya Afya imetoa maagizo katika vituo vyote vya kutolea huduma vile ambavyo nimevianisha ili kuhakikisha kwamba makundi haya yaweze kupatiwa huduma bure.

Nafahamu tatizo hapa ni kwamba ni ule utekelezaji kule katika maeneo, kwa hiyo, suala hapa siyo kwamba ni Serikali haijatoa maagizo, suala ni kusimamia katika maeneo katika zile hospitali zetu ili waweze kuhakikisha kwamba inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu, kuna maeneo mengine ambayo unakuta kwamba hayana hospitali teule mathalani au hayana vituo vya kutolea huduma vya Serikali lakini Serikali pia imekuwa ikizungumza na Halmashauri na kuagiza kwamba waweke mikataba ya kutolea huduma na vile vituo kwa mfano mashirika ya dini au binafsi ili yale makundi ambayo yanapata huduma zile katika yale maeneo ambayo si teule waweze kutoa hizi huduma na kulipa kupitia zile fedha ambazo zinapatikana katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachoomba hapani kwamba naomba tuendelee tukishirikiana na TAMISEMI wale ambao katika Halmashauri sehemu ambazo zinatoa huduma za Serikali na zile teule waendelee kutoa huduma hizi bila malipo na yejote ambaye hatafanya hivyo anakiuka.

Lakini wale ambao hawana hospitali za Serikali na wala hawana teule waandike mikataba ya huduma ambayo inaitwa *service agreement* ili waweze kuwalipa wale wanatoa hizi huduma za binafsi ili watoto wanaotibiwa pale waweze kutibiwa bure na wale wa makundi maalum. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu wastaafu wa Jeshi. Bahati mbaya mstaafu kama ni wa Jeshi au kama ni mstaafu mwagine kama ataangukia katika kundi la wazee kama yeje hana uwezo basi ataingia katika kundi maalum na kama ni mzee wa miaka 60 na ambaye hana uwezo.

Kwa hiyo, siwezi nikasema hapa wafanyiwe utaratibu tu wastaafu wa Jeshi tu ndiyo wenyewe waingizwe katika huo msamaha. Hapa tunachozungumzia wazee wote

wa miaka 60 ambao hawana uwezo wawe Walimu, Wanajeshi au wengine ambao hawana kazi itakapofika ana miaka 60 anatakiwa aangaliwe kama hana uwezo apate huduma bure.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Muda umetutupa mkono tunahamia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na swali linaulizwa na Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mbunge wa Makete.

Na. 9

### **Uuzaji wa Viazi Mviringo Vilivyosindikwa**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, maduka mengi nchini maarufu kama *Supermarkets* yanauza bidhaa ya viazi mviringo vilivyosindikwa maarufu kwa jina la *Potato Crips* ambazo kwa sasa inaagizwa kutoka nchi za nje; na kwa kuwa, Tanzania inao wakulima wakubwa wa viazi mviringo katika Mikoa ya Iringa, Arusha na Kilimanjaro:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kusindika bidhaa za viazi mviringo ili kuongeza thamani ya viazi na kutoa ajira kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge Mbunge wa Makete kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, kuwa upo umuhimu wa kuanzisha viwanda vya usindikaji katika maeneo aliyotaja.

Hata hivyo, uanzishwaji wa kiwanda chochote katika Wilaya yoyote unatokana na utashi wa wananchi na wawekezaji mbalimbali kuibua miradi ya usindikaji kwa mazao hayo. Serikali kwa upande wake inaendelea na jukumu lake la msingi la kusimamia na kuweka mazingira wezeshi ya kuanzishwa viwanda vidogo vya kusindika ikiwa ni pamoa na kufanya mambo yafuatayo:-

(a)Kuandaa utaratibu wa kuhamasisha utambuzi na ushiriki wa wananchi kutoa mtazamo kwa mazao maalum vikiwemo viazi mviringo, katika kila Wilaya ili utaratibu wa kuhakikisha hatu mbalimbali za maendeleo ya mzao husika inahudumiwa ipasavyo – *District Agricultural Development Programs (DADPs)*.

Hatua hizo ni pamoja na upatikanaji wa pembejeo, ulimaji, uvunaji, usindikaji, usafirishaji na utafutaji wa masoko ya bidhaa husika ili mkulima aweze kupata thamani halisi ya nguvu zake.

(b) Kutoa mafunzo katika nyanja za usindikaji wa mazao mbalimbali, vikiwemo viazi mviringo kwa kulingana na mahitaji ya mahali husika. Katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2008 jumla ya wajasiriamali 1,989 walipatiwa mafunzo, na wajasiriamali 730 kati ya hao, walianzisha miradi ya usindikaji wa vyakula na kuifanya kama kazi yao ya kudumu.

(c) Kuhamasisha sekta binafsi kujitokeza kuwekeza kwenye usindikaji wa mazao vikiwemo viazi mviringo kutoka Mikoa ya Iringa, Arusha na Kilimanjaro na kwingineko kunakopatikana zao hili.

(d) Kuendelea kujenga uwezo wa Shirika la Viwango Tanzania ili kusimamia ubora wa bidhaa tunazozalisha zikiwemo za viazi mviringo.

(e) Kuanzisha utaratibu wa kuendeleza mazao mbalimbali kwa kila Wilaya ujulikanao kama *One District, One Product*. Hadi sasa jumla ya mazao/bidhaa 40 za aina mbalimbali zimeainishwa katika Wilaya zote za Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote tusaidiane kuwahamasisha wananchi woe kuanzisha miradi ya viwanda vidogo vya kusindika ili kuwapatia soko wakulima mazao haya na kutoa ajira kwa wananchi.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupewa nafasi hii na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Nini mkakati wa Wizara wa kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vya mazao ya kilimo *Agro Industrialisation Program* inayozingatia fursa ya umeme wa grid unaosambazwa na unaopatikana mikoani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimesema hapa kwamba tuna utaratibu wa kuainisha zao moja kwa kila Wilaya na hadi sasa tumekuwa na mazao 40 kwa Wilaya 40, utaratibu wa kuanisha siyo tu lile zao lenyewe lakini vilevile ni namna gani ya kuzalisha na mojawapo ya mambo ambayo tunazingatia ni upatikanaji wa Nishati hasa ya umeme.

Napenda nimhakikishie tu kwamba hayo tunayazingatia kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuhakikisha kwamba viwanda hivi vinaanzishwa kwa namna ambayo vitaweza vilevile kupata Nishati kwa urahisi.

## **SIDO Kusaidia Wajasiriamali Wanawake Pemba**

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la *SIDO* linasaidia sana kuwaendeleza wajasiriamali hapa Tanzania hasa wanawake:-

Je, Serikali haioni haja sasa ya kuliagiza shirika hilo kuanzisha harakati za maendeleo kwa Wanawake kisiwani Pemba?

## **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*) linasaidia sana kuwaendelea wajasiriamali hapa nchini wakiwemo Wanawake. Aidha, Shirika hilo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 28 ya mwaka 1973 kwa lengo la kuendeleza viwanda vidogo vidogo. Shirika hili lina Ofisi katika Mikoa yote Tanzania Bara na kwa sasa halina mipango ya kuanzisha harakati za shughuli zake Pemba au Unguja kwani Sheria iliyokianzisha chombo hiki iliweka bayana kuwa eneo lake la kufanya kazi ni Tanzania Bara.

Hata hivyo, *SIDO* imekuwa ikitoa huduma zake visiwani ikiwemo mafunzo ya usindikaji wa matunda, nafaka, mboga na viungo (*spices*). Kwa mfano, wajasiriamali zaidi ya 60 kutoka visiwani (wengi wao wakiwa Wanawake) wamefaidika na mafunzo hayo. Aidha, shirika liko tayari kuendelea kutoa ushirikiano kwa makubaliano na wadau au vyombo vinavyotoa huduma za kuendeleza sekta hasa katika harakati za kutekeleza Sera maalum ya kuendeleza sekta ya viwanda na biashara ndogo huko visiwani. (*Makofii*)

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swalii moja tu dogo la nyongeza.

Je, Wizara iko tayari kama tukigharimia wanawake kuwaleta na *SIDO* ikawagharimia kuwatolea mafunzo ?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Maghimbi, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Maghimbi kwa kuona umuhimu wa kuwasaidia akina mama wengi zaidi kuweza kupata mafunzo ambayo yanatolewa na taasisi yetu ya *SIDO*.

Pili, napenda kumhakikishia kwamba *SIDO* tutaendelea kutoa yale mafunzo kama tulivyokuwa tunafanya pale tunapoombwa. Lakini kama anaona kwamba akiwaleta wanawake kwa wingi itawasaidia kujifunza zaidi, napenda nimhakikishie kwamba *SIDO* na Wizara tuko tayari kurahisisha zoezi hilo. (*Makofī*)

Na. 11

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara zimo katika mchakato wa kutafuta mafuta nchini kwa manufaa ya baadaye na kwamba hivi karibuni *TPDC* ilisema kuwa Zanzibar hakuna mafuta:-

- (a) Je, ni sheria gani mojawapo inayoipa *TPDC* mamlaka ya kutoa kibali cha kutafuta mafuta Tanzania Zanzibar wakati wao siyo chombo cha Muungano?
- (b) Je, mamlaka gani iliyowapa *TPDC* nguvu ya kutangaza kuwa Tanzania Zanzibar hakuna mafuta wakati Wazanzibari wanasema mafuta yapo?
- (c) Je, kama *TPDC* si chombo cha Muungano Serikali haioni kuwa, kuitangazia Tanzania Zanzibar mambo yasiyo ya Muungano ni kuingilia mamb o yasiyoihusu?

**SPIKA:** Pamoja na tahadhari hiyo, majibu Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swal la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *TPDC* iliundwa kwa tamko la Rais chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 *Public Cooperations Act* na kupewa majukumu ya kutafuta, kuzalisha na kuendeleza mafuta ya *petrol* chini ya Sheria ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta ya mwaka 1980 iliyopitishwa na Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheria hii ya utafutaji mafuta inampa Waziri wa Serikali ya Muungano mwenye dhamana ya *petrol* madaraka ya kufanya mazungumzo na wawekezaji na kuingia mikataba ya utafutaji na uzalishaji kwa niaba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Sheria ya utafutaji mafuta kifungu namba 17. Waziri ndiye anayetoa na kusaini leseni za utafutaji mafuta na siyo *TPDC*.

(b) Kuwepo ama kuwepo kwa mafuta katika eneo lolote lile kunawenza kuthibitishwa kwa uchambuzi wa taarifa za kitaalamu ambazo zinatokana na uchimbaji wa visima vya utafiti katika eneo husika. Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa pamoja ziliteua mshauri mwelekezi kuangalia pamoja na mengineyo ni

jinsi gani Serikali mbili hizo zinaweza kuendeleza utafutaji wa mafuta katika maeneo ya Zanzibar na Pemba ambapo utafutaji unasuasua.

Pamoja na hayo, mshauri alipewa kazi kuchambua taarifa zilizopo na kutoa mawazo yake kama utafiti inabidi uendelezwe maeneo hayo. Mshauri mwelekezi aliona kuwa kwa taarifa ya kihistoria alizoonyeshwa mafuta yalikuwa hayajapatikana, yumkini alipendekeza ukusanyaji wa takwimu zaidi ufanyike ili tathmini nzuri iweze kufanywa. Ushauri huu aliutoa kwenye warsha ya Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla uwepo wa miamba tabaka *Sedimentary Rocks* ambayo kitaalamu duniani inafahamika kuwa na uwezekano wa kuandamana na mafuta Tanzania Bara na Visiwani zinaashiria uwezekano wa kuwepo kwa mafuta na gesi asilia na kwa maana hiyo uwekezaji zaidi unaweza ukaleta matokeo ya kina na ya uhakika zaidi kuhusu uwepo wa Nishati hizi.

(c)Mheshimiwa Spika, *TPDC* hawakutangaza kuwa Zanzibar hakuna mafuta. Katika warsha mbalimbali na taarifa wanazotoa *TPDC* kama ilivyo kwa maeneo mengine ya Jamhuri ya Muungano wanatoa taarifa ambazo ni matokeo ya tafiti zilizokwishawahili kufanywa na uwekezaji tofauti kwa upande wa tafiti zilizofanywa upande wa Tanzania Visiwani.

Tafiti hizo zimebaini ishara za uwepo wa mafuta yaani *Indications au traces* lakini kitaalam hiyo peke yake siyo ishara ya uwepo wa mafuta.

Hatua ya uwepo wa mafuta au gesi asilia inatambulika kitaalamu kama *discovery*. Hatua hiyo haijafikiwa na tafiti yoyote iliyowahi kufanywa Tanzania Visiwani.

Kama taasisi maalum kwenye nyanja ya mafuta ya *petrol TPDC* wana jukumu la kutoa ushauri wa kitalamu na Serikali ina jukumu la kufanya maamuzi yanayostahili.

Kwa maana hiyo, kama chombo cha kitaifa cha kitaalam na cha ushauri, *TPDC* wana dhamana ya kutoa maoni yao ya kitaalamu yenye lengo na dhununi la kujenga ili mradi maoni hayo yawe na makusudi ya kuboresha na kuendeleza juhudzi za Serikali zote za Tanzania za kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii wananchi wa Taifa letu yanayotokana na uchumi wetu wenyewe na raslimali zetu wenyewe ikiwemo Sekta ya mafuta na gesi asilia. Kufanya hivyo kutakuwa siyo kuingilia mambo yasiyowahu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mahitaji makubwa ya uwekezaji na teknolojia zinazohitajika kwenye masuala ya tafiti za mafuta na gesi asilia Wizara yetu inahimiza ushirikiano wa taasisi husika zote za Kiserikali na za Kibinafsi ikiwemo *TPDC* kuendeleza jitihada za makusudi kwa lengo la kuongeza na kuhamasisha uwekezaji katika sekta hii ambayo inaweza ikafungua milango minge ya kujikomboa kiuchumi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningeomba sana kutokana na unyeti wa suala hili, ungenistahimilia kidogo ili kuweka mambo sawa ndani ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Naomba ninukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ukurasa wa 15, kifungu (3), inasema kwamba, kutakuwa na mambo ya Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano na yale ambayo si ya Muungano ndani ya Jamhuri ya Muungano. Nilikuwa nataka nizungumzie hapo, sitaki kwenda kwenye sehemu kubwa.

**SPIKA:** Uulize swali siyo uzungumzie.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, Mheshimiwa Waziri katika kujibu swali lake amenukuu suala la mashirika ya umma. Suala la Mashirika ya Umma, *TPDC* si ya Jamhuri ya Muungano. Sasa swali:-

Hivi Mheshimiwa Waziri anaweza kukumbuka kwamba mwaka 1994, Mwalimu alifanya kikao cha Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Viongozi wengine hapa Dodoma, katika kuweka muafaka wa suala hili la mafuta na hatima yake kikawekwa kifungu namba 15 katika nyongeza hii kwamba suala la mafuta ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Pili, kutokana na kifungu hiki cha 15 ambacho kinajumuisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo Wizara yake si ya Muungano katika mambo haya yaliyotamkwa humu; Mheshimiwa Waziri anaweza akaliambia Bunge hili kwamba sasa kuna haja ya kuunda chombo maalum au Wizara yake ikawa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kusimamia suala hili la mafuta na kuondoa matatizo yaliyopo?

**SPIKA:** Hivi ndiyo bado hata mafuta yenyewe hatujayapata. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nadhani kwa bahati mbaya, hatuna muda wa kumpatia maelezo ya kina Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kuhusu kwa nini jambo hili la mafuta likawepo mikononi mwa *TPDC*. Uamuzi huu ulikuwa ni wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, wakati huo Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere. Uamuzi huu ulifanywa kwa makusudi, kwa sababu wakati huo dhamana ya kutafuta mafuta ilikuwa imeangukia chini ya Agip amba walirithi mkatuba huo kutoka kwa BP.

Baba wa Taifa akaweka mkakati wa kusema kwamba, tupate shirika ambalo litaangalia maslahi yetu ndani ya utafutaji wa mafuta na kwa maana hiyo, ikaundwa *TPDC*, ambayo kusema kweli kazi yake ndiyo imepelekeea kupata gesi Songosongo na Mnazibay. Baada ya matokeo ya Agip; Agip walichemsha wakasema Tanzania hatuna gesi, lakini *TPDC* wakaja wakasema hapana tutaendeleza utafiti na tutaendelea kutafuta wawekezaji. Kazi hiyo, ndiyo imeendelea kufanywa mpaka kwenye maeneo yote ya Tanzania Visiwani. Kwa hiyo, kazi ya *TPDC* kusema kweli ilikuwa ni *strategic* ya kulinda maslahi ya Tanzania yote. *Notwithstanding* kwamba, iliundwa na *Public*

*Cooperation Act*, ambayo nadhani ilikuwa ni wazo la msingi na la busara la wazee wetu wa Taifa miaka hiyo ya 70.

Kwa hiyo, pamoja na masuala aliyoyaeleza hapa Mheshimiwa Mbunge, nadhani tukubaliane tu kwamba, kuwepo kwa *TPDC* na kazi zinazofanywa za ukusanyaji wa data na kumbukumbu, sasa hivi inatuwezesha sisi kama Taifa kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kuwa na uwekezaji ambao ukija utafikia hapo hapo *TDPC* ili ufanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba Mheshimiwa Mbunge na sisi wengine wote, tufanye mkakati wa makusudi ili tuwapatie *TPDC* ushirikiano wa pande zote mbili. Tuhakikishe kwamba tunawahamasisha ili waweze kuendelea na tuhamasishe uwekezaji ndani ya sekta hii ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kuhusu umuhimu wa kuunda chombo cha kusimamia masuala haya. Sijui Mheshimiwa Mbunge hajafahamu, lakini masuala haya yapo katika vikao ambavyo vinasimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Masuala haya yanashughulikiwa kila wakati. Nimwambie tu kwamba, sisi wenyewe Wizara mbili; Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya MUNA ambayo SMZ inashughulikia masuala ya Nishati, tumepanga mkakati wa kuwa tunakutana mara kwa mara, kuzungumzia masuala yote bila kusubili vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Kwa hiyo, sidhani kama kuna haja tena ya kuunda chombo maalum kwa ajili ya masuala haya, wakati yanashughulikiwa na Wizara mbili na tunaendelea na mawasiliano ya mara kwa mara. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, naongeza dakika kama kumi ili tufike kasorobo kuweza kumaliza yaliyobaki haya.

Na. 13

### **Dawa Bora ya Ugonjwa wa Ukungu kwa Zao la Korosho**

**MHE. MOHAMED S. SINANI (K.n.y. MHE. RAYNALD A. MROPE)** aliuliza:-

Kwa kuwa Ugonjwa wa Ukungu unaoshambulia zao la korosho ni tishio kubwa linaloweza kuangamiza zao hili; na kwa kuwa wakulima hawafahamu vizuri ipi ni dawa bora kwa ugonjwa huo:-

(a) Je, Serikali inawaelezaje wananchi kuhusu dawa bora ya kutumia kupambana na ukungu?

(b) Je, dwa ya salfa ya maji iliyopo kwenye soko msimu huu ni bora kuliko salfa ya unga ambayo wakulima wengi wameizoea?

(c) Je, kupungua kwa mavuno ya korosho msimu huu kunatokana na nini; ni matumizi ya salfa ya maji, kucheleva kwa pembejeo ama hali ya hewa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, viuatalifu vyote vya kudhibiti Ugonjwa wa Ukungu wa Mikorosho, vimefanyiwa utafiti wa kina na Serikali katika taasisi zake za utafiti ikiwemo *TPRI* iliyopo Arusha. Aina zote hizo za viuatalifu zikitumiwa kama inavyoelekezwa na wataalam, vina uwezo mkubwa wa kudhibiti ugonjwa wa ukungu wa mikorosho.

Napenda kuchukua fursa hii, kuwafahamisha wananchi kwamba, dawa zote zilizoandikishwa kwa ajili ya kudhibiti Ugonjwa wa Ukungu wa Mikorosho zinafa kudhibiti Ugonjwa huo.

(b) Mheshimiwa Spika, dawa ya salfa ya maji na salfa ya unga zote zinafanya kazi sawa katika kuzuia ukungu wa mikorosho iwapo zitatumika kama inavyostahili.

(c) Mheshimiwa Spika, makadirio ya viwango vya uzalishaji wa korosho katika msimu huu wa 2008/2009, yanaonyesha kuwa uzalishaji utashuka kwa takriban asilimia 10 ikilinganishwa na uzalishaji katika msimu wa 2007/2008. Kwa kiasi kikubwa, kushuka kwa uzalishaji kumechangiwa na mabadiliko ya ghafla ya hali ya hewa na sio matumizi ya salfa ya maji.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kuna matatizo katika Kituo cha Utafiti cha Naliendele ya kukosekana kwa fedha za kufanya utafiti na kuathiri pia ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika mashamba ya utafiti katika nchi nzima, hali ambayo inasababisha kuathirika kwa utafiti wa zao la korosho; je, Serikali ina mpango gani kutatua tatizo hili hasa baada ya Mheshimiwa Naibu Waziri kupata nafasi kuja kutembelea na kujionea mwenyewe matatizo yaliyopo katika kituo kile? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nilitembelea Kituo chetu cha Utafiti cha Naliendele na nikaona matatizo yale. Bahati nzuri, Serikali ilishaanza kuyafanya kazi na muda si mrefu shilingi milioni 500 zitapelekwa kwenye Kituo kile ili shughuli za utafiti ziweze kuendelea na wafanyakazi wapatao 50 waweze kulipwa mishahara yao. (*Makofi*)

**Na. 14**

**Bei ya Mbolea ya Ruzuku**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa baa la njaa limeenea katika dunia nzima na pia nchi yetu ambayo ni maskini sana imekumbwa na baa hilo:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imetenga fedha kidogo sana kwenye ruzuku ya mbolea hivyo kutosaidia sana katika kupunguza bei ya mbolea na mbegu?

(b) Je, Serikali inasemaje juu ya ukweli kuwa, mbolea ya ruzuku imekuwa kidogo sana na haina tija katika uzalishaji wa chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzia msimu wa 2004/2005, dunia imekuwa ikikabiliwa na hali ya upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali kutoptaka na hali ya ukame na baadhi ya mataifa yanayozalisha nafaka kwa wingi kama Marekani, kuanza kutumia nafaka katika utengenezaji wa nishati mbadala (*bio-ethanol*).

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo kuongeza kilimo cha umwagiliaji, kuhimiza kilimo cha mazao yanayostahimili ukame na kuongeza matumizi ya mbolea na mbegu bora.

Aidha, Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha fedha za ruzuku ya mbolea na mbegu kila mwaka, kulingana na uwezo wake wa kifedha kama ifuatavyo:-

- Msimu wa 2003/2004 shilingi bilioni mbili zilifidia tani 39,387 za mbolea;
- Msimu wa 2004/2005 shilingi bilioni 7.244 zilifidia tani 81,766 za mbolea;
- Msimu wa 2005/2006 shilingi bilioni 7.5 zilifidia tani 63,000;
- 2006/2007 shilingi bilioni 19.5 zilifidia tani 89,941, za mbolea na tani 814 za mbegu bora;
- Msimu wa 2007/2008 shilingi milioni 19.5 zilifidia tani 82,005 na tani 1,1071 za mbegu bora; na
- Katika msimu huu wa 2008/2009, jumla ya shilingi bilioni 31.5 zimetengwa kwa ajili ya ruzuku ya mbolea na mbegu. Aidha, kutoptaka na kuongezeka sana kwa bei ya mbolea katika msimu wa 2008/2009, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 40 zilizotokana na fedha za EPA kwa ajili ya ruzuku. Kiasi hicho ni kwa ajili ya kufidia tani

155,000 za mbolea na tani 6000 za mbegu bora. Taratibu za kupatikana kwa fedha hizo zinakamilishwa.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kiwango cha mbolea ya ruzuku kinachotolewa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya mbolea hapa nchini. Mathalani, idadi ya wakulima waliostahili kupata ruzuku ya pembejeo kulingana na vigezo vilivyowekwa na wadau ni milioni 2.5 katika Mikoa 11 iliyio katika mpango wa ruzuku kwa sasa. Kutokana na ufinyu wa bajeti, idadi ya wakulima wanaonufaika na ruzuku ya pembejeo kwa mwaka 2008/2009 ni 700,000 tu.

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kwamba, tija katika uzalishaji wa mahindi kwa eneo katika maeneo yanayotumia mbolea ya ruzuku imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.1 kwa hekta hadi tani 1.5 kwa hekta. Uzalishaji wa jumla wa mahindi nao pia umeongezeka kutoka tani milioni 3.218 katika msimu wa 2004/2005 hadi tani milioni 3.593 katika msimu wa 2007/2008, sawa na ongezeko la asilimia 11.65.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika ni kweli kwamba, Serikali imekuwa ikijitahidi kutoa fedha nyingi sana kuweka ruzuku katika mbolea. Katika Bajeti ya Mwaka 2008/2009, wananchi wa Mikoa ile minne ya Kusini, wamewekewa ruzuku ya mbolea katika Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu, ambayo kwa hakika haionyeshi matumaini kwamba, mbolea ile inaweza kuzalisha mahindi ya kutosha badala ya *DAP*. Kwa kuwa wananchi wanalamika; je, Serikali ipo tayari kuweka ruzuku ya mbolea ya *DAP* katika bajeti yake ya mwaka 2009/2010 badala ya hii mbolea ya Minjingu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kinachohitajika kwenye kupanda ni *phosphorus* na mbolea ya Minjingu ina *phosphorus*. Wananchi wale walikuwa hawajapata elimu hasa ya kutumia mbolea hii ya Minjingu, kwa sababu mbolea hii ilikuja kwa wingi ikiwa katika unga unga wakati wakulima walizoea kutumia ile ya chenga. Sasa hivi tumekwishawaeleza wenye kiwanda hiki, wazalishe mbolea ya kutosha yenye chengachenga.

Pili, sisi Watanzania tunatakiwa tujali viwanda vyetu hapa nchini na tuhakikishe kwamba, tunatoa elimu kwa wananchi waweze kutumia *products* za viwanda vyetu hapa nchini badala ya kunufaisha viwanda vya nje. Tutaendelea kuwashamasisha wazalishaji waweze kutoa mbolea inayotakiwa. Kwa kuwa elimu ilikuwa haijafika kwa wananchi, sasa hivi Serikali inaendelea kutoa elimu. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuwaelimisha wananchi kwenye Halmashauri juu ya matumizi bora ya mbolea hii ya Minjingu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swali la mwisho la Wizara ya Maji na Umwagiliaji, linaulizwa na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nimekwishapokea nakala ya majibu nimeridhika, lakini kwa *format* naomba swalilangu namba 15 lipate majibu.

**SPIKA:** Sitakuruhusu uulize swalilangu nyongeza kwasababu umeridhika. Kwa hiyo, sasa majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

## Na. 15

### **Kukamilisha Mradi wa Bwawa la Mibono**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Bwawa la Mibono lilipatiwa fedha ambazo hazikumaliza Mradi huo na kusababisha fedha za Serikali kupotea:-

- (a) Je, Serikali inafanya juhudigani katikakumaliza Mradi huo?
- (b) Je, Serikali inakubali ushauri wa kuwa Miradi yote inayoanzishwa imalizwe kwanza kabla ya kuanzisha Miradi mipywa?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swalilangu Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji Maji Mashamba ya Mibono lenye ukubwa wa hekta 400 ilifanyiwa uchunguzi na usanifu katika mwaka 2004/2005, ambapo ujenzi wake ulikadiriwa kugharimu shilingi milioni 374. Katika mwaka wa 2005/2006, Serikali ilitenga shilingi milioni 120 kwa ajili ya kutekeleza awamu ya kwanza ya Mradi iliyojumuisha ujenzi wa banio la mto, mfereji mkuu wenyewarefu wa kilomita 1.5 na mfereji wa utoro wa maji (*spillway*).

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007, Serikali ilianza kutekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo (*ASDP*) ambayo utaratibusi wake unazitaka Wilaya kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) ili kuomba fedha ya utekelezaji. Kwa bahati mbaya, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilikuwa haijalewa vizuri utaratibusi huo. Kwa hiyo, kwa miaka miwili mfululizo; 2006/2007 na 2007/2008, Skimu ya Mibono haikuungizwa katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Sikonge. Tatizo hilo Serikali imeliona na katika mwaka wa 2008/2009, Mradi huo umetengwa shilingi milioni 150.

Fedha hizo zitatumika kujenga mifereji midogo ya umwagiliaji, itakayoingiza maji mashambani pamoja na tuta la kuzuia mafuriko. Matumaini yangu ni kwamba, sehemu kubwa ya kazi zilizoainishwa zitakamilika na mradi kuanza kufanya kazi. Hata

hivyo, kama kutakuwa na kazi ndogo zitakazobaki, Serikali itazikamilisha katika mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, miradi vipozo ndiyo inatakiwa ipewe vipaumbele kabla ya kuanza miradi mingine mipyga.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza:-

Kwa kuwa Bwawa la Kamayahalanga linafanana na la Mibono; na kwa kuwa katika bajeti ya 2008/2009 lilipangiwa fedha kwa ajili ya kuchimba Bwawa Kamayahalanga ambalo linachukua Kata ya Kamayahalanga na Kata ya Mogwa katika Jimbo la Bukene: Je, Serikali ina utaratibu gani kuhakikisha kwamba fedha hizo zilizopangwa zinaanza kazi mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Bwawa la Kamayahalanga ujenzi wake bado uko palepale kama tulivyopanga kuwa utatumia jumla ya shilingi milioni 500. Kinachochelewesha kazi sasa hivi ni ule mchakato wa kumpata Mkandarasi. Nafurahi kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwezi huu wa Februari, mchakato ule wa kupata Mkandarasi atakayejenga bwawa hilo, utakuwa umekamilika na tenda ya ujenzi itatangazwa. Kwa hiyo, hata kama kuna makandarasi hapa ndani, basi wakae mkao wa kusubiri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana; muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Sasa matangazo: Ninafurahi kutangaza wageni wetu waliopo, nikianzia kwenye *Speakers Gallery* kama ifuatavyo:-

Tunae Balozi wa Nchi ya Norway hapa Nchini, Mheshimiwa John Lomoy yule pale, *welcome to Parliament your excellency, its always pleasure to have our partners in development to visit Dodoma and be here in Bunge. Thank you very much.* Ameambatana na Bi. Jest Tromsdaw, ambaye ni *First Secretary* katika Ubalozi huo wa Norway; *thank you.* Wengine ni Mheshimiwa Clemence Harch, Naibu Balozi wa Ujeruman, *thank you very much. German is an important partner, we are happy to see you here and welcome please.* Anayefuata ni Hester Somsen, *First Secretary* wa Ubalozi wa Netherlands yule pale, *thank you very much for your visit. (Makof)*

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambao wapo kazini kwa ajili ya Muswada ambao hivi punde utawasilishwa; Ndugu Blandina Nyoni, Katibu Mkuu wa Wizara yule pale, Dkt. Deo Mutasiwa, Dkt. Donan Mbando, Dkt. Zakaria Berege, Dkt. Khalid Mansa, Bi. Patricia Maganga, Bwana E. Chinamo, Bwana Idd Hayanga, Bi. Jackline Makupa, Bwana Amour Sulemain, Dkt. G. Dossy, Bwana E. Mashimba, Bibi Margreth Ndomondo Sigonda, Ndugu Kessy Mgonera, Dkt. Kitua na Bwana George Kameka. Tunawakaribisha sana katika Shughuli za Bunge.

Wageni wa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella wa Ukerewe ni kama ifuatavyo:- Bwana Japan ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Ukerewe, bwana Mashaka ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Nyamagana Mwanza, huyu nadhani pia mgeni wa Waziri Masha na Bwana Mfungo, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana Ilemela Mwanza. Ahsante. Karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wa Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame ni Bwana Ben Mwabasi Mbore, yule pale na Bwana Arthur Kabeha, yule pale; karibuni sana. (*Makofii*)

Matangazo shughuli zetu: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mweyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo, wakutane saa 5.00 asubuhi hii katika Ukumbi Namba 219 Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, ameniomba niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kwamba, kutakuwa na Kikao cha Kamati leo saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Halima Mdee, *Assistant Chief Whip* wa Kambi ya Upinzani, ameniomba nitangaze kwamba, Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, wahudhurie kikao cha Kambi hiyo leo saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Kasusura.

Mheshimiwa Dkt. Zainab Gama, Mwenyekiti wa APNAC, ameniomba nitangaze kwamba, kutakuwa na Mkutano wa Kamati ya Utendaji ya APNAC leo tarehe 27 saa 7.00 mchana na kikao hicho kitafanyika katika Chumba Namba 133.

Waheshimiwa Wabunge, mmegawiwa karatasi hii ambayo inaonyesha ratiba ya Shughuli za Mkutano huu wa Kumi na Nne, naomba sana muizingatie kwa sababu ndiyo inaonyesha shughuli ambazo zitakuwa zinafanyika, kwa mfano, leo ni Muswada ule wa *Public Health Bill*, kwa siku nzima hadi jioni. Kesho kuna Miswada miwili. Kwa hiyo, ili mtu usibabaike ni vizuri kuzingatia yaliyomo humu na kama yatakuwa yanabadilika kulingana na mjadala, basi tutatangaza pia.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii, kuwapa pole wote ambao wamepatwa na masaibu ya kila namna, tangu tulipokutana mara ya mwisho katika Mkutano wa Kumi na Tatu. Hizo ndiyo njia za Mwenyezi Mungu na hakuna namna ya kuepuka.

La pili, naomba niwapongeze wale wote ambao kwa namna moja au nyingine, katika vyama vyao vya siasa ama wamepanda vyeo au wamechaguliwa. Kipekee, nafahamu wapo Wabunge Wanawake wa CCM wengi ambao katika Jumuiya ya UWT wamechaguliwa tena kwa kishindo katika nafasi mbalimbali. (*Makofii*)

Kwa hiyo, siwezi kuwataja leo kwa sababu wala sijapewa orodha kamili, nimekuwa nikifutilia kwenye magazeti tu lakini kwa wakati muafaka nitawataja.

Kipekee, labda nimirata tu ingawa hayupo Mheshimiwa Sophia Simba, ambaye ndiye Mwenyekiti wa UWT Taifa. (*Makofi*)

Naelewa kwenye chama cha CHADEMA kumekuwa na upandishwaji vyeo, nayo sijapata rasmi wengine wamekuwa Wakurugenzi, wengine Wakurugenzi wasaidizi, basi nawapongeza sana kwa hayo. (*Makofi*)

Sijapata taarifa yoyote kutoka *CUF* na wala sijasoma katika vyombo nya habari, kama kuna mabadiliko yoyote ya vyeo. Kwa hiyo, kama yapo basi naomba Uongozi *CUF* wanipatie niweze kuutolea taarifa rasmi katika Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo nina udhuru ofisini, ninamwomba Mheshimiwa Naibu Spika aweze kuja ili aendeleze shughuli zilizosalia.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, habari za asubuhi?

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Nzuri.

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii wa Mwaka 2008**  
(*The Public Health Bill, 2008*)

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii wa Mwaka 2008 (*The Public Health Bill, 2008*), kama ulivyopangwa katika Orodha ya Shughuli za leo, pamoja na jedwali la marekebisho ambalo hivi punde litagawiwa, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, kabla sijaanza kuwasilisha hoja yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Shabani Kwaang', Mbunge wa Babati Mjini, kwa kuchambua kwa kina Muswada ulioko mbele yenu na kutoa michango na maelekezo ambayo yameniwezesha kuwasilisha Muswada huu hapa Bungeni siku ya leo.

Aidha, naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hususan Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hatua zote walizotekeleza hadi kukamilisha Muswada huu. Vile vile shukrani za dhati, ziwaendee wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine, walichangia maoni yao katika hatua za awali za maandalizi na hatimaye katika kukamilisha Muswada huu. Mchakato wa kuandaa Muswada huu, umechukua muda mrefu na ulishirikisha wadau wengi na hasa Halmashauri zetu, ambao ndio hasa wadau wakuu na watekelezaji wakuu wa sheria hii inayopendekezwa.

Naomba pia niwatambue ambao walishiriki kutoa maoni yao, wakati Muswada huu ulipojadiliwa katika kikao cha Kamati ya Huduma za Jamii. Wadau hao ni hawa wafuatao: *Legal and Human Rights Centre, National Organization for Legal Assistants, Tanzania Public Health Association, Youth Action Volunteers na Muhimbili University of Health and Allied Sciences*. Michango yao ilisaidia kuboresha Muswada uliopo mbele yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa na mabadiliko makubwa ya kisiasa, kijamii, kimazingira na kiuchumi tangu tupate uhuru. Katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kumekuwa na mabadiliko yenyе lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Hivyo, kuna umuhimu wa kutunga sheria mahususi ya afya ya jamii, ambayo itajulikana kama Sheria ya Afya ya Jamii. Sheria hii inayopendekezwa ni pana na mtambuka, kwa sababu inabeba mambo yote ambayo yanahusiana kwa njia yoyote ile na afya na uhai wa mwanadamu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla katika mazingira anayoishi au anayofanya kazi. Kwa misingi hiyo basi, afya ya binadamu inaweza kuathirika kutokana na shughuli zake au mambo yanayotokana na mabadiliko katika hali ya mazingira. Shughuli hizo ni pamoja na zile zinazomuwezesha kupata chakula na riziki, makazi na mavazi katika kudumisha uhai wake. Ni kwa misingi hiyo, sheria inayopendekezwa imegusa maeneo yote muhimu ambayo yanahitaji kudhibitiwa katika mazingira ya binadamu kwa lengo la kudumisha afya na uhai wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008, Umoja wa Mataifa uliupanga mwaka huo kuwa mwaka wa kimataifa wa usafi wa mazingira. Hivyo, Muswada huu umewasilishwa wakati muafaka, ambapo nchi yetu itakuwa imetekeleza moja ya mikakati yake ya kuwa na sheria itakayodhibiti masuala ya usafi wa mazingira ili kufanikisha malengo ya milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zinazosimamia masuala ya afya ya jamii zipo nyingi hadi sasa na zimekuwa katika sheria mbalimbali, yaani *scattered* na hivyo kufanya usimamizi wake kuwa mgumu. Hali hii imeweka dhahiri umuhimu wa kuwa na sheria mahususi, yaani *comprehensive legislation* itakayojumuisha masuala yote ya afya ya jamii. Aidha, machimbuko mengine ni kama yafuatayo:-

Kwanza, sheria za afya ya jamii zilizopo hazikidhi mazingira ya sasa kutokana na magonjwa mbalimbali yaliyoibuka, kwa mfano, *Ebola, SARS*, homa kali ya ndege, yaani *Avian Influezer, Rift Valley Fever* na kadhalika. Pili, kumekuwa na maendeleo makubwa ya sayansi na kiteknolojia. Tatu, kumekuwa na mabadiliko katika sera ya nchi yaliyosababisha kupanuka kwa sekta binafsi hapa nchini. Katika kutoa huduma za afya ya jamii, ipo haja ya kudhibiti utendaji wa sekta hii.

Nne, sheria za afya ya mazingira zilizopo hazikidhi mazingira ya sasa, kutokana na magonjwa mbalimbali yanayoibuka, yaani *imaging and remerging diseases*. Sheria hizi nyingi zilitungwa wakati wa ukoloni. Tano, kumekuwa na ongezeko la magonjwa yatokanayo na uchafuzi wa mazingira, ikiwemo kipindupindu. Sita, magonjwa ya saratani yameongezeka. Saba, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na biashara

mbalimbali. Nane, jitihada za Serikali katika kuboresha huduma za afya ya jamii ili itolewe kwa viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa maandalizi ya Muswada huu, mambo yafuatayo yalizingatiwa: Moja ni Sera ya Afya ya Mwaka 1990, ambayo ilirekebishwa mwaka 2007. Pili, ni dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi, yaani *decentralization by devolution* kwani Muswada umezingatia kuwa watekelezaji wakuu wa sheria inayopendekezwa ni jamii na wataalamu wa afya ya mazingira walioajiriwa katika Serikali za Mitaa.

Tatu, kubainisha aina ya wadau watakaojihusisha na utoaji wa huduma za afya ya jamii na usafi wa mazingira. Nne, kushughulikia huduma ya afya ya jamii na usafi wa mazingira nchini. Tano, kuweka vipengele vya sheria ambavyo vitasimamia utekelezaji, viwango na miongozo, ili kuboresha usimamizi na ufuatilaji wa afya ya jamii na usafi wa mazingira kwa ujumla. Sita, kuweka bayana makosa na adhabu zitakazotolewa kwa wale watakaokiuka matakwa ya sheria inayopendekezwa. Saba, kutokana na upana wa sheria inayopendekezwa, sheria zifuatazo itabidi zihuishwe. Moja ni ile ya NEMC ya Mazingira, TFDA, OSHA na *The Township Ordinance Cap. 101*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ukipitishwa na kuwa sheria na kutekelezwa ipasavyo, inatarajiwa kwamba, italeta matokeo yafuatayo: Itaweka utaratibu wa kusimamia utoaji wa huduma za afya ya jamii na usafi wa mazingira kwa kuzingatia mabadiliko ya sera na mfumo wa utoaji huduma za afya nchini, yaani *Health Sector Reform*. Tunategemea kwamba, italeta mabadiliko na kuboresha utendaji kazi kulingana na maendeleo ya teknolojia na kutoa miongozo inayohusu afya ya mazingira kwa jamii. Tunategemea kwamba, itaongeza makali ya adhabu kwa watakaokiuka utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Vilevile itampa uwezo Waziri mwenye dhamana ya Afya, kutengeneza kanuni chini ya sheria hii, ili kuweza kutekeleza kikamilifu sheria hii. Mwisho ni kufutwa kwa Sheria ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Mwaka 1920, yaani *The Infectious Diseases Act, 1920*; Sheria ya Kudhibiti Mazalia ya Mbu ya Mwaka 1935, yaani *The Mosquito Control Health, 1935*; na Sheria ya Magonjwa yanayotolewa Taarifa Kimataifa ya Mwaka 1964, yaani *The International Notifiable Diseases Act, 1964*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa mambo niliyoyataja, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba: Sehemu ya kwanza, inatoa maelekezo ya awali, yaani jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria na tafsiri ya maneno na misamiati mbalimbali iliyotumika katika Muswada huu. Sehemu ya pili, inahusu masuala ya kiutawala au kiutendaji. Muswada unaainisha majukumu ya Waziri mwenye dhamana ya afya ili kuhakikisha kuwepo kwa huduma ya afya ya jamii zinazokubalika nchini, pia sehemu hii inabainisha majukumu ya mamlaka ya Serikali za Mitaa, katika usimamizi na uboreshaji wa viwango vya afya ya jamii, katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na mamlaka ya kutunga sheria ndogo katika kurahisisha utekelezaji wa sheria hii.

Kutokana na hilo, sehemu hii inapendekeza uwepo wa maafisa waliodhinisha majukumu na haki ya kuingia katika sehemu yoyote ile kwa lengo la kukagua, endapo

sehemu au eneo au kifaa kinakidhi viwango nya sheria. Kwa sababu hiyo, Serikali imetoea kinga kwa maafisa hao kutoshtakiwa pale tu kwa nia njema, wanapofanya makosa wakati wanapotekeleza majukumu yao chini ya sheria hii.

Sehemu ya tatu, inapendekeza utoaji wa taarifa zinazohusu magonjwa ya kuambukiza, kuzuia na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza, chanjo kwa watoto dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, kuzuia na kudhibiti milipuko ya magonjwa, kuangamiza mazalia ya mbu, wadudu na wanyama waharibifu na kuhakikisha magonjwa ya kuambukiza yasiingie nchini toka nchi nyingine. Aidha, sehemu hii inatoa majukumu kwa maafisa mbalimblai wenye wajibu wa kutoa taarifa za magonjwa husika na njia wanazoweza kutoa, kutumia ama kufikisha taarifa hizo.

Sehemu ya nne, inahusu masuala ya usafi wa mazingira na nyumba kwa ujumla. Sehemu hii pia inahusu masuala yanayohusiana na machukizo mbalimbali ya kiafaya, makazi, nyumba, kuhifadhi na kutupa takataka zikiwemo taka ngumu na taka maji, mazishi na makampuni yanayohusika na masuala ya mazishi na nyumba ya kuhifadhia maiti na jinsi ya kuhifadhi maiti, uanzishaji na uendeshaji wake.

Sehemu ya tano, inapendekeza masuala ya chakula, usafi wa chakula, maduka ya chakula zikiwemo *supermarkets*, sehemu za kuuzia chakula, maeneo ya masoko, kushughulikia vyakula vibovu, machinjio, maeneo yanayohusika kutengeneza, kuhifadhi na kuuza chakula. Aidha, sehemu hii inampa Waziri mwenye mamlaka ya Afya, mamlaka ya kutengeneza kanuni ya jinsi ya kushughulikia vyakula vibovu au visivyofaa kwa matumizi ya binadamu ili kuilinda jamii. Vilevile sehemu hii inahusu machinjio ya mifugo na uendeshaji wake, ikiwa ni pamoja na usafi wa mazingira katika maduka ya nyama.

Sehemu ya sita, inahusu uanzishaji na uendeshaji wa nyumba za kulala wageni, hoteli, sehemu za kutengeneza au kunyoa nywele, sehemu za kuogelea, viwango vinavyokubalika kiafya kabla ya mtu kuendesha shule na ukaguzi wake na inatoa adhabu pale shule inapokutwa imekiuka sheria ya afya ya jamii.

Sehemu ya saba, inapendekeza masuala ya jumla yakiwemo masuala ya afya ya wafanyakazi sehemu za kazi. Waziri mwenye dhamana ya Afya amepewa mamlaka ya kutengeneza kanuni, kuhusu huduma za afya kwa wafanyakazi na afya ya mazingira au sehemu ya kazi na kuzuia utangazaji wa taarifa za afya ya jamii bila kibali chake.

Sehemu hii pia inaainisha makosa na adhabu mbalimbali na imetoea pia masharti ya uendeshaji wa sehemu za kuuzia pombe na vyakula. Aidha, sehemu hii inapendekeza kufutwa kwa baadhi ya sheria, pamoja na masuala ya mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, baada ya kutoa maelezo haya, kwa heshima kubwa naomba Waheshimiwa Wabunge wajadili Muswada ulio mbele yao na kuupitisha ili hatimaye uweze kuwa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2008, yaani *The Public Health Act, 2008*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, yanayohusu Mswada wa Afya ya Jamii (*The Public Health Bill, 2008*).

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, Kamati ya Huduma za Jamii inatoa pongezi za dhati kwa Dr. Thomas Kashilila, kwa kuteuliwa rasmi na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu wa Bunge. Tunamtakia kila la heri na kumhakikishia ushirikiano wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunakutakia Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika na Wabunge wote, heri na baraka kwa mwaka mpya 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata nafasi ya kujadili Muswada huu katika vikao viwili, ambapo kimoja kilifanyika katika Ukumbi Mdogo wa Bunge Dar es Salaam na kingine kilifanyika Dodoma. Katika kikao cha kwanza, kilichofanyika tarehe 13 Oktoba, 2008 Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, alitoa maelezo ya jumla juu ya madhumuni ya Muswada na yaliyomo kwenye vipengele vyake.

Kikao hiki kiliwashirikisha baadhi ya wadau wa sekta ya afya wakiwemo *National Organization for Legal Assistance* (nola); *Youth Action Volunteers; Tanzania Public Health Association*; na Kituo cha Haki za Binadamu na wengine.

Kamati inawashukuru sana, wadau wote walioshiriki na kutoa maoni yao ambayo yamezingatiwa na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika kuishauri Serikali ili iyazingatie katika Jedwali la Marekebisho ya Muswada wa Sheria hii ya Afya ya Jamii.

Katika kikao cha pili ambacho kilifanyika tarehe 31 Oktoba, 2008 hapa Dodoma, Kamati ilizingatia maoni ya wadau, maoni ya Mwanasheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, pamoa na ufanuzi uliotolewa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayopendekezwa imegusa maeneo yote muhimu ambayo yanahitaji kudhibitiwa kwa lengo la kudumisha Afya na Uhai wa binadamu. Kwa kuwa Sheria zinazosimamia Afya ya Jamii zinasimamiwa na Sheria mbalimbali na hivyo usimamizi wake kuwa mgumu. Kamati yangu inakubaliana na Serikali kuwa na Sheria moja itakayosimamia shughuli zote za Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Huduma za Jamii katika kuunga mkono Muswada huu wa Afya ya Jamii, imezingatia pia mabadiliko makubwa ya Kijamii,

Kiuchumi na Mazingira yanayoendelea na pia kuibuka kwa mambo mbalimbali kama vile: Magonjwa mapya kama *Ebola*, *SARS*, *Avian Influenza*, *Rift Valley Fever* na kadhalika; Kuongezeka kwa magonjwa yatokanayo na uchafuzi wa mazingira kama vile kipindupindu; Kupanuka kwa sekta binafsi hapa nchini katika kutoa huduma za Afya ya Jamii pasipo udhibiti wa kutosha; na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na biashara.

Hivyo, kutokana na changamoto hizi, kuna umuhimu mkubwa wa kuwa na Sheria mpya ya Afya ya Jamii ili kuiwezesha Serikali na Jamii nzima kwa ujumla, kuboresha huduma za afya na kusimamia kwa ukamilifu viwango vya utoaji wa huduma za Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia imejadili na kukubaliana na Serikali kuwa, kwa kiwango kikubwa, Muswada umezingatia mambo muhimu ya Sera ya Afya kama ilivyorekebishwa 2007; usimamizi wa Sheria hii katika ngazi za Serikali za Mitaa; na aina ya wadau watakaojihusisha na utoaji wa huduma za Afya. Vilevile Sheria hii katika kuboresha huduma za Afya ya Jamii, itafuta Sheria ya Magonjwa ya kuambukiza iliyotungwa tangu mwaka 1920. Pia, Sheria ya kudhibiti mazalia ya mbu iliyotungwa tangu 1935 na Sheria ya Magonjwa yanayotolewa taarifa ya Kimataifa ya mwaka 1964.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipitia sehemu, ibara na vifungu vya Muswada na kuishauri Serikali kuptita Mwanasheria Mkuu kurekebisha ibara, maneno na sentensi ili yaendane na Luga ya Kisheria (*Legal Language*) na Jedwali la marekebisho liletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Baadhi ya maeneo ambayo yalioainishwa na Kamati ni kama yafuatayo:-

- (i) Katika yaliyomo (*table of contents*) maneno yote yapitiwe na kufanyiwa marekebisho.

**SEHEMU YA IV**

Kichwa cha habari, neno “Anitation” lisomeke “Sanitation.”

**SEHEMU YA V**

Kichwa cha habari, neno “Natrition” lisomeke “Nutrition.”

- (ii) Katika sehemu ya ndani ya Muswada:

**SEHEMU YA I**

Utangulizi (*Preliminary Provisions*) kifungu cha tatu, tafsiri ya maneno yaliyotumika yarekebishwe ili yaendane na Luga ya Kisheria.

**SEHEMU YA II**

Kifungu cha 4(I) neno “Tanzanians” lisomeke “Tanzania”.

**SEHEMU YA III**

Kifungu cha 9, kiwekwe kifungu cha ziada ili kujumuisha masuala yanayohusiana kama ya usalama wa kiafya katika uvuvi, madhara ya kemikali, uchimbaji wa madini, mabadiliko ya hali ya hewa na kadhalika.

Vile vile vifungu vya 16, 36, 39, 44, 47(I)(a), 48(1) na 49 vifanyiwe marekebisho kuzingatia matumizi ya maneno, mkato na nukta.

#### SEHEMU YA IV

Makosa ya uchapaji kifungu cha 57(2)(c) neno “Whet” lisomeke “What.”

Kifungu kipyga cha 73(8) kinachohusu wajibu wa Mamlaka zinazohusika na uzoaji wa taka kuchunguza Afya za Wafanyakazi wanaowaajiri kila baada ya miezi mitatu kifungu hicho kiongezwe.

#### SEHEMU YA V

Marekebisho kwenye vifungu vya matumizi ya maneno yafanyike kama neno “may” na “shall” kwenye sehemu zinazohusika.

Kifungu cha 148, kuwepo na utoaji wa notisi ya maandishi kabla ya kufunga na kusitisha leseni za kuendesha biashara, maduka na masoko. Hivyo, kuwepo na kifungu kipyga cha 148(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho mengine ni kama yatakavyoletwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii katika Jedwali la Marekebisho.

Mwisho, matumaini ya Kamati ni kuwa baada ya Muswada huu kuwa Sheria, Serikali itaweka utaratibu mzuri kwenye kanuni ili Sheria hii iweze kueleweka kwa Wananchi na inapowezekana tafsiri ya Kiswahili ni muhimu kwa ajili ya kuleta ufanisi wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa (Mb), Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda (Mb) na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa ushirikiano wao wakati wa kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa kutoa maoni yao katika kuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati waliochambua Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Omar S. Kwaangw’ - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Haji Mwita Haji – Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Haroon Ali Suleiman, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Dkt. Samson F. Mpanda, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa

Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Dr. Lukas J. Siyame na Mheshimiwa Fatma Abdullah Tamim.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Kamati hii, Ndugu Hosiana John, kwa kuratibu vikao vya Kamati hadi maoni haya kutoka katika muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI – MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa uzima na nguvu za kuweza kusimama hapa mbele yenu ili kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii wa Mwaka 2008 (*The Public Health Act, 2008*) kwa mujibu wa kanuni za Bunge, kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kutoa salamu za mwaka mpya wa 2009 kwako wewe binafsi Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na wapiga kura wangu wa Jimbo la Konde. Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa sana, kwa Viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na timu nzima ya wataalam, kwa kazi kubwa ya kuandaa Muswada huu, japokuwa kuna upungufu wa hapa na pale, ambao tunaamini ukirekebishwa uleta dhana nzima ya dhumuni la kuanzishwa kwa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Muswada huu umejikita zaidi katika viashiria na vyanzo vya maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa kujikita zaidi kwenye Huduma za Afya za Serikali za Mitaa. Haukuongelea kuhusu usalama wa kemikali (*chemical safety*) na ni vipi kuzuia magonjwa yasiyoambukiza (*non-communicable diseases*) kama vile kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa, usalama wa kemikali umeainishwa katika Sheria ya *Industrial and Consumer Chemicals Management Act, 2003*; hivyo, ingekuwa ni bora angalau sheria hii ikatajwa katika Muswada huu wa Afya ya Jamii wakati wa kuongelea usalama wa kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tafsiri ya neno “*nuisance*” zaidi ya maneno ambayo yanetolewa tafsiri yake, Kambi ya Upinzani inashauri pia kiongezwe kifungu kipyga cha (h) kinachosema *unpleasant to others*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sehemu ya III (a) “*Notification.... Non Communicable Diseases...*” Magonjwa haya ambayo hayaambukizi limekuwa ni suala kubwa la afya ya jamii. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga kasma maalum ili kuanzishwa kwa vituo vya kufanya mazoezi na kutoa hamasa kwa wananchi kushiriki mazoezi ili kupunguza kama si kuondoa kabisa, tatizo la magonjwa yasiyoambukiza. Hili litachangia kubadili mtazamo wa wananchi kuhusiana na maisha yao ya kila siku. Aidha, Serikali ipige marufuku uvutaji wa sigara katika sehemu za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tisa kinachohusu utoaji wa tahadhari ya magonjwa ya muambukizo (*notification of infectious diseases*); ukiangalia jedwali la kwanza limeweka vilevile hali ya utapiamlo (*Malnutrition*) na huu sio ugonjwa, bali ni hali inayotokana na ukosefu wa lishe bora. Kambi ya Upinzani inashauri vilevile iongezwe “*pesticide poisoning*” katika jedwali la kwanza. Aidha, katika “*margin heading*” ya kifungu cha tisa isomeke kama ifuatavyo: “*Notification of Infectious Disease/Condition.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na *non-communicable diseases/condition*, kuna jambo ambalo kwa kiasi kikubwa, limekuwa na usumbufu ambalo limesababisha kupotea kwa maisha ya Watanzania wengi wasio na hatia. Suala la mtu aliyepata ajali, kukataliwa kupata haki ya kutibiwa mpaka kwanza kujaziwa Fomu ya PF3, Kambi ya Upinzani inajua kwamba kiapo kikubwa cha Daktari ni kuokoa maisha ya mgonjwa; hivyo, pale anapoletwa majeruhi wa aina yoyote, kazi yake ya kwanza ni kumpatia huduma na baadae ndipo itolewe taarifa kwa vyombo vya dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamepoteza maisha yao kutokana na utaratibu huu wa PF3. Tunaitaka Serikali kuliangalia upya suala hili la PF3 ili afya ya jamii iweze kuzingatiwa, kwani tunaamini kuwa, *non-communicable disease* inaweza kuwa chanzo cha *communicable disease* na madhara mengine yanatokea kutokana na suala la PF3

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 73(7), kinatoa adhabu ya shillingi laki moja au kifungo kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote kwenda sambamba, kwa mtu au kampuni ambayo imeshindwa kuwapatia wafanyakazi wake vitendea kazi kwa ajili ya kulinda afya zao. Kambi ya Upinzani inaona adhabu iliyotajwa katika Muswada huu ni ndogo sana. Kwa vile afya ya binadamu haiwezi kuthaminishwa na kitu chochote, hivyo basi, adhabu kali ilitakiwa iwekwe ili iwa fundisho kwa wale wote wanaocheza na afya za wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya VI katika kifungu cha 162 cha Muswada, kifungu kizima kinazungumzia shule na vyuo tu, lakini hakiongelei kuhusu vyuo vya elimu ya juu. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, itakuwa ni bora na vyuo vya elimu ya juu navyo vikaingizwa katika kadhaa hii na ikibidi hata vile ambavyo tayari vimeanzishwa, vikaguliwe upya kuona kama vinaendana na matakwa ya Muswada wa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyatoa machache hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, naona wale wasemaji wakuu wameshamaliza kusema. Mpaka sasa nina wachangiaji sita na kwa sababu ni Muswada wa siku moja, idadi inaweza kuongezeka kidogo. Kwa kuanzia, naomba nimwite Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Paschal Degera na Mheshimiwa George Malima Lubeleje ajiandae.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunirudishia afya yangu tena njema kabisa, baada ya matibabu makubwa yaliyofanywa na daktari wangu. Kwa kweli nimpongeze sana Dkt. Tosirio wa Hospitali ya Aga Khan, kwa kazi nzuri anayowafanya wagonjwa wote katika nchi yetu ya Tanzania. Mungu amzidishie maisha marefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitumie ...

**NAIBU SPIKA:** Sema na Madaktari wengine jamani!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na Madaktari wengine. Namkumbuka yeeye kwa sababu kwa kweli amefanya kazi maalum kwangu na kuniongezea uhai ambao Mungu amenipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia niwatakie Waheshimiwa Wabunge wote kheri ya mwaka mpya, lakini hasa wapiga kura wangu wa Jimbo la Peramiho na niwashukuru kwa jinsi tunavyoendelea kuwa pamoja; pamoja na mambo mengi ambayo tunayafanya ya kimaendeleo basi tunaendela vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWT *wing* ya Chama cha Mapinduzi Tanzania. Vilevile nimpongeze Dkt. Kashilillah kwa kuthibitishwa sasa na kuteuliwa rasmi kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umefika wakati muafaka kabisa na niseme ninaipongeza sana Kamati ya Huduma za Jamii, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwa kazi zuri waliyoifanya, lakini nitambue juhudzi za Serikali yetu kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ikiongozwa na Waziri wetu, Mheshimiwa Profesa Mwakyusa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kazi nzuri na kuona umuhimu wa kuleta Sheria hii kwa sasa. Nikifuatilia maelezo ya Mwenyekiti wa Kamati, Muswada wenyewe umejitosheleza lakini nilikuwa na mambo mawili, matatu ya kushauri katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, sehemu ile ya kwanza ambayo inatoa tafsiri ya maneno ukurasa wa 11 kumetolewa *definition* wa *dairy farm* kwa maana ya *includes any farm-house, ...milk-shop or other place* ambazo zitakuwa zina-supply *milk* kwa matumizi ya kuuza, kwa matumizi ya kutengeneza *butter, dried milk* na mambo mengine. Mimi nadhani tuongeze pia kwa matumizi ya nyumbani. Matumizi ya nyumbani hayakuwekwa, sijajua ni kwa sababu gani hayakuwekwa hayo maziwa ambayo

yatakuwa *produced* kwenye ile *dairy farm*. Nadhani Mheshimiwa Waziri aangalie, nafikiri kuna umuhimu pia na tumeona contamination kubwa sana ya maziwa hasa yanayotumiwa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, ambayo yamekuwa yakiuzwa kwa wateja mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 14, kumetolewa *definition* ya *septic tank* anasema *means a masonry structure*. Kama tukisema *masonry structure* ni *structures* ambazo ni *permanent* lakini kwa nini tusiongeze hata zile *short term tanks* ambazo wakati mwingine zimekuwa zikitumika pia kwa ajili ya kukusanya hizo *biological wastes* na vitu vya namna hiyo. Kwenye sherehe siku hizi za harusi na nini utakuta kuna vyoo ambavyo ni *mobile*, watu wanajisaidia wanajaza kwenye makontena ambayo huyaoni yaliko lakini sasa sijui kwa nini hiyo nayo hawajaifikiria kusudi na yenewe tuone tunaweza tuka-control namna gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Muswada huu pia ukurasa wa 32 unazungumzia *inspection* ya *imported used clothes* na *foot wears*. Pale kwa kweli nadhani kunatakiwa kuwekwa msisitizo sana sana. Nchi yetu imekuwa iki-*import* nguo hizo na viatu na kwa kweli sheria hii nafikiri isimamie sana na ninaamini kabisa tunaposema *clothes* tunamaanisha *clothes* za aina yote. Maana yake sasa hivi mpaka *underwear* zimekuwa *imported* na zinavaliwa kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, nadhani pale kungewekwa wazi kabisa ili kuwa na msisito wa kufanya *monitoring* ya hayo ambayo nimeyazungumza.

Nikija kwenye masuala ya jumla, niseme tu kwamba, Muswada huu unaendana kabisa na mpango wa maendeleo wa mwaka 2008/2009 na ukiangalia katika ukurasa wa 59 wa Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2008/2009, unakuta kuna Mikakati Maalum kabisa ya Wizara ya Afya, ambayo inaelezea ni namna gani sekta hii ya huduma ya afya inaweza ikaboreshwa kwenye nchi yetu. Ukiangalia yale yote yaliyoolezwa pale, kama yasingetungiwa Sheria Mama, isingweza kusaidia kabisa kuhakikisha kwamba haya ambayo tunayazungumza kwenye Muswada yanazingatiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, afya mahala pa kazi ni tatizo kubwa sana. Kamati yangu ya Maendeleo ya Jamii, inafanya kazi na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Ndani ya Wizara hiyo kuna kitengo cha OSHA, kinachozingatia suala zima la usalama na afya mahala pa kazi. Kamati yangu imekuwa ikifanya ziara mbalimbali na kukagua maeneo ya kazi na kuangalia ni namna gani wafanyakazi wamekuwa wakilindwa kwa afya zao. Yapo maeneo mengine ni hatari kubwa sana, sasa maadam Muswada unataka kumpa nguvu pia Waziri mwenye dhamana ya Wizara ya Kazi, kutunga Kanuni ambazo zitasaidia sana kuwalinda wafanyakazi, afya zao kwenye mahali ambako wanafanya kazi; hili ni jambo la msingi na mimi nalipongeza na naliunga mkono kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakutana na wazoaji takataka, huwezi kuamini wale ni wafanyakazi na ni wanadamu wenzetu. Hakika ni hatari, nani anawalinda hakuna anayejulikana. Hali ni hatari, huwezi kutoa hata maeleo wanafananaje, lakini nani anayewalinda watu hawa na wala hawafanyi vile kwa kupenda; ni kwa sababu hakuna

Sheria inayowalinda ili kuhakikisha afya zao zinakuwa salama. Hata ukienda viwandani, ukusanyaji wa taka, maji yanayotumika yenyeki kemikali katika suala zima la uhifadhi wa mazingira ni hatari tupu na sheria hii kwa kweli itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie lingine la jumla; tumekuwa na tabia ya kuzungumzia sana tiba badala ya kinga. Nadhani Sheria hii itatupa nguvu kujikita zaidi kwenye kinga. Tatizo la Malaria katika nchi hii, vifo vya wajawazito na watoto, asilimia kubwa vinatokana na malaria. Mimi nasema tatizo la UKIMWI haliu kama malaria, malaria inaangamiza watu wengi sana katika nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara, lakini vilevile katika nchi yetu ya Tanzania, pamoja na juhudhi kubwa za Serikali yetu lakini nadhani suala la kuamua kwa makusudi mazima kupitia Sheria hii kuhakikisha vyandarua vinafanyiwa matumizi yake kama yalivyokusudiwa kuua viatilifu vinavyosababisha malaria. Kulikuwa na ule Mpango wa DDT sijui imekwenda wapi?

Nadhani Mheshimiwa Waziri, angetupa pia taarifa ya mafanikio ya mpango wa kupuliza dawa ile ili kuua wadudu wanaoweza kusababisha malaria. Uchafu kwenye maeneo ya masoko, uchafu kwenye maeneo ya Stand za Bus, mifereji ya maji; ni uchafu kila mahali. Sasa kweli kabisa hizi mamlaka zilizotajwa kwenye Sheria, kutunga kanuni za kudhibiti usafi kwenye mazingira yetu ni wakati muafaka. Unafika kwenye hoteli chakula kinacholetwa mezani, ukiingia jikoni kinakopikwa unaweza baada ya kula ukakitapika tena chote na wewe uchafu mwininge kwenye hoteli hiyo. Hali ni mbaya mno; afya za Watanzania zipo katika wakati mgumu na bila kuangalia suala la Sheria hii, hali zetu zitakuwa mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tabia ya wenye mabasi kuchimba dawa barabarani imekithiri utafikiri watu kweli wanachimba dawa huko barabarani na watu wamejiwekea vituo vya kuchimba dawa. Utakuta mabasi yanasis mama watu wanakwenda kuchimba dawa, hebu niambie wanachimba dawa gani kama si kuongeza matatizo? Viwekwe vyoo maalum, viweze kutusaidia kuongeza hali ya usafi na afya za Watanzania katika nchi yetu. Mimi nashangaa, kwa mfano, pale Mikumi pamejengwa vyoo vizuri sana lakini mpaka leo havijaanza kutumika. Ukishapita tu pale Mikumi unakutana na post za kuchimba dawa, mabasi yanasis mama; hakuna maji ya kunawa mikono, jamani kwa kweli hali inatisha Sheria hii ichukue nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee na watoto wanatakiwa afya zao ziangaliwe. Tunasema kwamba, matibabu yao ni bure, Waheshimiwa Wabunge wameongea hapa asubuhi hilo bado ni tatizo. Kuna maeneo huko kwenye Majimbo yetu, tunazo Zahanati za Serikali, lakini kuna maeneo zipo Zahanati za *private*, hebu tuone ni namna gani tunaweza kuweka nguvu za kusaidia kuondoa tatizo ili wazee na watoto kweli waweze kutibiwa bure. Naibu Waziri amekiri hapa kwamba, Sera inasema hivyo, lakini usimamizi haupo. Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru kwa kuliona hilo. Sasa kama usimamizi haupo ni nani yupo *responsible* kusimamia hilo? Hebu tukumbushane nani anayewajibika na hilo achukue nafasi yake ili wazee na watoto waweze kupata matibabu yao bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna *crisis* kubwa ya kuwa na uhaba wa watumishi wa afya na uhaba wa mabwana afya katika maeneo yetu ya Wilaya. Sasa mimi nadhani Sheria hii iendane na suala zima la kuongeza ikama ya watumishi hao kwenye maeneo yetu ili kweli Sheria hii itakapoanza, iweze kutumika vizuri.

Nimalizie na suala zima la Ukaguzi wa Dawa na Chakula; hivi juzi juzi kumetokea crisis kubwa kule China, ambapo maziwa yamegundulika kuwa na kemikali ambayo imeleta maafa makubwa sana. Hata katika nchi yetu, maziwa ya Nido I nayo yalionekana yana tatizo hilo, lakini baadae ikaonekana hakuna. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo Sheria hii inatakiwa kuyazingatia.

Usalama wa chakula cha Watanzania ukoje? Tuna *Super Markets* nyingi, zina vyakula ambavyo vime-*overstay* kule; nani anakagua na kutuambia vyakula vile kweli ni *reliable* kwa ajili ya afya za Watanzania? Kwa hiyo, Sheria hii ichukue nafasi.

Dawa za mifugo *experiencing dates* zimeendelea kuandikwa kwa kiingereza, sijui kama wafugaji wetu wote wanaelewa. Hata dawa za binadamu nazo ni hivyo hivyo. Tusiishie kutunga Sheria, asubuhi tunesema usimamiaji, kunatakiwa kuongeza nguvu ya ziada kuokoa afya za Watanzania na kuhakikisha kwamba, Watanzania wote wanapata afya iliyo bora na kuokoa afya yao ni kujikita kwenye kinga zaidi kuliko kwenye tiba. Tukitoa kinga ya kutosha na Sheria hii itatusaidie zaidi kutoa kinga ili ile tiba isitugharimu zaidi kuokoa afya na maisha ya Watanzania kama nilivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niichukue nafasi hii, niipongeze sana Wizara, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kazi nzuri wanazofanya. Vilevile naipongeza Kamati iliyochambua Muswada huu.

Nasema kwamba, umefika wakati Watanzania tukubaliane; afya za Watanzania zipo hatarini na hazina mwenyewe, kama hatutatumia Sheria hii vizuri tunawenza tukasababisha maafa na magonjwa makubwa yatakayoweza kulisumbua sana taifa hili na kuligharimu fedha nyingi sana kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii.  
(*Makofii*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya pili, nami niweze kuchangia Muswada huu uliombele yetu. Kwanza, kabla sijaanza kuchangia Muswada, naomba kwa niaba ya wapigakura wa Jimbo la Kondo Kusini, niweze kutoa rambirambi na pole kwa ndugu, jamaa na marafiki na wapiga kula wa Jimbo la Mbeya Vijiji, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pame peponi, *amina*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya, kwa kuleta Muswada huu muhimu sana leo hii. Napenda niungane na Kamati iliyoupitia Muswada huu na kutoa mapendekezo na marekebisho

mbalimbali ambayo yamefanyika. Nitachangia katika maeneo machache tu, lakini nakiri kwamba, Mheshimiwa Waziri katika maelezo yake alisema kwamba, kuna jedwali la marekebisho sijalionia. Kwa hiyo, sasa napenda kusema ...

**NAIBU SPIKA:** Linagawiwa na sidhani kama wewe unaweza kuliona hilo, lakini wengine kwa sababu mtaishia jioni mtakuwa na muda tena wa kulipitia.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado sijapata jedwali hilo, mimi nitachangia kama Muswada ulivyokuja. Kwa hiyo, nitaanza kuchangia kwenye maeneo mbalimbali ya Muswada huu.

Nianze na aya ya 18 ya Muswada huu, kwenye ukurasa wa 21, ambayo inazungumzia kuhusu hatua ambazo zitachukuliwa kwa watu watakaoumwa na wanyama wenye maambukizi au wenye vichaa. Napenda niseme tu kwamba, kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada huu, hatua zinazochukuliwa ni nzuri lakini tatizo ni katika utekelezaji. Kilio cha wananchi mpaka sasa, kuhusu hatua zinazochukuliwa ni upatikanaji wa dawa zenyewe kwamba zinahifadhiwa katika hospitali za mikoa, ambako ni mbali sana na wananchi. Sasa nafikiri katika Kanuni ambazo zitatengenezwa, basi Waziri azingatie hili kwa sababu ni gharama kubwa na ni mbali kufuata dawa hizi za chanjo katika Hospitali za Mkoa, ikiwezekana basi dawa hizo zingesogezwa karibu na wananchi katika ngazi za Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka nichangie ni aya ya 22, ukurasa wa 22, ambayo inawasamehe makundi fulani fulani ya wananchi, kuhusu chanjo ambazo zimetajwa katika Jedwali la Nne na hapa waliotajwa kusamehewa kutokana na chanjo hizi ni wajawazito na watoto ambao ni chini ya umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni shahidi kwamba, kumekuwa na utaratibu huu wa kusamehe makundi mbalimbali ya wananchi wetu kulipa ada fulani fulani au gharama fulani katika matibabu, lakini tatizo linalojitokeza ni utekelezaji. Napongeza hapa kwamba, katika aya hii imezingatia tatizo hili la kusamehe makundi hayo mawili ya akinamama wajawazito na watoto chini ya miaka 18, lakini utekelezaji wake huwa mara nyingi ni mgumu sana. Ombi ambalo nalitoa kwa niaba ya wananchi ni kwamba, Serikali iweke utaratibu madhubuti ambao utahakikisha kweli ambao wametajwa katika aya hiyo wamesamehewa gharama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo napenda nilichangie ni ukurasa wa 40 aya ya 66, sehemu ndogo ya tatu. Sehemu hiyo ndogo ya 3.6. inazungumzia juu ya utaratibu wa kujenga nyumba na inaainisha kwamba, huwezi kujenga nyumba mpaka uwe na ramani ambayo itapitishwa na mtaalam. Katika aya ya tatu, inasema kwamba, kwa upande wa vijijini hakuna haja ya kuwa na utaratibu huo.

Wasiwasi wangu ni kwamba, utaratibu huu naona unalenga ujenzi wa nyumba katika maeneo ya miji, lakini hatuna utaratibu wowote wa kuzingatia au kisimamia ujenzi wa nyumba katika maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, wananchi wanaendelea kujenga nyumba ovyo katika maeneo ya vijijini. Tukumbuke kwamba, hata wananchi wa vijijini

wanastahili kukaa katika nyumba bora. Kwa hiyo, nafikiri kuna upungufu katika aya hiyo na sehemu hiyo ya tatu ya aya ya 66. Lazima tuwe na muongozo wa aina fulani wa kuweza kutoa hata kwa nyumba zinazojengwa vijiji ili tuwe na nyumba bora na tukumbuke kwamba, hivi vijiji tunavyoendelea kujenga baadae vitakuja kuwa miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu ya kuwa na utaratibu mzuri wa kuweza kuweka muongozo wa kusimamia ujenzi wa nyumba bora. Nafikiri Serikali iangalie, pamoja na utaratibu mzuri na Sheria mbalimbali ambazo zinazingatiwa katika ujenzi wa nyumba bora mijini, basi tutupie macho pia katika maeneo ya vijiji ambako nako wananchi wanastahili kuishi katika nyumba bora. Suala hili la ujenzi wa nyumba bora katika maeneo ya vijiji naomba lizingatiwe. Napenda niongezee hapo kwamba, hivi sasa katika maeneo ambayo yanapitiwa na nishati ya umeme ni kwamba, nyumba nyingi sana zinajengwa lakini zinajengwa holela hatuna utaratibu. Sasa naomba utaratibu huu ambao unazingatiwa mijini, pia uelekezwe katika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ambalo napenda nichangie lipo katika ukurasa wa 50 aya ya 86, sehemu ndogo za (f) na (g). Hapa napenda niipongeze sana Serikali kwa kuzingatia kilio cha muda mrefu cha watu wenyewe ulemavu. Aya ya 86(f) na (g) zimezingatia sana mahitaji ya watu wenyewe ulemavu katika maeneo ya maliwato na nyumba kwa ujumla. Nimesema hivi kwa sababu Kamati ya Bunge ya Miundombinu, ilitembelewa na ujumbe wa watu wenyewe ulemavu wakatuomba kwamba, pindi itakapotoka Sheria ya namna hii kuhusu ujenzi wa nyumba, tuombe Serikali izingatie mahitaji yao. Sasa napenda niishukuru sana Serikali kwamba, imezingatia mahitaji ya watu wenyewe ulemavu katika majengo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tano linahusu aya ya 126, sehemu ndogo ya sita ukurasa wa 66. Aya hii inazungumzia juu ya maeneo ya kuzikia vijiji. Aya inatambua kuwepo kwa maeneo ya kuzikia katika maeneo ya vijiji, lakini tatizo ninalotaka kuliibua hapa ni kwamba, kuna kipengele kwenye aya ya 126(6) inamatka kwamba, mazishi hayatafanyika bila kibali cha Mamlaka. Hofu yangu hapa ni katika maeneo ya vijiji. Mamlaka kwa mujibu wa tafsiri ya Muswada huu kwa kiingereza ni *authority* na katika maelezo ni *District Authority* au *Urban Authority*. Sasa kwa upande wa mijini, hakuna tatizo kwa sababu vibali vya kuzika vina utaratibu.

Kwa upande wa vijiji, kwa Muswada huu *Authority* maana yake *District Authority*. Sasa nahofia, sielewi kwa nini Muswada huu unapendekeza kwamba mazishi hayatafanyika mpaka kibali kitolewe na Mamlaka ya Wilaya? Tuzingatie maeneo mapana mfano Wilaya kubwa kama Kondoa, *District Authority* mimi sielewi maana yake ni nini hasa hapa inapozungumzia kwamba lazima uwe na kibali cha *District Authority*. Naomba nipate tafsiri ya neno *District Authority* ni nini? Inawezekana ikawa na tafsiri ile ile kwamba Mamlaka inaweza ikatoka kwenye ngazi ya Wilaya halafu tukakwamisha mambo ya mazishi katika maeneo mbalimbali ya Wilaya zetu. Naomba ufanuzi wa neno *District Authority* katika aya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la sita ambalo nataka kulichangia ni aya ya 174(1); napenda kusema kwa kifupi tu kwamba, naipongeza Serikali kwa kuleta aya hii ambayo imezingatia mahitaji ya kuwa na vyoo katika barabara kuu. Aya hii imebainisha wazi kwamba, Serikali itashirikiana na wasafirishaji kuhakikisha kwamba, kuna maeneo yatakayojengwa kwa ajili ya wasafiri kujisaidia katika barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia Muswada wenyewe, naomba nichangie maeneo mawili ya jumla. Katika Muswada huu, nilikuwa nategemea sana kuona matumizi ya chandarua yangeweza kusitisizwa lakini sijaona mahali popote ambapo vyandarua vinasitisizwa kama ni mbinu mojawapo ya kuweza kupunguza maradhi.

Katika magonjwa ambayo yanaambukiza ni pamoja na malaria, nilitegemea kwamba, Watanzania wote sasa wahimizwe kutumia vyandarua ama walazimishwe kutumia vyandarua, lakini sijaona mahali popote panazungumzia matumizi ya vyandarua, nafikiri kuna upungufu. Sasa kama kuna upungufu, izingatiwe katika kanuni.

Eneo la mwisho ambalo napenda kulizungumzia ni kwamba, utekelezaji wa Sheria hii kama itapita na bila shaka itapita, inategemea kuwepo na watumishi. Hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa afya katika Wilaya zetu. Kwa hiyo, kama Serikali inataka Sheria hii iweze kusimamia vizuri, wahakikishe kwamba tatizo la upungu wa watumishi wa afya limetoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naomba niishie hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Viongozi wote wa Wizara kwa ujumla, kwa kuleta Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha kuumaliza mwaka 2008 salama na sasa tupo mwaka huu wa 2009. Ninawashukuru sana Wananchi wa Jimbo la Mpwapwa, kwa kushirikiana nami na ninawahakikishia kwamba, tutaendelea kushirikiana katika kuleta maendeleo katika Jimbo letu na Wilaya yetu ya Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana. Leo asubuhi nilikuwa nasikiliza kipindi cha TBC Taifa, wananchi walikuwa wanatoa maoni kuhusu Muswada huu redioni hasa kuhusu suala zima la usafi wa mazingira. Wananchi wengi waliota maoni, walikuwa wanalenga hasa Mabwana Afya kwamba, Mabwana Afya kazi yao kubwa ni kukagua mabucha tu. Ninadhani kukagua mabucha ni jukumu mojawapo la Bwana Afya, kwa sababu tunataka mabucha yote yawe safi ili nyama ambayo tunanunua isiweze kupata maambukizi au vijidudu vyovyyote vya kuleta magonjwa ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Afya ya Kinga. Mara nyingi ninaposimama kuzungumzia suala hili ni kwamba, katika Wizara ya Afya tuna Idara ya Afya ya Kinga na Tiba (*Preventive Services and Curetive Services*). Tukiimarisha Idara ya Afya ya Kinga, mimi nadhani hata haya magonjwa mengi yanayotusumbua hasa ya kuambukizwa, yatapungua sana kwa sababu kuna mengine ya kujitakia na mengine ya bahati mbaya. Kwa mfano, suala zima la uchimbaji wa vyoo kwenye maeneo yetu; hivi kuchimba choo mpaka Bwana Afya aje akuhimize?

Lazima tuwe na tabia ya usafi, tuisubiri mpaka Bwana Afya aje atuhimize kwamba sasa chimbeni vyoo, sasa fagieni nyumba zenu hapana, tuwe na tabia ya usafi ili kupambana na haya magonjwa ya kuambukiza. Yapo magonjwa ambayo yanaweza kuzuulika. Kwa mfano, ugonjwa wa Kipindupindu, mimi siamini kama Watanzania hatuwezi kuuzuia; tunaweza kabisa kama tutazingatia kanuni za usafi au masharti ya usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika miji yetu mingi sana, hali ya takataka na umwagaji wa maji machafu kwa kweli inatisha. Ninazishauri Halmashauri za Wilaya, zitunge sheria ya kudhibiti suala zima la kukusanya takataka, kwa sababu chanzo kikubwa cha magonjwa ya kuambukiza ni uchafu; zaidi ya asilimia 75 ya magonjwa ya binadamu yanatababishwa na uchafu. Kama tutazingatia masharti au tutazingatia kanuni za afya za usafi, tunaweza kuzuia haya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Bwana Afya ni kufanya ukaguzi wa nyumba hadi nyumba (*routine inspection house to house*). Jukumu la Bwana Afya ni kukagua majengo ya vyakula (*food premises*) ili kuhakikisha kwamba, wale wanaofanya kazi kwenye hoteli (*food handlers*), wana afya nzuri, wasiwe *carriers* ambao wanawenza kusababisha kuambukiza magonjwa kwa walaji katika maeno hayo. Kwa hiyo, nawapongeza sana Mabwana Afya na mimi mwenyewe *profession* yangu ni Bwana Afya.

Leo asubuhi alipokuwa anasema kazi yetu ni kukagua mabucha; lakini ni jukumu la Bwana Afya kukagua mabucha, kukagua hoteli na kukagua maduka mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maoni yangu ni kwamba, sasa hivi Mabwana Afya ni wachache, tuna Maafisa kila Wilaya; Wilaya moja ina Maafisa Afya wawili/watatu. Lengo la Serikali ilikuwa ni kupeleka Bwana Afya kila Kata. Baadae Serikali iliamua kufuta vyuo vyote ambavyo vilikuwa vinafundisha Mabwana Afya Wasaidizi (*Health Asistants*), kwa lengo kwamba, wanataka kuwaendeleza wale waliopo, kwa hiyo, wakawa wamefuta vyuo hivyo. Nakumbuka Chuo cha Afya Mpwapwa, walikuwa wana-*train Health Officers*, Chuo cha Afya Ngudu, Chuo cha Afya cha Kagemu, Chuo cha Afya cha Mpanda, pamoja na Iringa, lakini baadae Serikali ilisema hapana, tutakuwa na *Health Officers* ambao watashughulikia afya ya mazingira katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, vile vyuo ambavyo vilikuwa vina-*train Health Asistants*, ningombia ivifufue tuwe na Maafisa Afya Wasaidizi katika Vijiji. Hawa watasadilia hata elimu ya afya na elimu ya afya ni muhimu

sana katika vijiji. Muhimbili kuna Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma (*Health Education Unit*) na mimi mara nyingi huwa nakizungumzia sana. Zamani walikuwa wana-train *Health Educators* ambao walikuwa wanazunguka Mikoa yote kwa ajili ya elimu ya afya, lakini tunasubiri mpaka kuwe na mlipuko wa kipindupindu ndio tunaanza kuhangaika sasa kwenda kutoa elimu ya afya. Elimu ya Afya iwe ni *routine*, kila wakati itolewe wananchi waelewe ugonjwa unaambukizwaje, maana lazima ujue ugonjwa ni nini; upate *definition* ya ugonjwa, halafu ujue *the mode of transmission, causative organisms* na lazima ujue *control measures*. Sasa bila kuwaelimisha wananchi wetu, hawawezi kuelewa. Kwa mfano, mtu unamfundisha kipindupindu, lazima aelewe maana siyo kila kuharisha ni kipindupindu, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nashauri kwamba, idadi ya Mabwana Afya katika vyuo vyetu iongezwe ili waweze kupelekwa mpaka vijijini waendelee kutoa elimu ya afya juu ya suala zima la kuchemsha maji ya kunywa. Ukichemsha maji ya kunywa, utakuwa umeshaua vijidudu vinavyoleta *Typhoid*, vinavyoleta kipindupindu, magonjwa ya kuhara na kuhara damu na utakuwa umeshazuia suala hilo. Mabwana Afya vile vile watasaidia sana suala zima la utupaji wa takataka katika miji yetu, katika kaya zetu, maana sasa hivi utaratibu unaotumika, ukienda katika miji yetu mingi, ule usafi hasa hauzingatiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri, mwaka jana tuliitembelea nchi ya Namibia na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tulipokuwa pale Windhoek, ule mji ni msafi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri baadhi ya Mameya na Wakurugenzi, hebu wakajifunze kuona wenzetu wanatumia mbinu gani hadi miji yao inakuwa safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, nazungumzia suala zima la chanjo kwa ajili ya watoto wadogo na akina mama wajawazito. Vijiji vingi havina zahanati. Ukishamchanja mtoto ni kinga kubwa sana, hawezi kuugua kifua kikuu, kifaduro, wala polio. Kwa hiyo, nashauri vijiji ambavyo havina zahanati, basi naomba muimarishe au mmboreshe huduma za afya hii *outreach* (huduma ya mikoba).

Tupeleke huduma sehemu zile ambazo hazina zahanati ili watoto wadogo na akina mama wajawazito waweze kuchanjwa, kwani wanapata tabu kusafiri kwenda kufuata huduma za afya katika maeneo mengine. Kwa kuwa mpango wa Serikali ni kujenga zahanati kila kijiji na kujenga kituo cha afya kila kata, mimi nadhani hii itasaidia sana. Zahanati si jengo tu ni dawa pamoja na wataalam. Kwa hiyo, Serikali iweke mikakati kuhakikiha kwamba, wananchi watakapokuwa wamejenga hizo zahanati na vituo vya afya, wataalam tunakuwa na waganga na waugazi wa kutosha, ili waweze kupelekwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la ukaguzi wa vyakula. Zamani kulikuwa na utaratibu, haya maduka ya vyakula na vyakula vingi ambavyo vinaagizwa toka nje, kuna vingine *vime-expire* lakini bado vinauzwa, sasa vile ni hatari sana kwa afya za binadamu. Kwa hiyo, ninaomba utaratibu

wa kukagua vyakula hivyo vya makopo uendelee ili wananchi wasiuziwe vyakula ambavyo vimepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dawa ambazo zime-expire hasa maduka ya dawa katika miji yetu, katika vijiji vyetu, yako maduka mengi sana ya dawa baridi; piteni muweze kukagua mara kwa mara. Dawa zikaguliwe kuhakikisha kwamba zinazouzwa kweli hazijapitwa na wakati, kwa sababu dawa yoyote ambayo imepitwa na wakati, ukiitumia ni sumu kwa mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii. Nawapongeza wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Najua wanafanya kazi katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, Idara hii ya Kinga ni muhimu sana. Mabwana Afya lazima wapewe vitendea kazi, hatuwezi kuwalaamu Mabwana Afya kuwa hamtekelezi majukumu yenu, wakati hawana vitendea kazi. Wapate vyombo vya usafiri ili waweze kwenda vijijini, kwa ajili ya kutoa elimu ya afya inapotokea milipuko.

Ningeshauri kabla ya wagonjwa kutibiwa, kuwe na utaratibu kama ule wa zamani wa kutoa elimu ya afya ili wagonjwa waelewe kama wana kipindupindu, wana ugonjwa wa homa ya matumbo au wanaharisha damu; basi wajue chanzo cha kuharisha damu ni nini na chanzo cha *typhoid* ni nini ili wakirudi majumbani waweze kuzingatia yale masharti ya afya na kupambana na suala zima hili la magonjwa ya kuambikiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Bwana Afya Mstaifu. Sasa nitamwita Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ania Chaurembo ajiandae na kama nilivyosema, Mheshimiwa Pindi Chana pia ajiandae. Naomba sasa tufunge orodha, msiniletee tena barua. (*Kicheko*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa na mimi napenda kutoa pole kwa wananchi, kwa msiba mkubwa uliotupata wa Mbunge mwenzetu Nyaulawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ponezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu wa UWT-Taifa. Mungu ambariki sana na amuongoze. Pia nitumie nafasi hii mimi binafsi kuwashukuru sana Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa UWT-Taifa, kwa kunichagua kwa kura nyingi sana kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT, pia kuwawakilisha wazazi. Mungu awabariki kwa imani hiyo waliyonipa na ninaahidi kuwatumikia ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa Muswada huu. Mimi ninasema Muswada huu ni dalili mojawapo ya kutoka tulikokuwa, kwenda kwenye maboresho zaidi. Hivyo, ninapenda kuzungumzia masuala machache kidogo kutokana na muda na mengi wenzangu wameshayazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuboresha huduma hii ya afya katika Idara hii ya Kinga, ninataka tu kusema kwamba, Wizara hii inalo jukumu kubwa sana la kuhakikisha inashirikiana na Wizara nyingine kwa sababu imeainisha maeneo mengi sana hapa na tukizingatia kwamba, huduma ya afya imeenda mpaka vijiji. Nikisema Wizara nyingine, nakuwa na maana hata ya Miundombinu, kwa sababu tunapozungumza kuongeza vituo vya afya, basi vituo vile haviwezi kufikika kama miundombinu itakuwa haijaboreshwa kwa maana ya barabara. Nikichukulia tu kwa mfano wa Hospitali ya Wilaya ya Manyoni, mgonjwa akiwa amezidiwa pale hasa mama mjamzito, anatakiwa akimbizwe katika Hospitali ya Mkoa wa Singida, ataanza kukutana na barabara ambayo itamchelewesha kufika katika hospitalini kupata huduma. Kwa hiyo, lazima Wizara hizi ziweze kutegemeana.

Ninazungumza hivyo kutokana na suala la usalama wa chakula au dawa. Wizara ya Afya inatakiwa pia ihusiane na Wizara zinazolinda mipaka yetu, kwa sababu kuna dawa au vyakula vinavyoingizwa ambavyo vimeisha muda wake au si salama kwa Wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nikizungumzia suala la magonjwa ya kuambukizwa, tunajua wazi kabisa malaria imekuwa ni ugonjwa sugu sana hapa Tanzania na tumeshindwa ni namna gani ya kuweza kuudhibiti ugonjwa huu. Japo unapungua, lakini si kwa kasi ambayo tumeitegemea ukizingatia ni lini tulipata uhuru wetu hapa Tanzania. Bado kuna tatizo pia la kuhama hama kwa dawa. Watu wengi sana wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na kutokujua ni dawa gani hasa inayotibu malaria. Tumetoka kwenye *chroloquine*, sasa hivi hata sijui tuko kwenye dawa gani, maana dawa zipo nyingi na watu wengi wanaathirika na hizi dawa. Kwa hiyo, labda sheria hii ambayo imeingia itatusaidia kuweza kudhibiti ugonjwa wa malaria ili usiwapate wananchi walio wengi, hasa wanawake wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika magonjwa haya haya ya kuambukiza, katika hospitali zetu utakuta kwenye wodi zetu hasa akina mama wanapokwenda kujifungulia ni hatari sana kwa sababu vitanda havitoshi; unakuta akina mama wanalala wawili wawili. Sasa wewe umekwenda kujifungua pale, lakini unaondoka na ugonjwa labda wa ngozi au mwingine wowote ule ambao ni hatari. Kwa hiyo, tunaomba sheria hii iangalie pia kwenye eneo hilo ili watu wasiweze kuambukizana yale magonjwa ambayo hayakutarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia magonjwa haya haya ya kuambukiza kwa mfano, katika *salon* zetu za wanawake na wanaume, kuna magonjwa ya kuambukiza na sielewi kama kuna uangalizi wa kutosha katika *salon* zetu.

**NAIBU SPIKA:** Unamaanisha *salon* za nini?

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Za kutengeneza nywele za wanawake, pamoja na wanaume. Kuna shughuli za kutengeneza kucha na kuosha miguu; ni vifaa vile vile vinatumika. Sasa hivi vifaa vinavyotumika wanaosha kwa *spirit*, hakuna uhakika pale kwamba hakutakuwa na maambukizi. Kwa hiyo, ninaomba pia eneo hilo litupiwe macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi katika masuala ya usafi wa mazingira; pamoja na kwamba Mabwana Afya wapo wachache kama inavyosemwa, lakini sielewi wa kuulizwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, sheria hii iangalie eneo hilo, kwa sababu ukifika kwenye miji yetu hasa miji mikubwa mikubwa, utakuta kuna mifereji inayotoa maji machafu, hata viongozi unakuta tunapita pale, lakini hujui ni nani wa kuulizwa kuhusu ule mfereji unaotoa maji machafu. Watoto wanacheza pale, viongozi kuanzia Serikali za Mitaa wanauona, labda mpaka madhara yatokee ndio uanze kufanyiwa ukarabati.

Kwa hiyo, ninaomba sana sehemu hizo hii sheria iweze kuziangalia. Pamoja na kwenye hoteli kama walivyokwisha kuzungumza; unafika kwenye hoteli, vyakula vinakuwa vimeshakaa muda mrefu. Saa nyingine unaletewa chakula labda samaki, unamwona kabisa samaki huyu ameharibika unamrudisha kwamba samaki ameingia sumu, ameoza au amekuwaje; lakini bado hakuna ufuatiliaji kuangalia hoteli zetu zinatunza viyi vyakula vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa ambazo zimekwisha muda wake imikuwa ni tatizo sugu, ambalo pamoja na kwamba TFDA wamekuwa wakijitahidi sana kuwakamata hawa watu, lakini sifahamu ni sheria ipi inayotumika wanapowakamata. Dawa au chakula kikiharibika zinachomwa, lakini watu wale wale waliokamatwa na dawa ambazo zimeisha muda wake au chakula, unakuta wanaweza kubadilisha leseni na wakaendelea tena kufanya biashara! Kwa hiyo, nafikiri ndio maana nilitanguliza kusema, Wizara hii ishirikiane na Wizara nyingine ili kuweza kudhibiti hata hili wimbi la dawa kuharibika au chakula kuchomwa, lakini bado wale watu adhabu zao zinakuwa siyo kali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Kamati yetu ilitembelea Milembe, tukaenda na Isanga, hali ya pale ni nzuri, wasafi. lakini majengo yaliyopo pale hakika kwa sababu tunataka kumtendea haki kila mmoja wetu, hewa inayopatikana pale kweli inaweza ikawa sababu kubwa ya kupata maambukizo ya magonjwa. Ninataka nirudi kwa wafanyakazi wa eneo lile; Wafanyakazi wanaofanya kazi katika eneo lile, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, sifahamu ni sheria ipi inayowalinda. Hii ni kwa sababu wale ni wagonjwa wa akili, wakati mwengine unakuta mgonjwa anampiga kofi mhudumu wake au hata kumng'ata na kumsababishia kidonda. Sasa sifahamu hii sheria kama inamgusa huyu atakayepata maambukizo kutoka kwa mgonjwa kama yule ambaye amemng'ata?

Katika eneo lile la Kituo cha Isanga, vyumba wanavyolala wale wagonjwa ambao wako pale ni vidogo sana kiasi kwamba, eneo lote lile linahitaji ukarabati. Wamejitahidi kwa usafi, lakini kutokana na msongamano uliopo, hakika inabidi Serikali ipatupie macho ili kuweza kukarabati eneo lile na kulipanua zaidi ili waweze kuishi bila kuambukizana.

Sijui kama sheria inamgusa huyo mgonjwa wa akili, kwa sababu kuna sheria ambayo kwa wale wagonjwa ambao wameua wametibiwa na wamepona, wanatakiwa wakae Gerezani kwa miaka mitatu ndipo waweze kuruhusiwa. Mgonjwa yule anakuwa ameshapona, lakini bado yuko pale gerezani akisubiri Bodi ikae miaka mitatu ipite, lakini unakuta wanakaa mpaka miaka minne/mitano na kuendelea. Sheria hii haioni kwamba, kwa ugonjwa wa kukaa muda mrefu bila kujuu hatima yao inawasababishia kuathirika zaidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema, hivi vituo vya afya tunavyokwenda kuvijenga sasa katika vijiji vyetu; vifo vingi vya akina mama vimekuwa vikitokea kwa sababu vituo vyetu bado havina wauguzi, hata vingine ambavyo vimeshajengwa.

Je, hivi tunavyotarajia kuvijenga, wauguzi watapatikana wapi; kwa nini basi tusichukue vijana wetu ambao wanamaliza kidato cha nne katika shule zetu za sekondari za kata nchi nzima, ambao hawafanikiwi kuendelea na kidato cha tano tukawafundisha ili warudi kuhudumia vituo vyetu vya afya kuweza kupunguza vifo hivi vya akina mama na watoto?

Mheshimiwa Naibu Spika, tiba tumesema kwamba watoto wanatibiwa, sasa hapo nataka kujuu ni kumwona daktari tu ndio bure lakini kununua dawa na vipimo wanalipa? Unakwenda kumwona daktari anakuandikia dawa za mtoto, lakini inabidi zile dawa ukazinunue kwenye *Pharmacy*. Sasa hiyo bure iko wapi kwa sababu vituo vyetu vingi vya afya vinakuwa havina dawa na hospitali hakuna dawa?

Unaposema kwamba, huyu mtoto au mama mjamzito au mzee anatibiwa bure, anatibiwa tu kumwona daktari lakini vipimo na dawa unanunua mwenyewe? Hilo ninaomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, ninaomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Sheria ya Afya ya Jamii ya 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imekuja wakati muafaka, wakati ambao Watanzania wengi wamekuwa wakiathirika kwa matatizo mbalimbali katika afya zao. Kwanza kabisa, kabla sijaanza kuzungumza, ningependa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Kamati zao walioandaa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitunga sheria mbalimbali hapa nchini, lakini utekelezaji wake umekuwa duni sana. Kwa hiyo, natia msisitizo kabla sijaanza kuchangia kwamba, sasa imefika wakati lazima hizi sheria zinazotungwa na Bunge lako hili Tukufu kufika kwa wananchi na kuangalia maslahi ya wananchi zitekelezwe badala ya kuzitunga na kubaki katika vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia suala zima la mazingira. Suala hili ni muhimu sana katika maeneo yetu, linaunganisha mambo yote ambayo wenzangu wameshatangulia kuyazungumza. Ukienda kifungu cha 74, ukurasa wa 45 kuna suala zima la majitaka, ambayo ni vinyesi na vitu mbalimbali vyta uchafu mzito, ambavyo vinachukuliwa na magari ya watu binafsi au ya Halmashauri na badala yake magari yale yanakwenda kutupa taka hizi nzito katikati wanakoishi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili nimekuwa nalipigia kelele siku nyingi, lakini napenda kulitilia msisitizo; Bwawa la Spenco lililopo Buguruni, jamani hili ni ombi, naomba bwawa lile lihamishwe. Bwawa lile na mabwawa mengine yapo katikati ya wananchi; yanaleta harufu mbaya, vidudu vinatembea na mara nyingi kipindupindu kinapotokea, utasikia inawekwa kambi ya kipindupindu katika Zahanati ya Buguruni na Vingunguti, kwa sababu hali ni mbaya sana. Nataka Waziri baadae katika majumuisho, anieleze kama alishalitembelea lile bwawa na kama hajalitembelea naomba tulitembelee mimi na yeze. Vilevile naomba hili bwawa liondolewe lipelekwe sehemu nyingine na mabwawa yote ambayo yapo katikati ya wananchi, maji ambayo yanamwaga kinyesi yaondolewe, kwani ni hatari kubwa sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa napenda kulizungumzia ni kuhusu masoko na vyakula ambavyo vinauzwa katika masoko yetu. Tunatunga sheria, kweli ni muhimu sana zifuatwe lakini bado tukubali katika Bunge hili, kabla hizi sheria hatujawapelekea wananchi, masuala yanayohusu Serikali kuyatekeleza, masuala yanayohusu Halmashauri kuyatekeleza kwanza kwa sababu mfano hai pale Jiji la Dar es Salaaam, ukiangalia masoko, baadhi yake ni mabovu sana; aidha yawe chini ya Halmashauri au chini ya sekta yoyote masoko ni machafu.

Masoko hayana hata mabati juu yanavuja, masoko hayana sehemu ya watu kufanyia biashara zao, mtu anatoka Mkuranga, anatoka Kisarawe na mihogo yake na visamvu vyake anakuja sokoni, anatupa pale mvua ikishanyesha, vyakula vinakuwa katika majimaji ya masoko na vyakula matunda yanaoza.

Tumeshuhudia sasa hivi maembe yaliyooza yanaitwa maembe ya juisi; watu wanununa kwa bei rahisi kidogo. Tumeshuhudia sasa hivi kwa mfano, pale Buguruni sokoni utawakuta akina mama wanachukua utumbo wa kuku na miguu, imekuwa ndio chakula.

Watu waelimishwe, mbona zamani wazee wetu walikuwa hawafanyi hivyo; yote hii ni kwa sababu watu hawana elimu ya kutosha hawaelewi; na wale wanafanya kazi ya utumbo kwa sababu wanataka pesa, uchungu wa maisha wanaamua kuwauzia wenzao, je, afya ya Mtanzania iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo ya msingi; sheria hizi mimi nazikubali kwa asilimia mia moja, lakini utekelezaji wake haupo kabisa. Tutengeneze kwanza masoko, wale wote wanaohusika, Madaktari wawepo wakati bidhaa zinaposhushwa. Zile ambazo zipo pale kwa muda mrefu, wawe wanaziangalia.

Wenzangu hapa wamesema kwamba, Madaktari wanaoangalia mambo ya vyakula ni wachache; kweli ni wachache utaratibu ufanyike, naamini tuna vijana chungu nzima wamesomea fani ya Udaktari ambao hawajapata ajira.

**NAIBU SPIKA:** Hapana Mheshimiwa Mbunge, unamaanisha Madaktari au Mabwana Afya?

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani ni Mabwana Afya. Wapo ambao bado hawajapata ajira, tutangaze nafasi za kazi kwa Mabwana Afya katika Halmashauri mbalimbali ili waajiriwe wasaidie kazi hii, kuhakikisha afya za Jamii zinapatikana na wananchi wetu wanakuwa na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza ni suala zima la machinjio; nawapongeza hapa Dodoma kwa machinjio mazuri sana na ya mfano kabisa, basi Tanzania nzima iwe kama Dodoma. Ukienda leo Vingunguti, unakuta damu zimekaa zimeganda zimegeuka rangi ya kijani kabisa. Unakuta mbuzi wanachinjwa wanatupwa tu juu. Sasa tunaposema tunazitunga hizi Sheria, kwanza, tuhakikishe vile vitu tunavyovitungia sheria tumeshaviweka katika mazingira yanayostahili kabla sheria hii haijamwadhibu mwananchi. Tutengeneze mazingira ya wananchi ambayo watawekewa hizi sheria yawe safi. Sheria ichukue mkondo wake kama tunavyoamua kuzipitisha katika Bunge hili, lakini kwenda kumwambia mchinji Mbuzi kwamba, amevunja sheria kifungu fulani wakati pale anapochinjia suala hilo siyo lake ye ye ni Halmashauri na ndiyo wanaotakiwa watengeneze eneo lile, bila hivyo sheria zetu hizi tunazozitunga nzuri zitakuwa bado hazijafanya kazi inavyopasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nilikuwa katika Kamati ya *LAAC*, tulitembelea mikoa mbalimbali; Mkoa wa Arusha, Manyara, katika baadhi ya zahanati tumekuta tunahitaji kuboresha huduma ya sehemu wanazojifungulia akina mama, kwa kweli hazipo katika kiwango kinachotakiwa na vilevile vifaa ambavyo vinatumika kuzalisha akina mama havistahili kutumika na ndiyo maana tunapoteza akinamama wengi wakati wanapojifungua. Vitanda vya kujifungulia ni maalumu kwa ajili ya kujifungulia, sasa unakuta vingine vinafungwa mpaka mbao. Mama akienda na tumbo anakaa huku na kule, anaingia chini; ni lazima tuwapoteze na haya yote tuyaangalie, hili ni ombi rasmi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa ili kupunguza vifo vya watoto na akina mama, tutengeneze mazingira angalau ya kuzalia yafikie hadhi inayostahili. Watu wasizalie sehemu ambazo mtoto anakula uchafu na kupoteza maisha na mama vilevile anapoteza maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kulichangia, nimefurahi sana kuona Serikali zetu za Mitaa kwa sasa zimesaidia kwa kiwango kikubwa katika kusimamia masuala haya. Vuguvugu lote linatoka kwenye Serikali za Mitaa, Vitongoji na Vijiji, ninyi wenyewe hapa katika Bunge hili, mnashuhudia jinsi gani katika maeneo yetu tulipokuwa tuna mambo mbalimbali machafu; tuna watu ambao wanapewa mikataba kwa mfano ya kusafisha mifereji ya kusafisha barabara lakini hayatekelezwi. Adhabu iliyotolewa nakubaliana kabisa na Kambi ya Upinzani kwamba, adhabu ya laki moja ni ndogo sana kwa wale watendaji wetu, maana wanawafanyisha kazi wale wananchi bila ya kuwa na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anaingia kwenye mifereji hivi hivi bila kuwa na vifaa, ilishasemwa sitaki kurudia tena lakini msisitizo tu hii ni kero kubwa sana. Vyoo vinatiririka katika mifereji, wale watu wanaathirika sana. Juzi mtakuwa mmeshuhudia vile vile katika Kiwanda cha Samaki Dar es Salaam, imetokea katika televisheni wafanyakazi wanalamika kwamba, afya zao ni mbaya sana kutokana na harufu chafu inayotoka kiwandani. Jiji la Dar es Salaam ambalo Serikali yote iko hapo, basi hao mabwana afya hawapiti katika viwanda wakaangalia. Kwa hiyo, tunaomba katika maeneo yale yote ambayo yanalamikiwa kwenye televisheni sasa hivi, yafanyiwe kazi ili kuboresha afya zao. Tunahitaji nguvu kazi ya Watanzania

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Pindi Chana, nafikiri na Mheshimiwa Suzan Lyimo anaweza kupata nafasi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kutuvusha wote kuingia mwaka mpya wa 2009. Vile vile nawashukuru sana ndugu zangu Wanyalukolo wote wa Iringa, kwa Mungu kutuwezesha kufikia hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa kuuleta Muswada huu unaohusiana na Afya ya Jamii (*Public Health*). Taifa lolote likitaka liendelee inategemea rasilimali watu; tunaposema rasilimali watu maana yake ni watu wenye afya. Watu wanapokuwa na afya, wanaweza kufanya kazi, wanaweza kuwajibika na kufanya mambo mengi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mzuri, umeandaliwa vizuri, nianze kuchangia kwa kuishauri Serikali au Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na ukurasa ule wa tisa pale; katika tafsiri kuna kipengele cha tatu kifungu cha (3) kinaelezea mamlaka na mamlaka ambayo Muswada huu umeutambua ni mamlaka ya Wilaya na Mamlaka ya Mji inasema, *District Authority or Urban Authority*. Kwa jinsi nilivyouona Muswada huu na katika maeneo

ambapo Muswada huu unapaswa kutumika, tafsiri hiyo haitoshelezi; hivyo, ningeshauri kuongeza *Township Authority, City Authority* ili maeneo hayo pia yawe na mamlaka ya kutekeleza majukumu ambayo yapo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu mzuri umeelezea mambo mengi sana; umezingatia watoto wale mavu. Kwa upande wa watoto, kifungu cha 23 cha Muswada kimezungumzia suala la kinga kwa watoto kuwa ni kitu cha msingi sana na hata ifike wakati watoto wanapoingia darasa la kwanza, wahakikishiwe kwamba wamekwishapata kinga inayostahili na endapo watakuwa hawajapata hiyo kinga, basi inawezekana kabisa mzazi au mlezi atapaswa kwenda kumpa chanjo mtoto ili kuweza kupata nafasi ya kusoma.

Jambo hili ni jema sana na ni la maana sana, kwa hiyo, ningeomba nitumie nafasi hii kusema kwamba, wapo watoto wetu wengine hawakai na wazazi, wanakaa katika vituo vyta kulelea watoto yatima; kwa hiyo, katika maeneo hayo tungeomba kama ni *NGOs* au Mashirika yoyote yanayolea wale watoto, yaweze kuzingatia zile kinga stahili kwa ajili ya watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kusema yafuatayo; kuna wakati kulikuwa na utaratibu wa kuwapa kinga watoto mashulen. Watoto wale walikuwa wakipata kinga; wengine walikuwa wanazirai na wengine walipata matatizo. Mtakumbuka jambo hilo lilitokea, sasa tungeomba sana wataalamu wetu wazingatie maeneo mengine, tulipokuwa tunaulizana kwa nini watoto wanapata kinga mashulen na wanapata matatizo wadondoka, wakasema kwamba, yamkini walikuwa hawajapata chai na ile kinga ili ifanye kazi vizuri ilikuwa ni lazima mtu uwe na kitu tumboni. Kwa hiyo, vitu kama hivyo tusingependa viendelee kutokea kwa sababu vinaleta madhara mengi sana. Kwa hiyo ni muhimu sana wataalamu wetu wakazingatia ni vigezo vipi ambavyo vinapaswa kuwepo kabla ya watoto wetu kupata kinga ili viweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kuhusu afya ya jamii ni pamoja na usafi wa mazingira yetu. Mambo haya katika maeneo ya Miji mikubwa kama Dar es Salaam, yamekuwa yakifanyika na Halmashauri zetu ambapo wamekuwa wakibinafsisha shughuli hii ya kuzoa taka. Watu mbalimbali wanachukua shughuli hizi za uzoaji wa taka, lakini maeneo mengine katika mikoa mingine, Halmashauri hazijatenga hata maeneo maalum ambayo yanafahamika kwa wanajamii wapi pa kwenda kutupa taka au madampo na maeneo mengine hata yale magari hayafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kusema kwa mujibu wa Muswada huu, kuna maeneo ambapo tumesema kama jamii haitatekeleza wajibu wake, basi kulingana na hicho kifungu, jamii au mtu husika au shirika, litakuwa limetenda kosa. Hiyo ni sawa kabisa. Sasa kunapokuwa kuna kosa kwa upande wa jamii; ni muhimu sana sheria ikawa pande mbili. Serikali, Wizara au Mamlaka husika ni muhimu nayo ikaweza kutekeleza wajibu wake pale inapobidi, isije ikawa upande mwengine usipotekeliza tunawaambia kuna faini ya laki moja, kutakuwa na kifungo au kutakuwa na *penalty* ya aina hii. Endapo Wizara au Serikali haikusimama kwenye nafasi yake ambayo inapaswa, basi hakuna mtu wa kuwakumbusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana, wanasema popote kwenye *rights* ni lazima kuwe na *obligation*, kwa hiyo mambo haya yanakwenda pamoja; tunaposema wananchi wasitupe taka ovyo, wasizembee kufanya wajibu wao, basi lile jambo kama ni Serikali kuandaa maeneo ya kutupa taka ni vizuri yakaeleweka ili pande zote ziwe zinasimama kwenye nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo nitumie nafasi hii kushauri katika kifungu cha 174, tumekubaliana kwamba, itakuwa ni kosa mtu au mashirika yanayosafirisha watu, kujisaidia eneo ambalo hakuna choo. Lazima eneo hilo kuwepo na choo, lakini ni lazima tujiulize; tumeandaa vyoo hivi au tunategemea vile vyoo vyaa *petrol station* ambavyo viro barabarani?

Serikali kupitia Mamlaka za Miji, Mamlaka za Wilaya, inasema kuwa wananchi wenyewe mabasi msiende porini; ni sahihi kabisa, lakini vyoo hivyo viro wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali na zile Halmashauri ambazo barabara kuu zinapita katika maeneo yao kwa mfano Mikumi, Morogoro, Ruaha Mbuyuni, Mufindi, Njombe, watenge maeneo na si lazima wao wenyewe *wai-operate* wanawenza kubinafsisha; watu watapata ajira, watawekeza na kadhalika. Kwa hiyo, hata tunaposema tunatekeleza sheria hii, basi upande wa Serikali unakuwa umeshamiliza kufanya wajibu wake. Jambo hilo naomba lifanyike mara moja ili pande zote ziwe zimekamilika, kwa sababu sheria hii ikishasainiwa inaanza kutekelezwa, hasa upande huu usipokuwa umefanya wajibu wake, tutakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna baadhi ya vifungu vimeelezewa juu ya maneno *overcrowding* (kuzidisha watu). Ninaomba sana liingie kwenye *interpretation*, nini maana ya neno *overcrowding*. Imesemekana kwamba ni kosa, sasa wakati mwingine *overcrowding* inatokea kwenye mabasi na sasa hivi tumekuwa tukishuhudia mabasi mengi yanapata ajali na majeruhi wanakuwa wengi sana, wakati mwingine inatokana na hiyo *overcrowding*. Naongelea kifungu cha 63, ukurasa wa 39 wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusije kupishana katika tafsiri; unapomwambia mtu kwamba basi lako umezidisha, tuelewane kwamba kama ni basi maana yake ni *level seat* na ye yule atakayekuwa kwenye korido, hiyo itakuwa ni *overcrowding*; na kama ni kwenye nyumba nini maana ya neno *overcrowding* inapohusiana na nyumba?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa mashahidi, kuna watoto wamefariki Tabora wakati fulani walikuwa kwenye chumba fulani, ilikuwa ni michezo walikosa hewa, sasa ile ilikuwa ni *overcrowding* au ilikuwa ni nini?

Haya mambo ni muhimu sana sheria ikaeleza vizuri. Kwa hiyo, ningeomba neno *overcrowding* litafsiriwe ili liweze kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya maeneo wametumia neno *summary conviction*; *summary conviction* ni pale ambapo mtu ametenda kosa na moja kwa moja

bila kutafuta ushahidi, unasema tayari hilo ni kosa unapewa adhabu hapo hapo, ndio maana wanatumia neno *summary*. Una-summarise zile taratibu badala ya kusema lete shahidi wako, maana yake kuna maneno naomba ninukuu kwa kiingereza: “*The person is innocent until prove guilty.*” Katika *summary conviction* hakuna muda wa ku-*prove* kwamba, huyu mtu ni *guilty*; amefanya makosa na hapo hapo unampa adhabu.

Tunaomba maafisa wetu katika yale maeneo ambayo tumekubaliana kwamba kutakuwa na *summary conviction*, kwa mfano, mtu ameacha maji yanatunza mbu au amefanya kitu tofauti, lengo la *summary conviction* lisiwe ni chanzo cha mapato. Maana watu wengine unampa *penalty*, anapokusanya yale mapato vizuri ndio mtu unaonekana unachapa kazi vizuri. Lengo la sheria hii si kukusanya mapato bali ni afya bora. Kwa hiyo, ikiwezekana maafisa wetu katika mamlaka mbalimbali, wampe mtu saa 24 rekebisha jambo hili, nakupa siku mbili, nakuja kesho. Mimi ni Bwana Afya, umeharibu hapa hakikisha kesho saa sita limerekebishwa, ikishindikana basi unachukua hiyo hatua ya *summary conviction*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu yangu ni kwamba, wasije wakawa wanatumia vibaya, mtu anafika tayari umeshatenda kosa ni kweli kutokujua sheria si kinga kwamba hukujua; ni lazima ufahamu. Maeneo hayo, ningeomba sana wataalam wetu wayazingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia mambo mengi kwa maandishi nitayakabidhi.

Baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana na kuupongeza Muswada huu.

**MHE. SUZAN J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuzungumza asubuhi ya leo; pamoja na kwamba, nilikuwa nimefikiri nitachangia mchana lakini nashukuru kwamba nimepata muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na Muswada wenyewe; awali ya yote niseme kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati, kwa kiasi kikubwa tulichangia katika marekebisho. Pamoja na kuwa Mjumbe, bado nimeona kuna sehemu ambazo nadhani zinahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukianza na *section 9(1)*, ambayo inaelezea *noticeable diseases*. Ukiangalia ukurasa wa 98, magonjwa hayo ya kuambikizwa yapo manne nayo ni *Ebola*, *Rift Valley*, *Yellow Fever* na *Marburg Fever*. Kinachonishangaza ni kwamba, ukienda *section 21(1)*, ukurasa wa 22 inaeleza kwamba, mtu ye yote atakayeingia Tanzania Bara awe na *certificate* ya *yellow fever*. Sasa suala langu ni kwamba, kuna haya magonjwa mengine manne ambayo pia ni ya kuambukiza, lakini tunaambiwa kwamba atapata chanjo ya *yellow fever* tu; je, haya mengine ni namna gani? Naomba ufanuzi kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *section 18(1) na (2)*, inaelezea suala zima la *rabid animals*, lakini hii haijaonesha kama wale mbwa koko nao wanahusika, kwa sababu ukipita katika mitaa mingi, unakuta mbwa waliozagaa, pamoja na kwamba hatujui kama wana vichaa. Nilikuwa nataka kujuu kama mbwa wa namna hii pia nao wanahusika?

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna Mjumbe mmoja ameongelea sana suala la dawa kwa ajili ya watu wanaong'atwa na mbwa au wanyama wenye vijidudu hivyo. Dawa hizi ni kwamba, zinapatikana katika hospitali za mikoa, lakini vilevile bado ni ghali sana. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwa sababu watu hawa wanang'atwa na mbwa au wanyama wa namna hiyo, nadhani iwe ni jukumu la serikali au dawa hizo zitolewe bure kwa sababu hawakupenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ukiangalia *section 84(3) (a) – (d)*, inaelezea kuhusu *control of industrial gaseous wastes and wastes from the vehicles*. Kinachoshangaza ni kwamba, haijaonesha *penalty* yoyote atakayopewa mtu anayekiuka taratibu hizo. Vilevile naomba kujuu adhabu hii atapewa dereva au yule mwenye gari?

Kitu ambacho kimenifanya nisimame ni *sections 73 mpaka 81*, ambazo zinaelezea waziwazi kuhusu usimamizi wa taka ngumu na laini, yaani *solid and liquid waste management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *sections* zote hizi hakuna sehemu yoyote iliyofocus moja kwa moja kwa mtu binafsi anayechafua mazingira. Tumeona maeneo mengi sana, hasa wanaume wanakojoa ovyo sana katika sehemu mbalimbali za miti, stendi na sehemu nyingi. Kwa hiyo, huu Muswada haujaeleza kabisa mtu binafsi anahusikaje na akifanya kosa hilo, anachukuliwa hatua gani. Watu wanatupa taka ovyo wakiwa kwenye magari yao binafsi, mtu mzima ananunua hata vocha unakuta karatasi anatupa nje, anakunywa maji anatupa ile chupa nje, lakini hakuna sehemu yoyote huu Muswada unapoeleza. Kwa hiyo, nadhani hapa kuna upungufu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie Mji wa Dar es Salaam ni jinsi gani ulivyo mchafu, ukipita kila mahali kuna takataka hasa hizi za nailoni. Ukienda kwa mfano, Mji wa Kigali ni msafi sana, lakini si Kigali tu Miji mingi ulimwenguni ni misafi. Ukienda Singapore, ukitema mate tu chini unakamatwa. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna haja ya Mameya na Wakurugenzi labda wapewe *trip* mbalimbali, waende wakaangalie ili waifanye miji yetu iwe safi. Mji wa Dar es Salaam ni mchafu kupindukia, nadhani tusipoweka *responsibility* kwa watu binafsi, tatizo la taka litaendelea kuwa pale pale na harufu mbaya inayotokana na vinyesi pamoja na mikojo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie ya jumla sasa; niseme tu kwamba, Muswada huu ni mzuri lakini umekuja kwa kuchelewa. Nasema umechelewa kwa sababu afya ni jambo la msingi sana, kwa maana ya kwamba, kama hatuna afya njema basi watu tusingweza kuwepo hapa Bungeni leo, watu wasingweza kwenda makazini. Pamoja na kwamba umechelewa, Muswada huu ni *cross-cutting* kwa maana ya kwamba, unapita katika Wizara mbalimbali; kwa mfano, hapa kuna Wizara ya Mazingira, kuna Wizara ya Afya yenyewe, TAMISEMI, Miundombinu, wasiwasi wangu ni kwamba,

mara nyingi jambo linapokuwa linagusa Wizara mbalimbali, inakuwa ni vigumu sana kujua ni nani hasa anawajibika. Kwa hiyo, naomba pamoja na kwamba jukumu hili lipo Wizara ya Afya, waone ni jinsi gani wanaweza kushirikiana kwa pamoja na Wizara hizo nilizozitaja ili isiwe kwamba, hili limetokea anasema mimi sipo *responsible* anayehusika ni Wizara ya Afya, wakati lipo TAMISEMI au Miundombinu. Naomba washirikiane.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la udhibiti wa chakula. Pamoja na kwamba tuna Mamlaka ya Kudhibiti Chakula na Madawa (*TFDA*), kumekuwa na matatizo makubwa sana. Tunajua kwamba, hawa ndiyo wana mamlaka ya kuhakikisha wananchi wanapata chakula salama, lakini hapo hapo kuna wakati *TRA* kwa mfano wanaachia makontena yenye chakula yanapita moja kwa moja, hasa kwa wale watu wanaoaminika mizigo yao haikaguliwi. Hili ni tatizo kubwa sana, tumekuwa kwenye Kamati tumeliongea, tunaomba kama hii mamlaka imepewa kazi hiyo, basi ifanye kazi hiyo ili isiingiliwe na mamlaka nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa sana, kwa sababu kama ambavyo wengine wamesema, ubovu wa chakula umekuwa unawa-*affect* wananchi wengi na kama ambavyo tunajua kinga ni bora kuliko tiba na *actually* kinga ni rahisi zaidi. Kama ambavyo amesema Mheshimiwa Malima Lubeleje ni ukweli kwamba, zaidi ya asilimia 75 ya wagonjwa tulionao hospitalini, wanasumbuliwa na magonjwa ya kuambukizwa, ambayo tungeweza kuyadhibiti. Labda nitoe mfano mmoja, pamoja na kwamba, watu wanasema wana elimu duni ya afya, lakini tuchukulie mfano wa Dar es Salaam; katika wiki nne zilizopita, Dar es Salaam kulikuwa hakuna maji na tunajua magonjwa mengi ya kuambukiza yanatokana na ukosefu wa maji au maji machafu. Kwa hiyo, hata mtu uwe msafi namna gani, kama hupati maji safi bado tatizo lipo palepale. Hii ndiyo sababu nasema huu Muswada, pamoja na kwamba ni mzuri, lakini ni *cross-cutting* na kwa maana hiyo ni lazima Wizara husika zihuashwe.

Tatizo la maji Dar es Salaam ni kubwa sana na ninaamini siyo Dar es Salaam peke yake na ndiyo sababu kunakuwa na kipindupindu na inajulikana kabisa kipundupindu ni ugonjwa unaotokana na uchafu. Kwa hiyo, naishauri Serikali iangalie ni jinsi gani inaweza kuboresha miundombinu ya majisafi na majitaka na kuhakikisha kwamba maji yanatoka muda wote. Tusiwalamu wananchi kwamba ni wachafu, kumbe bado Serikali haijatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nataka kuzungumzia suala zima la usafi wa mazingira. Wengine wamesema lakini mimi bado nasisitiza kwamba ni lazima mazingira yetu yaboreshwe na kama walivyosema wengine kwamba, wale Mabwana Afya na Mabibi Afya waliokuwepo zamani warudishwe ili waweze kuendelea kutoa elimu. Sasa hivi idadi ya wananchi imeongezeka, lakini vilevile mazingira yamekuwa yakiathirika kutokana na hali ya hewa duniani na kutokana gesi katika viwanda vyetu. Kwa hiyo ni lazima Mabwana Afya na Mabibi Afya wawepo ili waweze kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia kwa sababu tunaongelea suala la afya ya jamii ni suala zima la ugonjwa wa malaria; suala hili ni suala

ambalo tunajiuliza kwamba kwa nini bado linaendelea kuwepo na jibu bado ni rahisi ni kwa sababu hatujatibu chanzo chake, yaani yale mazalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko zamani hakuna nchi iliyokuwa inasumbuliwa na malaria kama Italy na Ujerumani, lakini ndugu zetu wale walifanya uamuzi wa kumwaga *DDT*. Suala la kuleta vyandarua halisaidii sana, kwa sababu bado mtu unatembea nje huwezi ukatembea umevaa net; bado wengine hata kama utalala ndani ya *net* lakini utaweka mkono pembeni mbu watakung'ata. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani suala la msingi hapa siyo net ni dawa ya kuua mazalia ya mbu.

Bado Serikali ina jukumu la kufanya hilo na nadhani kama Zanzibar wamefanya, sioni kwa nini huku Tanzania Bara tushindwe kufanya kitu hicho. Lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la wenzetu wanaofanya kazi katika hizi saloon za kutengeneza kucha, nywele na kadhalika. Nimejaribu kufika katika maeneo hayo hasa kwenye saloon za wanaume. Jambo ambalo nimeligundua ni kwamba, vinyozi wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu ni jinsi gani mtu anaweza akaambukizwa UKIMWI kupitia vile vifaa wanavyotumia.

Bado wanatumia spiriti, anamnyoa mtu kwa wembe, ule wembe unapata damu anausafisha kwa spiriti. Kwa hiyo, nadhani bado kuna haja kubwa sana ya Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba, hawa watu wa saloon wanapewa elimu ya kutosha ya jinsi gani wanaweza waka-*sterilize* vyombo vyao ili mtu asije akaenda saloon akatoka na magonjwa mbalimbali.

Hilo nalisisitiza na ninaiomba sana Wizara ya Afya; nawapongeza kwa kuleta Muswada huu, lakini utekelezwe kwa sababu mimi naona bado ni mgumu. Kwa mfano, ukiangalia ukurasa wa 68, kuna suala la makaburi. Wameeleza pale, mimi nikafikiri labda ni Ulaya lakini huku tuendako, inawezekana kwamba kila eneo la makaburi lazima liwe *fenced*, liwe na *attendants* na kuwe na *toilets*. Tukiangalia maeneo ya makabuiri tuliyonayo hata Dar es Salaam ambako ndiyo Jiji na Makao Makuu ya Nchi, bado makaburi yetu yapo wazi wazi; sehemu nytingine hazina ulinzi, watu wanazikwa leo watu wanakwenda kupora pale. Kwa hiyo, nadhani pamoja na kwamba wana lengo zuri, tuone kama kweli haya mambo yatakelezwa, tusiwe tu tunaandika Miswada mizuri sana lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na huu Muswada, lakini naomba wafanye marekebisho na vile vile wahakikishe kwamba, yataweza kutekelezeka. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lyimo kwa kuokoa muda. Kwa shughuli za asubuhi hii, tumefikia tamati yake, tukirudi jioni Msemaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Blandes, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Prof. Mtulya, baada ya hapo tutaingia kwenye Kamati ya Bunge zima.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)  
(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wakati tunasitisha shughuli za Bunge mchana tulikuwa na majina ya Wabunge watatu ambao watamalizia kuchangia kabla hatujaita watoa hoja kujibu. Kwanza kabisa Mheshimiwa Blandes, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi na Prof. Idris Mtulia. Mheshimiwa Blandes karibu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nichukue nafasi hii kuwatakia heri ya mwaka mpya wananchi wa Jimbo la Karagwe wote kwa ujumla. Pili, natoa pongezi nyngi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu wake na timu yake kwa kuleta Muswada mzuri hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri nasema hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kama nilivyo sema Muswada huu ni mzuri. Isipokuwa ninazo hoja kidogo tu za kuchangia ili kuweza kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza naomba nianze na Ibara ya 174 (1), ambayo inahusiana na suala zima la abiria au wananchi wetu watakaokuwa wanasa firi, kuweza kupata huduma ya haja kubwa na haja ndogo. Muswada huu unapendekeza kwamba itakuwa ni sheria kuwa kila mtu lazima apate haja ndogo au haja kubwa katika vyoo ambavyo vimejengwa kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili ni zuri sana na naliunga mkono, isipokuwa nilikuwa nataka nitoe angalizo tu. Kwa kuwa sheria imesema (*shall*), kwamba ni lazima mtu huyo apate huduma kwenye vyoo hivyo. Nilitaka niulize pale inapotokea dharura, kwamba labda mtu amepata ugonjwa wa kuhara ghafla katika sehemu ambazo hazina vyoo hivyo sijui inakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna watoto wadogo, mtoto mdogo haja yake inakuja mahali ambako hakuna vyoo, itakuwaje katika eneo kama hilo. Pengine hata wazee, lakini neno linalotumika hapa ni *natural call*, yaani kwamba mtu kupata haja kubwa au ndogo sio suala la utashi, huwa linatoka mahali popote. Sasa ikitokea mtu yuko kwenye basi na ambapo katika eneo hilo hakuna choo, sasa huyu mtu afanyeje ndani ya hilo basi maana anaweza akaharibu hata ile starehe ya abiria wote ambao wako ndani basi hilo. Sasa nataka kusema kwamba, pengine itolewe *exception* kwamba, pale mazingira yanapobana sana, basi huyo mtu aruhusiwe kupata huduma ya haja ndogo au kubwa sehemu ambayo vyoo havipo. Vinginevyo hii sheria itakuwa ngumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nataka nigosie *section 126 (6)*, hiki kinahusiana na masuala mazima ya maeneo ya kuzika – makaburi (*burial sites*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unasema kwamba: “*Every village authority established under the Village Land Act shall designate a burial site within its area of jurisdiction where dead bodies shall be buried upon obtaining a permit from the authority*”. Maana yake ni kwamba, kila kijiji hapa nchini ambacho kimesajiliwa, kikitaka kuzika lazima kizike katika maeneo ambayo yametengwa kwa madhumuni hayo. Lakini pia lazima ule mwili kabla haujazikwa upate kibali cha mamlaka husika ili kuweza kuzikwa. Sasa, nchi hii tunambua kwamba tunazo sheria za kimila ambazo zinatambulika katika nchi yetu, kwa mfano, kabilia letu sisi Wanyambo watu wa Karagwe; hatuna kawaida hata kidogo ya kuzika miili ya marehemu katika makaburi mbali na maeneo yetu ya nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaburi la babu yangu haliko mbali na mji wangu, ninakoishi na hata leo hii nikifa ninalo eneo ndani ya mji wangu ambalo ni lazima nizikwe pale, ndio mila zetu Wanyambwa wa Karagwe na wanaamini kabisa Wanyambo wa Karagwe kwamba ukimzika marehemu baba yako au mama yako mbali na nyumbani kwako, ni kwamba umeudharau sana huo mwili wa ndugu yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lingine, kuna vijiji ambavyo mpaka sasa ninavyozungumza havina maeneo ya kuweza kutenga maeneo ya kuzikia, ardhi haipo tena, je, hawa watafanyaje? Maeneo mengine ni ya milima na miamba kama kwangu Karagwe, hakuna maeneo ya kutenga ya kuzikia. Lakini lingine tunaposema kibali cha kuzika mpaka kipatikane, tuchukulie kwenye Jimbo langu la Karagwe, kilomita labda 120, maeneo ya Chamchuzi, maeneo ya Nyakakika, maeneo ya Ihembe, maeneo ya Mlongo, Kituntu, mtu amefariki siku hiyo, mpaka kuja kupata ile *burial permit*, ni kazi ngumu sana *unless* tunasema hii *authority* watakuwa na watu wao mpaka kule vijijini ambako wanaweza kupata hii *permit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la dini. Kuna dini ya Kiislam, wenzetu mara nyingi wanapenda kuzika mapema mwili wa marehemu, sijui ni katika masaa mangapi? Sasa mpaka ile *permit* ije kupatikana kutoka Wilayani, hawa watu watazika saa ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilitaka nishauri kwamba, pamoja na sheria kuwa nzuri hivi, basi iangalie haya mapungufu ambayo nimeyataja hapa.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, lingine naomba nigosie *Section 129(3)*, hiki kifungu kinazungumzia suala zima la majeneza. Nimefurahishwa sana na kifungu hiki ambacho kinazungumzia kuweka majeneza katika sehemu za wazi ambako watu wanapita kwa ajili ya kuvutia wateja. Hakuna asiyejua maana ya jeneza. mtu yeoyote ukiona jeneza tu, bila shaka unajua kuwa aidha, mwenzetu maisha yake yamefikia mwisho na hakuna anayependa kuona hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekuwa tukipita Manzese pale Arjentina, unakuta majeneza yamepambwa rangi mbalimbali, kuna jeusi, kuna jekundu, kuna lenye maua, sijui kuna nini. Ukiingia pale mwanzoni mwa Muhimbili, unakuta majeneza mengi yamepangwa pale. Mgonjwa yeoyote huwa anahitaji kufarijiwa, sio kutishwa.

Mgonjwa akishaona jeneza pale maana yake ni kwamba unamwambia sasa wewe unaondoka. Sasa huo kwa kweli sio utu na wala sio ubinadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kuona kipengele hiki na ninakubaliana nacho. Lakini ambacho nilikuwa nasema, sijaona ni adhabu gani itatolewa kwa mtu atakayeweka majeneza hadharani. Mimi sijaona humu adhabu ambayo kwa kweli inakidhi. Yule ambaye atavunja, maana kuna watu wengine wamekuwa na tamaa ya pesa, anaona akiweka majeneza pale basi anavutia wateja, utadhani kwamba yeze siku moja hatakufa. Sasa ningeomba isemwe ni adhabu gani kali itatolewa kwa mtu yule atakayevunja hiyo sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka nigosie kipengele 135 kifungu kidogo cha (1), hiki kinahusiana na masuala ya maeneo ya kuchinja mifugo yetu. Sasa niko *concerned* hapa na neno linaloitwa *slaughter facility*. Neno hili limetumika kuonyesha kwamba hakuna mtu yeoyote anayeruhusiwa kuchinja mnyama katika eneo ambalo halikutengwa na mamlaka kama *slaughter facility*. Sasa shida yangu hapa hili neno halikuwa (*defined*) halijatafsiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Nikiwa kijijini kwangu kule Ihembe II, Karagwe nikataka kuchinja labda mbuzi wangu au kuku ninafanyaje, inabidi nibebe huyo kuku nimpeleke kwenye machinjio ya kule Wilayani nimchinje halafu ndiyo nirudi nyumbani, mwananchi wa kawaida wa mbali wa kijijini anafanyaje katika mazingira kama hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sisi wote ni mashahidi kwamba hata Jiji la Dar es Salaam lenyewe halina machinjio ya kisasa. Ukienda kule Pugu kama una kinyaa hutakula nyama tena. Lile eneo lilikuwa limetengwa la *Sungura Textile*. Nakumbuka mzee mmoja anaitwa Idd Simba aliwahi kuleta mapendekezo kwenye Kamati ya LAAC kwamba eneo hilo alikuwa anapendekeza lijengwe machinjio ya kisasa, lakini mpaka sasa hivi Jiji la Dar es Salaam halina. Sasa kama Jiji la Dar es Salaam hakuna machinjio ya kisasa huko kijijini itakuwaje? Ningeomba hapa tupate ufanuzi, tusitunge sheria ambayo haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusiana na suala zima la upimaji nyama. Sheria tunayotaka kuitunga hapa inasema kwamba lazima nyama yote ipimwe kabla ya kuchinjwa na hata baada ya kuchinjwa, hili sina tatizo nalo. Lakini ninalotaka kusema hawa watu tunao wa kwenda kupima nyama vijijini? Nitatoa mfano mdogo, kwenye Jimbo langu la Karagwe ninazo Kata nne, Kata moja inaitwa Ihembe Kata nyingine Lugu, Kata nyingine Nyakasimbi na Kata ya Nyaishozi. Kata hizo zote nne zenye vijiji kumi na kitu zinaye Bwana Mifugo mmoja na huyo Bwana Mifugo ana pikipiki ambayo haina mafuta siku zote.

Sasa niambie wananchi wa Kata nne hao kila mtu akitaka kuchinja Bwana Mifugo atafika saa ngapi kwenda kupima hiyo nyama. Pengine Serikali itueleze kwamba imejiandaa kupeleka Mabwana Mifugo ama Mabwana Afya kwa kila kijiji, hapa naweza kukubaliana na kifungu hiki, vinginevyo tutatunga sheria ambayo hata sisi Wabunge

itatubana. Mheshimiwa Mbunge akitaka kuchinja mnyama wake huko, atashindwa kupima kwa sababu hakumpata huyo Bwana Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu 163(b)(x) kimenifurahisha sana kwa sababu kimewajali wale mavu, kinasema wamiliki wote wa shule za binafsi na za Serikali lazima waweke *facilities* kwa ajili ya wale mavu. Nasema kwamba, huu ni mwanzo mzuri, lakini Serikali ilete sheria ya wale mavu ili tuweze kuyaweka mambo mengi sana ya wale mavu katika sheria zetu. Pia nilitaka niseme kwamba kwa wale watakaokaidi, wachukuliwe hatua za kisheria haraka sana ikiwa ni pamoja na kufunga shule zao.

Lingine, kuna kifungu cha 83 (1) kiko *very interesting*, yaani hiki nadhani kiko *for academic purposes*. Hakiwezi kutekelezeka, kinasema kwamba sheria hii kama ikipita ni kwamba kila nyumba ambayo utakuwa nayo au makazi ni lazima iwe na jiko lenye *chimney*, jiko la kupikia lenye sehemu ya kutolea moshi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya nchi yetu kila mtu anayafahamu, tunaishi kwenye nyumba za msonge, tunaishi nyumba ambazo ni za ajabu ajabu, ndiyo hali yetu sisi Waafrika au Watanzania. Sasa unaponiambia kwamba sheria itahakikisha kwamba kila nyumba inakuwa na jiko la kisasa lenye sehemu ya kutolea moshi, sidhani kama sheria hii itatekelezeka. Tusije tukatunga sheria baada ya siku mbili, tatu tukakuta ni ngumu tukaja kurudi hapa kuibadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sheria hii imezungumzia masuala mazima ya kuhamisha viwanda vinavyotoa moshi katikati ya makazi. Kuna kiwanda cha Chibuku pale Dar es Salaam Ubungo, ningeomba Serikali ianzie hapo. Hicho kiwanda kiko katikati ya Mji kinatoa harufu mbaya ya pombe wengine hatunywi pombe, lakini pia kinatoa moshi mkali sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele kingine ni hiki kinachohusiana na (*nuisance*) usumbufu au kero. Zimeorodheshwa *nuisance* nyingi katika sheria hii. Mojawapo ambayo imenivutia sana ni wale wanaopiga miziki kwenye baa, kwenye kilabu ambazo ziko kwenye makazi ya wananchi. Wale watu kwanza ni wakorofi, muziki wao unapigwa kuanzia saa nne za usiku pale watoto wanapojiandaa kulala na siyo watoto tu pengine na watu wazima, utapigwa mpaka karibu na alfajiri. Mtoto halali akienda darasani anasinzia hata na Mbunge ukija hapa Bungeni unasinzia. Sasa nilitaka niseme kwamba Serikali lazima ichukue hatua za madhubuti tusiishie kutunga sheria hii na miziki ikaendelea kupigwa kwenye majumba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi ya kuzungumza lakini kwa sababu ya muda naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako, ulikuwa *very detailed*. Sasa namwita Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie Muswada huu ambaeo upo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kuitazama Sheria hii na Tanzania ya leo sioni nafasi ya Sheria hii kuweza kufanya kazi ipasavyo. Katika Tanzania ambayo ina makazi ya holela, Tanzania ambayo imejengwa bila mpangilio inakuja inaletwa sheria ambayo kwa kweli ina umuhimu wa kipekee kabisa inahusu na inagusa afya ya jamii. Yapo maeneo mengi sana sijui utekelezaji baada ya hii sheria kuitishwa utakuwa namna gani au kama Serikali imekwishajiandaa ili kuweza kuwatengenezea Watanzania mazingira mazuri na salama yanayojali afya zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwanza nianze na eneo moja ambalo linahusu chanjo. Chanjo kwa kweli ni muhimu na hatuna sababu yoyote ya kusema neno juu ya chanjo kwa sababu tunafahamu kabisa umuhimu wake. Lakini ninachotaka kukizungumzia kuhusu chanjo ni pale tu maana ya kuwepo hizi chanjo inapopotea inaposimamiwa na watu wasiokuwa wataalam wa afya. Sasa ni vyema basi Serikali itoe kauli juu ya utekelezaji wa hizi chanjo zinazofanywa nchini. Nikichukulia tukio la hivi karibuni tu lililowapata wanafunzi wa shule kule Sumbawanga na Morogoro ambao wengi walipata matatizo katika ile chanjo au dawa za kichocho wakaanguka, lakini ni kwa sababu kulikuwa hakuna wataalam wa afya waliokuwa wanasimamia zoezi hilo, na zoezi hilo waliachiwa watu wasiokuwa na uzoefu na utaalam wa afya.

Naomba sana Wizara ya Afya katika masuala yanayogusa afya za binadamu wawe makini sana pale ambapo wanaona hawana watu wa kutosheleza wa kulisimamia zoezi, basi walifanye angalau hatua kwa hatua, lakini chini ya usimamizi wa watu wenye uzoefu na utaalam mkubwa kwa masuala ya afya ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia maji ni tatizo lingine, magonjwa mengi yanababishwa na maji, kipindupindu ni moja katika magonjwa ambayo yanababishwa pia na maji, kuharisha damu na kadhalika na haya ni magonjwa ambayo yanaweza yakazuilika tu pale ambapo tutakapokuwa tumefikia mahali wananchi wetu wamepata maji safi na salama katika maeneo ambayo wanaishi. Ni kwa sababu ya kutokulisimamia suala la kuhakikisha watu wetu wanapata maji safi na salama milipuko ya magonjwa kama kipindupindu na kadhalika hutokea mara kwa mara na hasa katika Jimbo langu la Uchaguzi pale Mjini katika Kitongoji cha Mpanda Hoteli kila mwaka linakuwepo tatizo la kipindupindu kwa sababu ya kunywa maji ya kutoka Mto wa Mpanda, maji ambayo si safi na si salama.

Kinachohitajika ni kisima tu ambacho hakizidi shilingi milioni 15, lakini Serikali inasita kutoa huduma hiyo ya kisima matokeo yake inaingia gharama ya mamilioni kwa ajili ya kutibu wagonjwa wa kipindupindu kila mwaka. Kwa hiyo, Serikali pia iangalie, yapo mambo ambayo inaweza ikayazuia kama itatimiza wajibu wake na kuhakikisha kwamba inawapatia wananchi huduma inayostahili.

Labda nzungumzie pia suala la mazalia ya mbu, yameelezwa katika Sheria hii katika kipengele namba 30. Ni kweli ili tuweze kushinda vita dhidi ya malaria ni lazima tuangamize mazalia ya mbu katika maeneo ambayo tunaishi na yanayotuzunguka. Sina tatizo juu ya eneo hilo na umuhimu wake kwa sababu ya tatizo la malaria jinsi lilivyo,

hofu yangu tu ni pale sheria inapotoa adhabu ya faini ya 200,000/= au kifungo cha miezi mitatu kwa kutazama kosa ambalo amelifanya mtu pengine tu la kuacha vifuu vya nazi au maji yakatuama na mbu wakazaliana, mtu huyo anapewa adhabu kubwa kiasi hiki bila kujali kipato chake ni kiasi gani. Hasa Watanzania wengi ambaao kipato kwa mwezi wengine ni chini ya shilingi 80,000 lakini anapewa adhabu kubwa kiasi hicho. Adhabu inastahili, lakini nafikiri kwamba adhabu iliyowekwa kwenye sheria ni kubwa sana kwa Mtanzania wa kawaida na kabla ya kuwafikisha mahali pa kupewa adhabu, basi elimu ya kutosha itolewe ili wananchi waweze kuangamiza mazalia ya mbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa na mashaka na kifungu 73 ambacho kinahusu taka ngumu na taka za majimaji. Sheria inaeleza bayana kabisa kwamba kila mtu atatakiwa awe na madebe au vyombo vya kuhifadhiwa taka na viwe na mifuniko ni jambo jema na nzuri kabisa kwa ajili ya afya zetu. Lakini sheria haisemi chochote pale mwenye jukumu la kuziondoa hizo taka anaposhindwa kuziondoa taka hizo. Ni kwamba watu wataweka madebe, wataweka mapipa lakini je, kuna utaratibu gani ambaao umewekwa wa kisheria kama mamlaka hizi ambazo zina wajibu na majukumu ya kuziondoa hizi taka wanaposhindwa kutimiza wajibu wa? Tatizo la kuzagaa kwa taka, kulundikana kwa taka katika Miji yetu ni jambo ambalo limekwishazoeleka kabisa. Ni namna gani Halmashauri zetu zimejipanga katika eneo hili la usimamizi na uondoaji taka. Ni matarajio yangu kwamba Serikali itatoa msukumo wa aina yake kuzisaidia Halmashauri zetu ziweze kukabiliana na hii changamoto ya kuweka Miji yetu kuwa safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nilikuwa nakitazama kifungu 83 ambacho ndugu yangu Mheshimiwa Gosbert Blandes amekizungumzia sasa hivi kuhusu hizo nyumba ambazo zinatakiwa ziwe na njia za kutolea moshi katika majiko. Sheria hii nilikuwa naitazama sana kama haikutazama mazingira ya uhalisia wa nchi yetu na hasa pale inapotamka kabisa katika kifungu hicho hicho cha 83 (2) kwamba: “*Every dwelling house shall have a way ventilated kitchen*, kwamba kila nyumba ambayo ni ya makazi basi ni lazima iwe na jiko lililokuwa nzuri lenye kupitisha hewa ya kutosha. Sasa tunazitazama nyumba gani, kwa sababu zipo nyumba ambazo wanaishi Watanzania ambazo wote tunafahamu tunafanyaje kwamba hao wanaishi katika nyumba hizo watakuwa wametenda kosa kwa mujibu wa sheria hii au sheria hii ni kwa ajili ya kundi fulani tu la Watanzania na kundi fulani la Watanzania hawahusiki na sheria hii? Ni sheria ambayo imetazama sana mazingira ya Mjini kuliko mazingira yanayowagusa Watanzania wengi wanaishi vijijini. Hebu tuleteeni sheria ambayo itasaidia sana kutengeneza afya za wananchi wengi zaidi wanaishi vijijini kuliko kujikita na sheria ambazo zinajikita sana katika maeneo ya Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa pia nalitazama eneo lingine katika kifungu 129 ambacho kinahusu majeneza, sina tatizo kabisa na madhumuni ya sheria na mahitaji ya sheria pia kuzuia kuyaweka majeneza hadharani na kutangaza vitu kama hivyo. Lakini hofu yangu ni pale kwamba mtu hawezi kutengeneza sanduku la kuzikia mpaka awe na leseni ambayo ameipata kutoka kwenye mamlaka. Msitazame Dar es Salaam na miji ambapo kuna watu wanaotengeneza masanduku kama hayo.

Mpanda hawatengenezi sanduku mpaka mtu kafa. Sasa huyu anayetengeneza sanduku wakati linahitajika sanduku kwa sababu wengi uwezo wa kutengeneza sanduku haupo kwa hiyo, wala hawazikii masanduku lakini wanapohitaji sanduku wanakwenda kwa fundi seremala wanatengeneza sanduku. Sheria sasa inalazimisha kwamba yeyote atakayefanya biashara ya kutengeneza masanduku basi ni lazima awe na leseni. Naona ni kikwazo hasa kwa watu wa pembezoni na kule vijijini. Nadhani hapo hamkuwatendea haki kwa mujibu wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nikitazama kifungu 147 ambacho kinagusa masoko. Natazama masoko yetu katika Tanzania ya leo, natazama sheria inavyohitaji masoko yawe ya namna gani, sijui tutafanyaje. Kwa sababu ama vinginevyo kwa mujibu wa sheria hii itakapoanza kutumika, basi wenye mamlaka na wasimamizi wa sheria hii ni lazima wayafunge masoko yote katika nchi hii kwa sababu hayakidhi matakwa na mahitaji ya sheria inavyotaka. Sheria imeainisha vitu vingi ambavyo vyote vimeorodhesha hapa, leo ukienda katika masoko yetu mpangilio, maji, vyoo na kadhalika ni matatizo makubwa sana. Sasa sijui sheria hii itabaki tu kwamba imeandikwa na kwamba imepitishwa lakini haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, nilikuwa nataka tu kufahamu Wizara imejipanga namna gani katika suala la kusimamia sheria hii? Kwa maana kwamba wale watu muhimu sana watakaoisimamia sheria hii ni Mabwana Afya. Kipindi cha nyuma kwa sababu wanazozijua au kwa makusudi vyuo vyote ambavyo vilikuwa vinawaandaa Mabwana Afya katika nchi hii vilifungwa kikiwepo cha Mpwapwa, Mpanda, Kibondo na kadhalika, leo Serikali inajipanga namna gani katika kukabiliana na suala la wasimamizi wa sheria. Muda mrefu umepita hawakufundishwa hawakuandaliwa watalaan wa kutosheleza kuweza kusimamia sheria hii. Hii ndiyo hofu yangu. Nitafurahi kujua mpango wa Serikali ulivyo katika kuisimamia sheria hii ili iwe na maana katika Tanzania ya leo. Ahsante sana nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nimalizie ngwe hii yetu ya leo. Hakika napenda kuipongeza sana Wizara ya Afya kwa kuleta Muswada huu ambaa hapa nimeuandika *three in one*, wenyewe umeondoa uzito uliokuwepo wa kuanza kutazama sheria ya magonjwa ya kuambukiza (*Infection Disease Act*), halafu utazame tena magonjwa ya *International Notify Diseases Act*, halafu utazame tena magonjwa ya *Mosquito Control Act* hayo yote yapo katika kitabu kimoja.

Kwa hiyo, kwa jambo hili naona wamefanya jambo nzuri. Ila nilikuwa nataka niseme tu kwamba kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tulipitia Muswada huu vizuri. Lakini hata hivyo, yapo mambo nadhani yanabidi kutiliwa mkazo. Mathalani madhumuni yenyewe makubwa ni kuboresha afya ya wanajamii na ukiboresha afya yao basi umri wao utazidi na watazalisha zaidi, hili ni jambo zuri sana.

Hakika Serikali tungeiomba ifahamu tu kwamba, suala la afya ya jamii ni masuala mtambuka kwa sababu wahuksika wakubwa humu ndani ukiacha Wizara ya Afya, kuna Wizara ya Miundombinu. Mara nyingi tunapata matatizo kwa miundombinu mibaya, imeshasemwa ya kuwezesha kufikika sehemu ya hospitali au dispensari, lakini hata mijini saa nyingine kazi inafanyika madimbwi yanaachwa ovyo mvua zinanyesha, mazalio ya mbu yanazidi kuwepo. Kwa hiyo, miundombinu ni Wizara ambayo nadhani wafanye kazi karibu sana na Wizara ya Afya katika suala ya kuboresha afya ya jamii. Pili kama ilivyokwishatamkwa kama ukiweza kuwapa watu maji safi na salama ya kutosha utapunguza magonjwa ya kuambukiza kwa asilimia themanini kirahisi kabisa, kwa hiyo Wizara ya Maji ni muhimu sana kufanya kazi karibu sana na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano nilivyokuwa Mganga Mkuu Kiongozi kulitokea *cholera* Dar-es-Salaam na tulichukua maji ya bomba tukaenda kuyapeleka kwa Mkemia yakaonekana yana vidudu vyta *cholera*. Yule *Managing Director* wa DAWASA wakati ule alipata tabu kweli kweli kwa sababu hatuwezi kuiamini Kampuni ya kusambaza maji, halafu Kampuni hiyo maji yale ukifungua unapeka *laboratory* unakuta yana *cholera*, kwa hiyo pale tulizozana, hata hivyo sikuwa na sheria ya kumpeleka kortini, lakini mambo baadaye yalikuwa mazuri, kwa hiyo suala la maji ni muhimu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine mtambuka ni elimu ya afya binafsi yaani *Personal Hygen Education*. Wakati wetu tulivyokuwa *school* tulikuwa kabisa na leo asubuhi nimewakumbusha Watanzania kwamba tulikuwa tunaonyesha mikono hivi kabla ya kuingia darasani, Mwalimu anapita kwa kila mstari kuangalia kucha *zimekatwa*, nywele zimetengezwa vizuri, mtu ametengeza nguo vizuri, sasa ukiwa na mtu mmoja mmoja afya yake imewekwa vizuri basi afya ya jamii itakuwa kwa jumla nzuri zaidi, nilikuwa naomba sana suala hili litiliwe mkazo. Huu ilikuwa ni utaratibu wa walimu wetu wa zamani, kwa hiyo naomba huo utaratibu utazamwe upya na urudishwe

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulivyokuwa darasa la nne vile sijui, tulikuwa tunafundishwa elimu ya afya, mtu unajua kabisa kwamba ukikaa katika nyumba yako, yako mambo unatakiwa uyatimize, kwanza kuzuia malaria kwa kuua vimelea vyta mbu pale wanapozaliana. Tulikuwa tunafundishwa hata kumwagia mafuta ya taa tu katika madimbwi yale, tunafundishwa kufyeka nyumbani kwetu, tunafundishwa mambo yote yanayoonekana katika sheria hii, Kifungu cha 30 mpaka 34. Mambo haya nimeyatazama kwa uangalifu sana, ni mazuri, tatizo lake watu wetu sijui wana nini, kutekeleza inakuwa tabu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, a wakati ule tunakua pale Dar es Salaam, utakuta kabisa mara moja kwa wiki hivi wanapita Mbwana Afya, wamebeba mtoto lakini ni mzinga umejaa dawa na kila nyumba ina karatasi, ina fomu ya Bwana Afya inasema Bwana Afya kapita leo tarehe kadhaa. Nimetazama afya ya mazingira ya nyumba hii ni salama na kwamba anapita uani katika vyoo vyta mashimo anatia dawa na sehemu zote na vile vile watu wengi walikuwa wanapelekwa kortini, katika kuonana na Bwana Hakimu kwa sababu ya kukosa au kuvunja sheria hizi. Sasa pamoja na kwamba imeandikwa vizuri, lakini mambo hayo yalikuwepo zamani vilevile, kumetokea nini mpaka siku hizi

yule Bwana Afya hatembei tena, wala hatumuoni vizuri wala hatuoni kutiliwa mkazo kwa watu ambao wanavunja taratibu hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine nalo ni suala la vyombo vya Mahakama, mara nyingi *local authorities* nyingi zilikuwa na korti zake, kulikuwa na maaskari nadhani siku hizo watu wa *City* bado wanao maaskari hao, wangeweza kabisa kutumika. Asili ya mwanadamu yoyote akitiwa msukosuko mara moja juu ya jambo ambalo anaweza kulifanya atafanya tu na huko nadhani hii habari ya kupita na kuangalia sehemu za usafi wa mazingira ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 66 kinanikumbusha wakati nilivyopata *certificate of occupancy* ya nyumba yangu ya kwanza miaka ya 72. Siku hizi naona watu wanajenga kila mahali hata hatuoni, yani mtu anamaliza anaingia hata katika choo chake cha kuvuta au hicho cha lindi na watu wenyewe madaraka na uwezo wa kuhimiza sheria hii wapo, inatia simanzi kidogo. Hapa imeelezwa kwamba kutakuwa na lazima kupatikane *certificate of occupancy* kwamba nyumba yako sasa ni sawasawa watu wanaweza kuishi kwa usalama, lakini nyumba za mjini nyingi siku hizi hawana *certificate of occupancy*, sasa utaona mambo kama haya yanaturudisha nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sasa nataka niirudie Wizara kwa maana ya kunitoa hofu yangu tu, kwamba hivi tunaweza kutimiza maudhui ya sheria hii, tunao watumishi wa kutosha? Nadhani jibu ni wazi, kwamba vyuo vilifungwa, lakini tunaomba sana sasa na huu niko mwisho, naomba kuwe na *aggressive training* ya Maafisa Bwana Afya kwa makundi makundi, iwe kama Wizara walivyoamua kufundisha *Medical Assistant or Clinical Officers* kwa makundi na makundi na wauguzi basi na kada hii ifundishwe kwa wingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ninaloomba ni kwamba hawa wenzetu mishahara yao iko chini mno, maslahi yao yatazamwe upya, kwa maana hiyo sina maana ya Mabwana Afya tu kwa kweli hata Madaktari, nimeshakuwa Daktari najua maneno ninayozungumza. Mishahara yao jamani ni midogo mno tuiangalie, wanafanya kazi nzito. Kwa hiyo, nadhani ili tuifanye kazi ya Bwana Afya iwe inapendwa tuongeze mishahara yao, tuongeze maslahi yao. Kwa hiyo hili ni jambo linaonekana kama mzaha lakini jamani kazi yao kubwa, tuwape nao *something*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho nilikuwa nataka niombe sana kwamba kama tukiweza kumpiga vita mdudu mbu, kama walivyoweza kule Kisiwani Pemba na hata Unguja, basi tuvae njuga hapa kwetu tufanye kazi hiyo na kwa ajili ya kuleta kumbukumbu nzuri kuwe na wiki ya kuua mbu kwa Tanzania nzima. Hii itatufanya tuwe tunajua kwamba adui yetu mkubwa ni mbu na kuwa tutashughulikia vizuri na ku-control magonjwa ya malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache naunga mkono hoja na nakushukuru, asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa msemaji wetu wa mwisho katika kuchangia Muswada huu. Sasa nitamwita mtoa hoja kwanza Naibu Waziri halafu Waziri mwenyewe, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Bunge zima. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii. Lakini kabla sijachangia pia nasema naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii pia kupitia Bunge lako Tukufu kuwatachia heri ya mwaka mpya 2009, Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu, atuzidishie afya nguvu na hekima katika jitihada zetu za kuwashudumia wananchi wanaotutegemea. Lakini vilevile nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Dokta Thomas Kashililah, kwa kuteuliwa kwake kuwa Katibu wa Bunge, wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyezi Mungu amuongoze. Baada ya salamu hizi sasa naomba nianze kuchangia kwa kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, wakati wa kuchangia Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii na Mheshimiwa Waziri baadaye atahitimisha kama ulivyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, katika mchango wake wa maandishi alikuwa amezungumzia kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeonekana kuangalia sana zaidi eneo la matibabu kuliko kuzuia magonjwa kwa maana hiyo akawa amependekeza kuwe na *Regional and District Medical Officers of Health*. Lakini vilevile pawepo na *team work* ya wataalamu wa Wizara vikiwemo vitengo vya Afya na Mazingira na TFDA na taasisi mbalimbali kama OSHA wakishirikiana na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mkoa au wilaya inayo timu ya Wataalamu wa Afya inayoongozwa na *RMO* na *DMO* wakisimamia shughuli zote za kinga na tiba na hii ni kuzingatia kufanya kazi kwa pamoja ili zisivurugike na hii inaitwa *Regional Health Management Team* na *Council Health Management Teams*. Katika kusimamia masuala ya afya ya jamii suala la ushirikiano ni suala la msingi nakubaliana, kwa hiyo Wizara inazingatia kwa mfano bidhaa mbalimbali zinazoingia na zilizomo ndani ya nchi huwa zinakaguliwa na kupitia kwenye Halmashauri husika lakini vilevile huwa wanashirikiana na TFDA. Lakini pia kuna Kamati ya Ukaguzi wa Vyakula na dawa ambayo inaitwa *Council Food and Drug Committees* ambayo ipo katika kila Halmashauri. Vilevile Sheria ya Chakula na Dawa na Vipodozi ni mojawapo ya kuhakikisha kwamba vyakula na dawa vinakaguliwa

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mbunge wa Kilombero, katika kuchangia kwake amesema kwamba watendaji wa mitaa au wamepora madaraka ya maafisa afya kiutendaji, lakini kwa kupitisha sheria hii kutarejesha uwezo wa maafisa afya ambaa uliporwa na watendaji wa mitaa au vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaafikiana na Mheshimiwa Mbunge kwamba umuhimu wa sheria hii katika kuweka utaratibu wa majukumu ya kiutendaji kwa mamlaka zinazohusika ikiwemo mabwana afya kwamba utasaidia. Lakini labda niseme tu kwamba watendaji katika serikali za mitaa hawakuwa wamepora wala hawakuwa wameteka nyara, bali walikuwa wanatimiza wajibu wao. Kwa kuzingatia kwamba tulikuwa na upungufu mkubwa sana wa hawa Maafisa Afya, mimi naamini katika maeneo husika kwasababu hawa watendaji wa Serikali wako kisheria kwa hiyo walikuwa wanatimiza wajibu wao kuhakikisha kwamba wanatusaidia kuweka mazingira mazuri katika maeneo husika. Kwa hiyo vilevile tunapenda tuwapongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Sarungi, Mbunge wa Rarya, anasema kwamba anapendekeza kuwe na Maafisa Afya kwa kila Kituo cha Afya au Tarafa, lakini vilevile anasema kwamba kila Halmashauri ya Wilaya katika bajeti ya afya itenye fungu maalum kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya magonjwa ya kuambukiza. Ni kweli kabisa Wizara imepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na itaufanyia kazi. Vilevile kwa jinsi tutakavyokuwa na uwezo basi Serikali itaweza kuhakikisha kwamba Maafisa Afya wataweza kupatikana katika ngazi zote husika kama Mheshimiwa alivyopendekeza.

Mheshimiwa Profesa Maghembe, Mbunge wa Mwanga na Mheshimiwa Waziri, anasema kwamba Wizara irudie kazi ya kuangamiza viluwiluwi wanaoleta magonjwa ya malaria, lakini anasema kwamba Wizara iongeze nguvu ya kupambana na ugonjwa wa kichocho kwa kuwa Wilaya ya Mwanga tatizo hili ni kubwa sana katika maeneo ya kule Kilewe, Kivulini, Kituri, Kihururu na Jipe na anaomba timu ya wataalam imtembelee huko Mwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inakubaliana na ushauri wake kwamba viluwiluwi viangamizwe lakini kuhusu ugonjwa wa kichocho ipo *program* maalum ya Kitaifa ambayo inashugulikia ugonjwa wa kichocho. Kwa hiyo Wizara itazingatia na tutaishauri timu ile iweze kufika katika Mkoa wa Kilimanjaro na hususan katika Mkoa wa Wilaya ya Mwanga ili kuweza kuona na kutoa maelekezo kwa wale wenzetu wanaoishi kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, alisema tatizo kubwa la sheria nyingi hazisimamiwi ipasavyo. Aidha amehoji ni jinsi gani kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii imejiandaa kukabiliana na tatizo hilo? Lakini vilevile pia ameuliza sheria hii inatekelezwa vijijini tu au ni sheria ya wakazi wa mijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii imewekwa kwa mujibu wa majukumu ya utekelezaji katika ngazi mbalimbali za uongozi na kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta kama ilivyokuwa imezungumzwa. Lakini vilevile madhumuni ya sheria hii iliyoitungwa ni kutekelezwa Tanzania Bara kwa maana hiyo itagusa maeneo ya mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mbunge wa Magogoni, amependekeza Muswada huu usimamiwe vizuri na Serikali na kuachana na mazingira mabaya na kuepuka magonjwa ya kuambukiza. Tunachukua ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janet Morris Masaburi, Mbunge wa Viti Maalum, anatoa pendekezo kwamba Muswada huu uwe na kipengele kinachodhibiti kiwango cha sauti zinazotoka katika majumba ya starehe na sehemu nyinginezo na ziwe na *sound proof*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, kuhusu suala hili umepokelewa aidha na wakati wa kutengeneza kanuni basi utekelezaji wa sheria hiyo utazingatiwa na nakala ya sheria alikuwa ameomba kwamba zisambazwe katika kila Halmashauri ili zifike katika vijiji. Sasa itakapofikia hapo basi tutaweza kuona ni jinsi gani Wizara ya Afya kwa kushirikiana na *TAMISEMI* basi sheria hii itafikia mpaka ngazi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dokta Mzeru Omar Nibuka wa Morogoro Mjini, anasema Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iimarishe ukaguzi wa vyakula na madawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inarudiwa tena na kwa kutumia vifaa vyatya kisasa pamoja na wafanyakazi wenye utealam wa kutosha. Wizara inayo taasisi ya kudhibiti ubora wa usalama wa chakula na dawa, vipodozi na vifaa tiba, ambayo ni *TFDA* ambayo tunaifahamu. Katika kuimarisha udhibiti wakaguzi wameteuliwa katika maeneo mbalimbali na katika vituo 32 vya forodha nchini. Wizara kupitia mamlaka ya chakula na dawa imeimarisha ukaguzi wake kwa kushirikiana vilevile na *TAMISEMI*. Kwa hiyo shughuli hii inaendelea na tutaendelea kuhakikisha kwamba tunafanya vizuri zaidi kuweza kuipa nguvu sheria hii ambayo tunaitengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, Mbunge wa Viti Maalum, anasema *Section 86* katika Muswada huu, pawepo na ufuatiliaji wa *waste management* unaotokana na usafiri wa reli na ndege; ujenzi wa vyoo katika maeneo kadhaa ya reli inapopita, Wizara izingatie kutoa kipaumbele kutupa mabaki ya kemikali, matumizi ya *DDT*, lakini vilevile ma-generator na ma-computer yanapokuwa yanaharibiwa basi yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa ushauri huu lakini vilevile Wizara ya Afya, itazingatia kuhimiza suala la ujenzi wa vyoo katika maeneo ya reli. Nafikiri tutashirikiana pamoja na Wizara yake, lakini vilevile Baraza la Mazingira *NEMC* na *TFDA* na Kilimo na Wizara zote ambazo zinahusika, basi na sisi tutashughulika ili tuhakikishe kwamba haya yote aliyoyataja yanafuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *DDT*, ni kweli kwamba Wizara ya Kilimo ilikuwa na mabaki ya dawa za *DDT* na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, italicchukulia kwa umuhimu wake tutakapokuwa tunatumia *DDT*. Kwa upande wa majenereta tatizo sio majenereta isipokuwa ni mafuta ya kulainisha

*transformer* ambayo ni kemikali yenye sumu. Kwa hiyo Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, vilevile watafanya mpango wa kudhibiti kemikali hii ili kuhakikisha kwamba haiwezi kuleta madhara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dokta Mpanda Samson, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, alikuwa amepongeza, tunashukuru lakini anasema kwamba tumezingatia watu wenye matatizo ya ulemavu na kwamba alikuwa ana masuala mawili alizungumzia kuhusu suala la nyumba ya vijibweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala analogumzia kwamba kuna nyumba ya vijibweni ambayo alikuwa ameizungumzia hapa nadhani tutakaa na Mheshimiwa Mpanda tuweze kuona ili hili suala nafikiri sio la Wizara ya Afya lakini kama yeje kwa mtu mwenye ulemavu yuko katika Wizara yetu basi tutashirikiana na Wizara husika aidha labda itakuwa ni Wizara ya Ardhi au labda Kazi na Maendeleo ya Vijana. Basi tutaona ni jinsi gani hili suala la nyumba ya Vijibweni ambalo analizungumzia atawezu kupatiwa msaada. Lakini vilevile suala la kutoa vyandarua kwa watu wenye ulemavu, Serikali inajiandaa kuweza kutoa vyandarua si kwa watu wenye ulemavu tu lakini kwa wananchi wote waweze kuwa na vyandarua vyao. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumeanza mgawo huu kwa makundi maalum, tutazingatia kuwa sio wale watoto tu lakini hata walemavu waweze kupatiwa vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum, alizungumzia kuhusu suala la chanjo kwamba je, kosa likitokea kwa upande wa Mamlaka sheria inasemaje? Kwa mfano, wanafunzi waliopata madhara. Lakini vilevile amezungumzia mambo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri pia atayatolea maelezo kama mambo ya *summary conviction*, masuala ya uwezekano wa utaratibu wa muda wa kurekebisha kosa badala ya kujikita kwenye faini kwamba tusiwe tunaweka kama vile ndio sasa tumeweka mahali pa kupatia pesa. Vilevile amezungumzia marekebisho ya kwenye *by-laws*, mambo madogo ya kurekebisha sentensi, hili tutalizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inamshukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya matumizi ya baadhi ya maneno katika Muswada. Kwa hiyo Wizara itaufanya kazi ushauri wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mlingwa, yeje Mbunge wa Shinyanga Mjini, katika mchango wake wa maandishi alizungumzia suala la magari ambayo yanaingizwa hapa nchini yaweze kuangaliwa vizuri kwa sababu baadhi ya magari na yenye yanasaidia pia katika uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili ni suala ambalo tutalisimamia sisi na wenzetu wanaoshughulika na uuzaaji wa magari. Lakini pia na sisi kwa upande wa kiafya tutafanya kazi yetu kuhakikisha kwamba magari yanayoingia yana ubora, lakini pia alikuwa ameweza angalizo kwamba kama tutaangalia magari yote tuyasimamishe basi wananchi watakosa magari, kama nilikuwa nimemwelewa vizuri. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba tutatumia haki ili yale ambayo ni mabovu yafuate utaratibu

lakini yale ambayo yanakidhi viwango basi yataingia Wizara ya Fedha pamoja na wale wote ambao wanahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ishengoma, katika mchango wake wa maandishi vilevile alikuwa anazungumzia masuala mazima ya malaria lakini kusimamiwa vizuri kwa suala hili la hii sheria. Lakini pia alizungumzia suala la upungufu wa madawa katika vituo vya kutolea huduma na kwamba Serikali pamoja na ufinyu wa bajeti ilionao lakini tuangalie kwa sababu wananchi wanapata taabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wake tumeuchukua na tumekuwa tukizungumza naye katika maeneo mengi kwa sababu na yeye pia ni mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kwa hiyo tunashukuru kwa ushauri wake na sisi tutazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tumeepanga kwamba, nitajibu hoja za maandishi na Mheshimiwa Waziri atajibu hoja za wale ambao wamechangia kwa kuzungumza. Lakini napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wajumbe wa Kamati ambao wametusaidia sana katika kuutengeneza Muswada huu, lakini vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao waliyoitoa na vilevile kwa ushirikiano wao ambao wanatupatia katika Wizara yetu. Ninawashukuru sana, ahsanteni sana.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nyingine ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza ndani ya Bunge lako Tkufu na Waheshimiwa Wabunge ambao walipata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Wote nawashukuru na michango yao tutaizingatia kwa sababu nia ni kusaidia katika utekelezaji wa hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatambue waliochangia; kwanza wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ambao ni Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii; Mheshimiwa Dokta Ali Tarab Ali, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Paschal Constantine Degera, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Dokta Aisha Omar Kigoda. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Janet Moriss Masaburi, Mheshimiwa Vuai Abdala Khamis, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Castor Ligalama, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, Mheshimiwa Dokta Mzeru Omari Nibuka, Mheshimiwa Janet Bina Kahama, Mheshimiwa Dokta Christine Ishengoma, Mheshimiwa Dokta Samsoni Mpanda, Mheshimiwa Dokta Charles Mlingwa, Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, Mheshimiwa

Dorah Mushi. Nawashukuru sana wote walioweza kupata nafasi ya kuchangia na kama nilivyosema michango yao itaboresha utendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu hoja za Wasemaji Wakuu; Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', alitoa hoja kama ifuatavyo: Alisema sehemu, vifungu na ibara vya Muswada virekebishwe kwa kuzingatia lugha ya kisheria na jedwali la marekebisho liwasilishwe Bungeni. Katika yaliyomo, yaani *table of contents*, maneno yote yapitiwe na kufanyiwa marekebisho. Alitaja sehemu namba nne, Kichwa cha Habari, sehemu namba tano kichwa cha habari, *natrition isomeke nutrition*. Katika sehemu ya ndani ya Muswada sehemu ya kwanza, utangulizi kifungu cha tatu, tafsiri ya maneno yaliyotumika yarekebishwe ili yaendane na lugha ya kisheria. Sehemu ya pili kifungu namba nne neno Tanzania's lisomeke Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanuzi ni kama ifuatavyo: Wizara imepokea mapendekezo na ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu masuala mbalimbali yaliyohitaji marekebisho. Marekebisho ya kiuchapaji katika Muswada huu yatashughulikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kulingana na Sheria ya Tafsiri, Sura Namba Moja, Toleo la 2002. Aidha katika sehemu ya tatu kifungu cha tisa kuhusu kuongeza kifungu cha ziada; Muswada umezingatia katika ibara namba 171 (3) katika mabano (i), (j), (l) na kifungu cha 6(a). Vilevile suala la mabadiliko ya tabia, yaani *climatic change*, lingeongezwa katika jedwali la marekebisho ibara ya 171 (3) (n). Suala la utoaji wa *notice* kama ilivyotajwa kwenye ibara 148 (c) limezingatiwa katika ibara 148 (3).

Sehemu ya tatu kifungu cha 9 kiwekwe kifungu cha ziada ili kujumuisha masuala yanayohusiana kama usalama wa kiafya katika uvuvi, madhara ya kemikali, uchimbaji wa madini, mabadiliko ya hali ya hewa, haya nimeshayazungumzia, makosa ya uchapaji yameshughulikiwa na marekebisho kwenye matumizi ya maneno yafanyike kama neno *may* na *shall* kwenye sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu 148 kuwepo na utoaji wa notisi ya maandishi kabla ya kufunga na kusitisha leseni ya kuendesha biashara, maduka na masoko, hiyo imezingatiwa kwenye kifungu kipywa cha 148 (c).

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dk. Ali Tarab Ali alisema Muswada umejikita zaidi katika viashiria na vyanzo vya maambukizi ya magonjwa mbalimbali kwa kujikita zaidi kwenye huduma za afya za Serikali za Mitaa. Masuala kuhusu usalama wa kemikali yaani *chemical safety* na kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari hayakuongelewa katika Muswada.

Alisema vilevile kwamba ni vyema sheria ya *Industrial and Consumers Chemicals Management Act* ya mwaka 2003, ikatajwa katika Muswada huu wa Afya ya Jamii wakati wa kuangalia usalama wa kemikali. Ufanuzi unaotolewa na Wizara ni kwamba sheria ya *Industrial Consumers Management Act* ya mwaka 2003 itaainishwa sambamba na sheria hii, aidha Muswada wa sheria hii umezingatia masuala ya usalama

wa kemikali na kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama ilivyo katika ibara ya 171 (6) na ibara ya 9 (1). Alisema pia katika tafsiri ya neno *nuisance* Kambi ya Upinzani inashauri kiongezwe kifungu kipy yaani *unpleasant to others*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Tarab atakumbuka kuwa hoja hii ilijadiliwa katika Kamati ya Huduma za Jamii ambaye na yeze ni mjumbe wakati wa kujadili Muswada na ikaonekana kwamba kuongeza maneno *unpleasant to others* itakuwa ni tafsiri pana ambayo inaweza kutoa tafsiri tofauti, hivyo haikujumuishwa kwenye marekebisho ya Muswada. Katika sehemu Na. 3. (a) *Notification of non communicable diseases*, Kambi ya Upinzani imeitaka Serikali moja kutenga kasma maalum ili kuanzishwa kwa vituo vya kufanyia mazoezi na (b) Kupiga marufuku uvutaji wa sigara katika sehemu za umma, sehemu za hadhara.

Majibu ni kwamba, katika sera ya afya ambayo ilidurufiwa mwaka 2007 na mpango wa mkakati wa 3 suala la magonjwa yasiyo ya kuambukiza yamepewa kipaumbele kwa mfumo uleule unaotumika katika magonjwa yanayoambukiza. Kwa hali hiyo yatatengewa kasma maalum kuanzia mwaka wa fedha ujao. Kwa upande wa uvutaji wa sigara katika maeneo ya hadhara, tukumbuke kwamba tulipitisha mkataba hapa Bungeni na kama mnavyojua mkataba hauna nguvu ya kisheria na kwa hivi sasa tumeshaandaa sheria ambayo tutaileta hapa Bungeni kwa hiyo yale maudhui yaliyokuwa katika mkataba tulioiptisha ndio yatapewa nguvu ya kisheria baada ya kanuni kutengenezwa.

Suala lingine kwa kifungu cha (9) ni kuhusu utoaji wa tahadhari ya magonjwa ya kuambukiza: Jedwali la kwanza limeweka utapiamlo ambao sio ugonjwa iongezwe *pesticide poisoning* katika jedwali la kwanza na *marginal note* ya kifungu cha 9 isomeke *Notification of infectious diseases and conditions*, agizo lake litazingatiwa katika marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliibua vilevile hoja ya matumizi ya fomu ya *PF 3* ambayo yamekuwa yanachelewesha upatikanaji wa matibabu na hata wakati mwingine kusababisha kupoteza maisha, hivyo Serikali iangalie upya suala la matumizi ya *PF3* ili mganjwa apatiwe matibabu kwanza ndipo taratibu nyingine za ujazaji wa fomu hizi ziendelee. Tunaahidi kwamba kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kulishughulikia suala hili ili kupata ufumbuzi wa kudumu. Lakini utaratibu uliopo ni kwamba mganjwa majeruhi anapokuja kwa kawaida anatibiwa na kuna wakati ambapo Polisi wanapigiwa simu wao ndio wanakuja na *PF3* inajazwa palepale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa katika ibara ya 73(7) adhabu ya shilingi 100,000/= au kifungo kisichozidi miezi mitatu au adhabu zote kwenda sambamba kwa mtu au Kampuni ambayo imeshindwa kuwapatia watumishi wake vitendea kazi kwa ajili ya kulinda afya zao. Aliona kwamba adhabu iliyotajwa katika Muswada huu ni ndogo sana, hivyo basi adhabu kali itolewe. Tumelizingatia hili lakini nilitaka kusema tu kiujumla, kwamba sheria nyingi katika afya za siku hizi ni za kuelimisha na

kuwabdalisha watu tabia, kwa hiyo zaidi tunalenga katika kuwabdalisha watu kuliko kuwapa adhabu.

Lakini kama tulivyosema tutawasiliana na Wizara ya Sheria ili kuhuisha sheria nyingine zilizopo hapa nchini isije ikawa hii sheria inaenda tofauti kabisa na adhabu zinazotolewa mahali pengine na kwa kawaida adhabu zitolewe kwa wale ambao hawaambiliki baada ya kuwafundisha, hao ndio tungependa kuwapa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 6 ibara ya 162 kifungu kinazungumzia shule na vyuo lakini hakizungumzii vyuo vya elimu ya juu, Msemaji alishauri ni bora vyuo vya elimu ya juu vikaingizwa katika kadha hii na ikibidi vile ambavyo vimekwishaanzishwa vikaguliwe upya ili viendane na matakwa ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa hoja atakumbuka kwamba katika *definition* ya *Institution* kama ilivyoletwa katika Muswada ulivyoletwa mbele ya Kamati ilikuwa inasomeka *Institution means Higher Learning Institution office, Hospital* na inaendelea na ikakubalika katika kikao hicho tuondoe *Higher* kwa sababu *Institution* itachukua shule zote kuanzia chekechea hadi chuo Kikuu, kwa hiyo sheria hii imezingatia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujibu hoja zilizotoka kwa Wasemaji Wakuu wa pande zote mbili sasa naomba nitoe mambo ya jumla kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia hoja hii, walizungumzia kuhusu uchafu wa mazingira, nimesikia habari za uchafu uliokithiri katika masoko yetu katika stendi za mabasi katika Hoteli suala nzima la kuchimba dawa, katika machinjio na kadhalika, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chaurembo alizungumzia pia kuhusu dampo ambalo lipo katika maeneo ya makazi ya watu, nimesema wengi wamezungumzia hapa Mheshimiwa Mhagama amelizungumzia, Mheshimiwa Chaurembo, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Lyimo na Mheshimiwa Lubeleje na wote walisema kwamba hii inatokana na elimu duni ambayo watu wetu wanayo na kukawa na wazo kwamba idara ya kinga iimarishwe na kitengo cha afya ya umma vilevile kiimarishwe na kwamba tabia ya watu ibadilike kwa sababu kulitolewa mfano wa mtu mzima ambaye anatupa takataka ovyo.

Kwa hiyo nasema kwamba nakubaliana na yote yaliyosemwa kuhusu mazingira na hii ndiyo sababu moja wapo tukaona itungwe sheria ya kuweza kudhibiti hali hii. Vilevile tutaimarisha kitengo chetu cha elimu ya afya, mambo mengi yanaweza yakazuilika kama watu wengi watakuwa na elimu inayofaa; hii itawafanya wawze kukwepa kupata magonjwa na matatizo mengi ya kiafya ambayo wanayapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na suala kwamba sheria zinatungwa lakini utekelezaji ni duni, Mheshimiwa Chaurembo yeye alisema kwamba sheria hazitekelezwi. Akaendelea kusema tuweke mazingira kwanza ndipo tutunge sheria akatoa mfano wa Vingunguti kwamba kule mahali wanakochinjia mifugo ni pachafu na hakuna sehemu nzuri, sasa tukitunga sheria namna hii itatekelezwa vipi. Masuala mengi haya yaliyopo katika Muswada wetu tunayajua na yamekuwa kero kwa wananchi, yanajulikana kuwa yanaathari kwa afya ya Watanzania lakini hatukuwa na sheria ya kuyashughulikia yaani tulikuwa tunaona uchafu lakini hakukuwa na mahali ambapo ungeweza kumbana huyu anayefanya uchafu au Halmashauri au watu wa machinjio. Ndio maana kukatokea haja ya kuwa na sheria ya namna hii ambayo tunaweza kuwa na kifungu cha kuweza kuwabana.

Tumeelezwa na leo tumejifunza kwamba wananchi wanaokwenda kutengenezwa kucha kwenye *salon*, kwenye *guest houses*, suala la kuchimba dawa, lakini wazoa taka ni watu waliosahaulika, wanafanya kazi katika mazingira magumu na kwamba katika eneo tunalozikia watu katika sheria tunasema ni lazima kuwe na choo lakini kwamba itatekelezwaje? Sijawahi kuona *cemetery* ambayo ina choo na kwamba MMAM ni *document* nzuri lakini kuna maeneo ambayo yanahitaji sheria hii kuweza kutekelezwa. Kwa hiyo kwa kutumia sheria hii tunaweza kudhibiti na kutekeleza mambo yaliyoainishwa katika vipengele mbalimbali.

Tumekumbusha pia kwamba hii sheria ni *cross cutting* yaani ni mtambuka na kwamba kuna umuhimu wa kufanya *coordination* ya hali ya juu. Ni kweli tunatambua baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa wametoa mifano ya barabara, mifano ya maji, kwamba kusipokuwa na maji itakuwa kazi bure kuzuia kipindupindu na maji hayapo. Tunakubali hilo na tunalichukua na utaona katika maeneo mengi tunasema kwamba kwa kushauriana na Wizara fulani suala hili lifanyike hivi na hivi. Hii yote inaonyesha kwamba tumeona *coordination* kwamba ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la malaria limezunguzwa sana na wajumbe wengi. Walisema hatutibu chanzo Mheshimiwa Mlata alisema madawa yanabadilika mara kwa mara na Mheshimiwa Degera alisema matumizi ya chandarua hayakutajwa. Labda niseme tu kwamba kuna programu kwa kila ugonjwa, hata hivyo kanuni, zitatayarishwa ili zielekeze nini cha kufanya kwa kila kipengele ambacho kinahitaji kufanyika. Haiwezekani utendaji wa kila eneo uwekwe kwenye sheria ndiyo maana kuna sehemu kubwa ya kanuni na Waziri mwenye dhamana amepewa fursa hiyo ya kutengeneza kanuni na hasa kwa mambo ambayo yanabadilika ikiwa kwenye sheria na unataka utende tofauti na vile ilivyozungumza kwenye sheria ni lazima hili suala liletwe hapa katika Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la vyakula na dawa ambavyo vimepitwa na wakati na vyakula ambavyo vinatoka nje na pia tulishauriwa kwamba tuone umuhimu wa kukagua na kufanya msako. Pia kulikuwa na suala kwamba wahalifu, yaani wale wanaokamatwa na vyakula ambavyo vimepitwa na muda wanapewa adhabu halafu wanaendelea kupeta tu. Labda niseme kwamba kitengo chetu cha *TFDA* ni moja ya wakala ambayo inafanya kazi kwa nguvu zote, haipiti mwezi mkasikia kwenye

vyombo nya habari kwamba wamekamata dawa, wamekamata vyakula vimeteketeza lakini sheria haishii hapo katika kuteketeza, kuna dhahabu zinazohusika wengine sijui kama wamewahi kufungwa lakini inakwenda mpaka huko na kufunga maeneo ya biashara. Tunachosema ni kwamba huo msisitizo tumeuchukua na tutaendeleza kasi ya utendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, limejitokeza pia suala la uhaba wa watumishi na limejitokeza hata kwenye swalii tulilojibu asubuhi, ni kweli watumishi ni wachache lakini kama tunafikiri sheria hii kuwepo ni kitu kizuri basi viende sambamba wakati tunajaribu kupata watumishi wa kutosha, hatuwezi tukasema tungoje tupate watumishi wa kutosha ndiyo tutunge sheria. Kwa sababu haitatokea tukawa na watumishi wa kutosha tunaongeza kwa jinsi muda unavyokwenda, wengi mnajua kwamba mikakati ambayo tumeipanga kwenye MAM na kama tulivyosema katika hii miaka mitatu toka awamu hii imeanza watumishi zaidi ya 11,000 wameajiriwa na tumepanua vyuo ili tuweze kupata watu zaidi katika kada yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wazo kwamba kuna vijana wengi waliomaliza *form four* ambao hawana kazi, kwanini hatuwatchukui? Nasema kwamba hivi sasa tunawachukua, mkumbuke kwamba kuna kada fulani ambazo zilikuwa zimefutwa kwa mfano *rural medical aids* au wauguzi kwa ngazi ya cheti hizo zote tumezirejesha, wakati tulikuwa tunachukua darasa la saba sasa tunachukua *form four*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ania Chaurembo, alisema kwa kuwa maradhi ya ugonjwa yamekuwa mengi, sheria hii isaidie kuhakikisha utekelezaji unakuwa makini, kamilifu na imara, usiwe kwenye vitabu tu. Alisema vilevile suala la mazingira hasa kuhusu maji taka na taka ngumu kuhusu uzoaji, usafirishaji na utupati uzingatie kanuni za afya na usalama wa watu, zisitupwe katikati ya makazi ya watu, mfano mabwawa ya maji taka Buguruni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa masoko na vyakula masoko mengi ni mabovu na machafu na bidhaa mbovu na nzima zinachanganywa na kuuzwa mfano wazi Dar es Salaam, hivyo elimu itolewe na ukaguzi na ujezi wa masoko ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na masuala yaliyosema kwamba sehemu nyingi za machinjio ni chafu ukiacha machinjio ya Dodoma, kwa mfano machinjio ya Vingunguti, na sheria zifanye kazi, sehemu za kujifungulia akinamama, vifaa, vyumba na vitanda ni vibovu vinachangia katika vifo nya akina mama na watoto. Kwa hiyo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa usimamizi uimarishwe na akasema vilevile kwamba adhabu ya shilingi 100,000 ni ndogo kwa kutotoa vifaa nya kujikinga, kwa mfano kama Kiwanda cha Samaki Dar es Salaam. Katika suala hili la adhabu, utakuta wengi hapa wamechangia kwamba 200,000 ni nyingi mno 100,000 ni ndogo mno lakini tutajaribu kuuhisha tukishirikiana na wenzetu wa idara ya sheria.

Sasa jibu la jumla kwa Mheshimiwa Ania katika hoja hizi alizotoa ni kwamba mengi yalikuwa mapendekezo ya kuimarisha na kutusaidia katika utekelezaji wa sheria hii na tutayazingatia kwenye kanuni ndogo za Halmashauri na kuimarisha ukaguzi.

Mheshimiwa Pindi Chana, alisema rasilimali watu ili iweze kutumika vizuri lazima iwe na afya, kwa hiyo sheria hii ihakikishe inasimamia vizuri haya. Hili tunakubaliana naye na tafsiri ya mamlaka ihusishe *Township, Municipal* na *City* pamoja na Wilaya na Miji. Tumeshauriana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu na ameshauri kwamba *definition* ya *authority* ibadilishwe isomeke kama ifuatavyo; *Authority means a district authority and urban authority as provided under the Local Government (District Authorities) Act and the Local Government (Urban Authorities) Act.* Katika *definition* ya *authority* inapendekezwa kutumia *definition* hii kwani ni pana zaidi kwa upande wa miji inajumuisha jiji na *township* na kwa upande wa *district* itajumuisha vijiji, vitongoji na mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ilitolewa hoja kwamba, sera ya huduma za kinga bure kwa watoto zisimamiwe vizuri vituoni, hasa alikuwa anazungumzia katika vituo vya kulelea watoto au vituo pale ambapo watoto hawakai na wazazi wao na hili litazingatiwa. Shughuli za usafi wa mazingira zitengewe sehemu maalum na usafirishaji wa taka uimarishwe, hili tutalizingatia. Katika suala la afya ya jamii sheria isisitize majukumu na wajibu wa jamii, Serikali na wadau mbalimbali, kwa mfano suala la kuwepo dampo na utumiaji wa dampo, hili tutazungumza na wenzetu wa Serikali za Mitaa kwa sababu wao ndiyo wenye maeneo sisi tunahusika katika kutazama usalama wa afya ya wananchi.

Kuimashwa kwa usafirishaji wa abiria kwenda sambamba na upatikanaji wa huduma ya vyoo vitakavyobinafsishwa, Halmashauri zisimamie, kuna kipengele kinachozungumzia na hasa ni katika suala zima la kuchimba dawa. Pia *summary conviction* isilenge kuongeza kipato bali kutekeleza sheria kupata afya bora na kwamba huyo anayetuhumiwa kwamba amekiuka sheria kabla ya eneo lake kufungwa basi apewe nafasi ya kujitetea na hilo limo katika sheria, anapewa siku thelathini katika muda huo kama hatarekebisha au kama hazitatokea juhudzi zinazoonekana kwamba amelifanyia kazi basi atajikuta kwamba ile adhabu inamshukia.

Mheshimiwa Susan Lyimo, alizungumzia habari ya tabia chafu ya watu kutupa taka hili nimelizungumzia na kwamba suala zima hili ni *cross cutting* na kwamba maeneo yaliyo katika sheria yaonyeshe nani atawajibika kufanya nini na hilo tutalizingatia kwenye kanuni. Alizungumzia pia kutopendezewa na usafi wa mazingira hali ilivyo kwa hivi sasa hilo tumelizungumzia na ndiyo aliyezungumzia kwamba malaria bado hatujatibu chanzo na akauliza kuhusu mafanikio ambayo wenzetu Zanzibar wameyapata kwamba kwanini isiwezekane huku Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumelizungumza hapa mara nyingi, ni kwamba kwa kutumia dawa hii ya ALU, pamoja na vyandarua pamoja na dawa ya ukoko kupuliza ndani ya nyumba, hiyo ndiyo imewafikisha wenzetu hapo walipo kwamba malaria sasa kule sio ugonjwa wa kutisha na sisi tayari tumeshaanza kutumia dawa ya ALU imepatikana na vilevile vyandarua tumeshazindua watoto walio chini ya miaka mitano wapate bure na akinamama wajawazito wanapata kwa bei pungufu, nia tunajiuliza

kwamba kwanini kila Mtanzania asitumie chandarua, kwa hiyo ndiyo masuala ambayo yanazungumzwa na kutafuta fedha za kutosha kwa shughuli kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupulizia dawa tuko katika mazungumzo na wenzetu wa mazingira sisi tumejiandaa na kwa dawa ambayo tuliipata kutoka Zanzibar tumeitumia katika Wilaya mbili na mafanikio yameonekana makubwa katika Wilaya ya Muleba na Wilaya ya Karagwe. Sasa hivi vifo na wagonjwa wamepungua sana mpaka tukienda huko wanatuuliza tulikuwa wapi siku zote, kwa hiyo mategemeo yetu ni kwamba, tutakwenda kwenye wilaya zingine zilizobaki hapa nchini kwa kuanzia na wilaya 26 ambazo zinapata milipuko ya malaria mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumzia kwamba *salon* ni mahali ambapo mtu unaweza ukapata ugonjwa kwa sababu *sterilization* ni ndogo na elimu ni ndogo, tunalichukua hilo kwamba elimu lazima iimirishwe na ndiye aliyezungumzia kwamba katika maeneo ya maziko hakuna vyoo na hakukuwa na sheria ya kuwabana hawa wenye kutunza hayo maeneo.

Mheshimiwa Blandes hakuwa na imani kwamba hii sheria inaweza ikatekelezwa lakini niseme tu kwamba tuipe nafasi, haikuwepo hii sheria kwa hiyo tuanze *with positive altitude*. Lakini mambo mengi aliyoyazungumza kuhusu mila nakubaliana nayo, kwamba tunapozungumza habari za kutenga eneo wakati yeye Mheshimiwa Blandes babu yake amezikwa karibu na pale anapoishi na yeye atazikwa karibu na eneo hilo hilo ni kweli inavyotokea katika maeneo mengi, kwa hiyo tutakapokuja kwenye kanuni hilo tutalizingatia.

Alizungumza vile vile kuhusu kujenga vyoo mahali pa kuchimba dawa. Akauliza swalii kwamba je, watoto wadogo akisikia haja akiwa ndani ya basi afanyeje au mzee. Lakini nadhani wengi wanaweza *waka-control*. Kweli kunaweza kukawa na dharura lakini utakuta wanaposema kuchimba dawa karibu watu wote wanatoka ina, maana wameweza kuvumilia kwa muda wa saa moja au saa mbili. Sasa itakapotokea dharura ya mtoto hiyo nadhani tunaweza tukai-*handle* kama dharura. Lakini hatuwezi tukasema kwamba haitatekelezeka kwa sababu mtoto mmoja ataanza kuhaarisha hiyo inaweza ikamtokea hata mtu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la maeneo ya kuchinjia mbuzi kule kijiji pia tutaangalia kwenye kanuni. Pia upimaji wa nyama na tukaulizwa kwamba je, tutakuwa na Bwana Afya kila kijiji? Mategemeo yetu ni kwamba tutakuwa na Bwana Afya wa kusaidia suala hilo.

Suala lililojitokeza mara kwa mara ni kwamba kutakuwa na mtu anatoka mjini kuja kupima hivi vitu na kutoa leseni za kutengeneza majeneza na vitu kama hivyo. *Authority* ina *definition* pana kama una *District Health Officer* ana watu wake hata Afisa Mtendaji wa Kijiji ni mtu ambaye anaweza akakasimiwa shughuli kama hizo. Kinachohitaji ni elimu tu.

Halafu tukaulizwa kwamba tunazungumza habari za *ventilation* kwa nyumba, wanasema labda hii sheria ni ya watu wa mjini. Lakini asubuhi wakati Mheshimiwa Degera anachangia alizungumza habari za nyumba kwamba michoro ya nyumba inazungumzia habari za miji je, sisi vijijini ndiyo tunaruhusiwa kujenga nyumba ambazo hazina ubora? Kwa hiyo, hapo utaona kwamba tunakoelekeea ni kila mmoja awe na nyumba ambayo ni nzuri na watu waelimishwe hivyo. Kwa hiyo, tunaposema *ventilation* hata kama ni nyumba ya msonge ni kwamba kuwe na dirisha. Hakuna aliyesema kwamba zilizopo itabidi zibomolewa zijengwe upya, lakini tunafundisha wananchi waelewe kwamba nyumba yenye *ventilation* nzuri ni nzuri kwa afya yake, kwa mambo mengi tu kama kifua kikuu na mambo mengine.

Pia ameshukuru kwa kuelezea suala la muziki na *nuisance* ingawa hatakubaliana na baadhi ya watu ambao wamenifuata wakati tulipopumzika saa saba kwamba wao wana-enjoy muziki wewe unakataza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Arfi aliuliza kwamba hii sheria inaweza ikatekelezwa, haamini kama inaweza ikatelezwa au wakati makazi ni holela, yanajengwa kiholela na Serikali imejiandaa vipi? Alizungumza habari za chanjo na matatizo yaliyotokea mwaka jana kule kwao pamoja na Morogoro na ye ye kwa *diagnosis* yake ni kwamba watu walioachiwa kuendesha zoezi hilo walikuwa hawana utalaam. Tumejifunza mengi kutokana na hilo na tutalizingatia. Vile vile akasema bila kuwa na maji ya kutosha tutakuwa hatufanyi lolote na hili limezungumzwa vile vile na Mheshimiwa Profesa Mtulia, ni kweli ndio maana tukasema sisi suala hili ni mtambuka. Wizara ya Afya peke yake haiwezi ikitimiza ni lazima tushirikiane na ku-coordinate na wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia pia mazalia ya mbu na kwamba tumesema kwamba mtu atakayekutwa na eneo linalo-*encourage* mazalio ya mbu huyu atepewa faini ya shilingi laki mbili na alipendekeza zaidi kwamba elimu itolewe. Elimu itatolewa na kwamba Sh. 200,000 ni nyingi labda itasaidia kumfanya asibweteke yaani asiache mazalia vinginevyo ataua wenzake kama hatakuwa ye ye watoto wake watakuwa. Lakini kwa kiasi gani tukiweke tutaongea na Wizara ya Sheria tuone kwamba inakwenda vipi kulingana na Sheria nyingine zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimegusia pia suala la majeneza kwamba kutengeneza hivi mpaka Mamlaka ihusike ndiyo tukasema tutaweka utaratibu kwamba tunaposema Mamlaka yanakwenda mpaka wapi na kwamba masoko hayakidhi matakwa na endapo hii Sheria ingeanza kutumika leo yote ingebidi yavunjwe. Sasa ni kweli kwamba tunaanza na masoko ambayo ni machafu na imani yetu ni kwamba Sheria hii ikitekelezwa tukawa na watu wa kutosha kama wasimamizi basi masoko yetu yatakuwa na unaifuu na hatuwezi kuacha kutunga Sheria kwa sababu sababu tunazo, tuna masoko machafu lakini tunataka yawe masafi. Kwa hiyo, sheria hii ndiyo inajaribu kulenga hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia alizungumzia habari za maji na umuhimu wake na elimu ya afya binafsi. Tunakubaliana naye kwamba ianze kwa mtu mmojammoja *then* inakwenda kwenye familia halafu ndiyo inakwenda hivyo.

kwenye jamii nzima na kijiji. Alituambia kwamba alipokuwa *Standard Four* alikuwa anafundishwa na kabla hujaingia darasani unaangaliwa kama una mikono michafu na unaweza ukapata kibano kama mikono ni michafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alisema kwamba Mabwana Afya siku hizi hawapo na niseme tu kwamba mwaka jana tulitunga sheria ya kuhusu Mabwana Afya lakini suala la Mabwana Afya kama Wataalamu wa Afya ni kwamba limechukuliwa pamoja na watumishi wengine wa afya. Kada ya *Health Assistants* ilifutwa kama Mheshimiwa George M. Lubeleje alivyosema lakini sasa tunairejesha kwa sababu ukiwapata hao wenye *diploma* ndiyo wagumu sana kuwapeleke vijijini. Ukiwa na *Health Assistants, Clinical Assistants* na *Nursing Assistants* hawa ni rahisi, tunapoongeza huduma hizi na kuzipeleka mbali na miji hawa ndiyo ambao tunawategemea kwamba watakubali maisha ya kuishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia pia alizungumzia habari za ujenzi kwamba hauko *supervised*, tutaongea na wenzetu wanaohusika na hilo na pia kwamba watumishi hawatoshi. Lakini pia alitupigia debe kwamba maslahi ya kada hii pamoja na ya Madaktari ni madogo kwamba mishahara ni midogo, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi amelisikia hilo. Pia alimalizia kwa kuzungumzia habari za malaria jinsi wenzetu Zanzibar walivyoweza kudhibiti na kwamba labda kuwe na wiki ya kuua mbu tuitenye wiki ya kuua mbu hilo tutalichukua na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kugusia masuala ambayo nilipata fursa ya kuyasikia wakati wenzangu wanachangia na niongeze tu kwa kushukuru kwa dhati kwa sababu yote yalikuwa mawazo na mapendekezo, machache yalikuwa yanatafuta ufanuzi, lakini yote tutayachukua na kuyazingatia na tunashukuru kwa sababu tunajua yatatusaidia katika utekelezaji wa Muswada huu ambao ningeomba muupitishe. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana! Hoja hii imeungwa mkono, sasa tulipokea orodha ya *amendments* zilizoandikwa asubuhi, sasa baada ya mjadala wa Waheshimiwa Wabunge kama kuna mambo ambayo mmeikubaliana na hoja za Waheshimiwa Wabunge basi tukifika kwenye *item* hiyo mtasimama na kusema hivyo kama kuna mahali ambapo mlikubaliana na maoni ya Wabunge wakati wanachangia hoja na yale ambayo hayamo katika *amendments* mlizogawa.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Shabani Kwaangw'!

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Kanuni ya 68 (7).

**NAIBU SPIKA:** Soma!

**MHE. OMAR S. KWAANGW’:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kanuni ya 92 inasema Muswada kama ulivyopitishwa na Bunge utatayarishwa chini ya uangalizi na usimamizi wa Katibu kwa kuingiza mabadiliko yote yaliyofanyika na atawasilisha nakala moja ya Muswada huo kwa Rais mapema ili Rais atoe kibali chake kwa mujibu wa Ibara ya 97(1) ya Katiba na pia nakala moja kwa Spika kwa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kupata mwongozo wako kidogo, ilitaka kulieleza vizuri lakini nilitaka kupata mwongozo zaidi kwamba tukishapitisha hapa Muswada Katibu atatayarisha na kuingiza mabadiliko chini ya uangalizi wake Muswada utatayarishwa, utatayarishwa chini ya uangalizi na usimamizi wa Katibu kwa kuingiza mabadiliko yote yaliyofanyika. Sasa nilitaka kujua wakati huo sasa wanapoingiza hayo mabadiliko je, Mwanasheria anahusika hapo kusema jambo lingine lolote? Maana ni kama nilimsikia Waziri kidogo kwamba yako mambo mengine ya marekebisho tuliyoyasema hapa yataingizwa baadaye na Mwanasheria Mkuu. Sasa nataka kujua Mwanasheria Mkuu ana nguvu yoyote baada ya sisi kupitisha hapa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Waziri anajumuisha alirudia mara nyingi tu kwamba atakwenda kuanisha na Sheria hii na Sheria nyingine, tulimnyamazia lakini wengine tulifikiri kabla ya kutunga ilitakiwa ianishwe hii na Sheria nyingine. Kwa hiyo, nilitaka kuamini kwamba hasemi kwamba tukitoka hapa anakwenda tena kuainisha na hizo Sheria nyingine halafu sijui iweje, kwa sababu nilitegemea kabisa kabla hawajafika hapa lazima walifanya maainisho hayo huko. Kwa hiyo, nilifikiri sikumwelewa lakini nikaona niache tu.

Kifungu cha 92 tunachokizungumza kwa mujibu wa Kanuni hizi zamani ilikuwa tukifanya mabadiliko hapa kwa sababu ya uchache wa Wataalamu wa Ofisi ya Bunge mabadiliko yale yanatolewa na Ofisi ya Bunge, yanakwenda kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali, inachukua muda mrefu pengine unaweza kusahau mpaka Rais anasaini inaweza kuchukua hata miezi mingine mingi. Sasa kwa mujibu wa Kanuni hizi mabadiliko yote tunayopata ni yale tunayopata hapa ndiyo maana nikamuambia kama hatuna mabadiliko yaliyokuwa humu na baada ya kuwasikiliza Wabunge katika mchango wao walipata muda mchana wa kwenda kushauriana huko na naamini wanasheria waliohusika na Muswada kwa upande wa Serikali walikuwepo huko, ndiyo nikasema tukifika kifungu hicho Waziri atasimama au Mwanasheria atasimama kwamba hapa tumekubaliana iwe hivi badala ya hivi ilivyokuwa humu ndani na yale tutakayofanya hapa ndiyo yatakayokuwa katika Sheria yetu na Ofisi ya Bunge itasimamia hayo na siyo vinginevyo.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ulivyosema ni sahihi lakini pia Sura ya Kwanza ya Sheria ya

*Interpretation of Laws* inampa Mwandishi Mkuu madaraka ya kufanya kitu chochote kinachoitwa *Topographical* yaani kusahihisha *Topographical errors*, ndicho Mheshimiwa Waziri alichokisema kwamba kama kuna matatizo yoyote ya kiuandishi na CPD atafanya masahihisho kufuatana na madaraka aliyonayo chini ya *Cap 1, Interpretation of Laws* ambayo inampa madaraka ya kufanya masahihisho ya *Topographical*.

**NAIBU SPIKA:** Kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 92 na tumeijadili katika Kamati ya Uongozi, hayo yatafanywa pamoja na Katibu wa Bunge siyo vinginevyo.

#### **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

#### **Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii Mwaka 2008 (The Public Health Bill, 2008)**

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

Ibara ya 5

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

Ibara ya 9

Ibara ya 10

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

Ibara ya 17

Ibara ya 18

Ibara ya 19

Ibara ya 20

Ibara ya 21

Ibara ya 22

Ibara ya 23

Ibara ya 24  
Ibara ya 25  
Ibara ya 26  
Ibara ya 27  
Ibara ya 28  
Ibara ya 29  
Ibara ya 30  
Ibara ya 31  
Ibara ya 32  
Ibara ya 33  
Ibara ya 34  
Ibara ya 35

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Ibara ya 36  
Ibara ya 37  
Ibara ya 38

(*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Ibara ya 39  
Ibara ya 40  
Ibara ya 41  
Ibara ya 42  
Ibara ya 43  
Ibara ya 44  
Ibara ya 45  
Ibara ya 46  
Ibara ya 47  
Ibara ya 48  
Ibara ya 49  
Ibara ya 50  
Ibara ya 51  
Ibara ya 52  
Ibara ya 53  
Ibara ya 54  
Ibara ya 55  
Ibara ya 56  
Ibara ya 57  
Ibara ya 58  
Ibara ya 59  
Ibara ya 60

Ibara ya 61  
Ibara ya 62  
Ibara ya 63  
Ibara ya 64

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 65

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 66  
Ibara ya 67  
Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 70  
Ibara ya 71  
Ibara ya 72  
Ibara ya 73  
Ibara ya 74  
Ibara ya 75  
Ibara ya 76  
Ibara ya 77  
Ibara ya 78  
Ibara ya 79  
Ibara ya 80  
Ibara ya 81  
Ibara ya 82  
Ibara ya 83

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 84

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

- Ibara ya 85
- Ibara ya 86
- Ibara ya 87
- Ibara ya 88
- Ibara ya 89
- Ibara ya 90
- Ibara ya 91
- Ibara ya 92
- Ibara ya 93
- Ibara ya 94
- Ibara ya 95
- Ibara ya 96
- Ibara ya 97
- Ibara ya 98
- Ibara ya 99
- Ibara ya 100
- Ibara ya 101
- Ibara ya 102
- Ibara ya 103
- Ibara ya 104
- Ibara ya 105
- Ibara ya 106
- Ibara ya 107
- Ibara ya 108
- Ibara ya 109
- Ibara ya 110
- Ibara ya 111
- Ibara ya 112
- Ibara ya 113
- Ibara ya 114
- Ibara ya 115
- Ibara ya 116
- Ibara ya 117
- Ibara ya 118
- Ibara ya 119
- Ibara ya 120
- Ibara ya 121
- Ibara ya 122
- Ibara ya 123
- Ibara ya 124
- Ibara ya 125
- Ibara ya 126
- Ibara ya 127

Ibara ya 128  
Ibara ya 129  
Ibara ya 130  
Ibara ya 131  
Ibara ya 132  
Ibara ya 133  
Ibara ya 134  
Ibara ya 135  
Ibara ya 136  
Ibara ya 137  
Ibara ya 138  
Ibara ya 139  
Ibara ya 140  
Ibara ya 141  
Ibara ya 142  
Ibara ya 143  
Ibara ya 144  
Ibara ya 145  
Ibara ya 146  
Ibara ya 147  
Ibara ya 148  
Ibara ya 149  
Ibara ya 150  
Ibara ya 151  
Ibara ya 152  
Ibara ya 153  
Ibara ya 154  
Ibara ya 155  
Ibara ya 156  
Ibara ya 157  
Ibara ya 158  
Ibara ya 159  
Ibara ya 160  
Ibara ya 161  
Ibara ya 162  
Ibara ya 163  
Ibara ya 164  
Ibara ya 165  
Ibara ya 166  
Ibara ya 167  
Ibara ya 168  
Ibara ya 169  
Ibara ya 170

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 171

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 172

Ibara ya 173

Ibara ya 174

Ibara ya 175

Ibara ya 176

Ibara ya 177

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati  
ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali 1

Jedwali 2

Jedwali 3

Jedwali 4

Jedwali 5

Jedwali 6

Jedwali 7

Jedwali 8

Jedwali 9

Jedwali 10

Jedwali 11

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na  
Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2008**  
*(The Public Health Bill, 2008)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Public Health Act, 2008* pamoja na mabadiliko yake kifungu hadi kifungu na kuukubali.

Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Public Health Act, 2008* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*  
*Mara ya Tatu na Kupitishwa*)

**NAIBU SPIKA:** Kama mtakavyoona Muswada huu una mambo mengi sana, kwa hiyo, kwa kweli itabidi Serikali iweze kuufanya kazi. Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo mwisho wa mchakato wa Muswada huu hapa Bungeni, kama tulivyosema kwa mujibu wa Kanuni ya 92 ambayo sasa inatoa nafasi kwa Katibu wa Bunge kufanya mabadiliko tuliyoyafanya, ila naomba *hard copy* ya huu Muswada tulionao pamoja na *soft copy* ambayo ni nakala tete wengine wanaita mgando. Kwa hiyo ni hivyo tu, tufanye ushirikiano kusudi sheria zetu ziwe hazikai kwa wingi kwa Rais mpaka mwishoni na ye ye anachoka kusaini. Tunafanya sisi wenyewe, sasa tuna kitengo kabisa na Mshauri wetu wa Kisheria yupo. Kwa hiyo, hayo ni mabadiliko nadhani Serikali tutafanya mapema kama ni *editing* na kufuatana na *Hansard* yetu ndiyo tunavyofanya sasa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo hatuna shughuli nyingine nashukuru tumemaliza kabla ya wakati, tulikuwa na wasiwasi juu ya ukubwa wa Muswada huu lakini nadhani tumeshiriki vizuri. Tunaomba Serikali iweze kuandaa maandalizi mazuri kwa sababu Muswada huu ni mageuzi, kwa maoni yangu nafikiri hata mengine yaandikwe kwa Kiswahili kwa sababu utawahu su wananchi wa kawaida, kwa hiyo ikiandikwa kwa lugha ya Kiswahili itakuwa ni vizuri zaidi. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 01.05 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,*  
*Tarehe 28 Januari, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)